**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 15 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**DUA**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *Assalaam Alaykum*?

**WABUNGE:** *Waalaykum salaam*.

**NAIBU SPIKA:** Bwana Yesu Asifiwe?

**WABUNGE:** Amina.

**NAIBU SPIKA:** Tumsifu Yesu Kristu?

**WABUNGE:** Milele, Amina.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mkutano wa 11, Kikao cha Tano.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, UTARATIBU NA BUNGE:**

Taarifa ya mwaka ya Kamisheni ya *UKIMWI* Tanzania

kwa Mwaka 2011/2012 *[The Annual Report of Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS) for the Year 2011/2012].*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 *(The Annual Report of the Bank of Tanzania, for the Financial Year 2011/2012).*

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji na Tathmini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mali ya Umma, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 *(The Annual Perfomance Evaluation of Public Procurement Regulatory Authority for the Financial year 2011/ 2012)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 34

### Ukamilishaji wa Ujenzi wa Vituo vya Afya Mufindi Kusini

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mtwango, Mninga, Mgololo na Bumilayinga katika Jimbo la Mufindi Kusini, haujakamilika:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Vituo hivyo ambavyo wananchi wamejitolea kujenga kuta?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati kwa sehemu kubwa huibuliwa na wananchi wenyewe. Kwa mantiki hiyo, aslimia kubwa ya gharama za utekelezaji wa miradi, zinatoka kwa wananchi wenyewe na wadau wa maendeleo. Halmashauri huchangia kiwango kidogo kwenye miradi hiyo, hasa kwenye ununuzi wa vifaa kama vile saruji, bati, mbao, nondo, na kadhalika na kutoa ushauri wa kitaalam na kusimamia ubora wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mtwango, Mninga, Mgololo na Bumilayinga, ni miongoni mwa miradi hii ya afya 21 iliyoibuliwa na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini, zikiwemo zahanati 17 na vituo vya afya 4. Miradi hii iko katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo kwa sehemu kubwa utekelezaji huu umechangiwa na nguvu za wananchi. Nawapongeza sana wananchi wa Wilaya ya Mufindi kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuibua miradi hii na kushiriki katika ujenzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Serikali, ilielekeza nguvu zake katika kujenga Hospitali ya Wilaya ya Mafinga, ili iweze kutoa huduma za rufaa kwa wananchi wa Wilaya hiyo. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013 Serikali, iliidhinisha shilingi 266.4 kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi *(*MMAM*)* kwa ajili, ya ujenzi wa Hospitali hiyo ambapo tayari Halmashauri imeshapokea milioni 90 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imeomba idhini ya shilingi milioni 420.5 kupitia MMAM, ili kuendeleza ujenzi wa Vituo vya Afya, Zahanati na Nyumba za Watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vituo vilivyotajwa hapo juu, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, imeshauriwa kuangalia upya vipaumbele vyake, ili fedha zilizotengwa kwa bajeti ya mwaka 2013/2014 viweze kutumika kuendeleza ujenzi wa vituo hivyo.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika,

nashukuru kwa majibu yaliyotolewa, lakini naomba Serikali, inithibitishie kwamba, hizi hela zilizotengwa ambazo ni milioni 420, zinaweza zikapelekwa kwenye vituo hivyo ambavyo tumevitaja kwa sababu, wananchi wale walishajenga kuta tayari na sasa hivi yale majengo yamekaa miaka miwili bila kuezekwa. Sasa naomba Serikali, inithibitishie kwa hili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwanza ambalo naanza nalo hapa, ni kumwomba Mheshimiwa Mendrad pamoja na Wabunge wenzake, watusaidie kupitisha bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, *that is the bottom line.* Kwa sababu, isipopita sasa maana yake ni kwamba, hii kazi haitaweza kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuthibitisha kwamba, hela hizi zitakwenda, sisi wote tunafahamu hapa kwamba, bajeti tunayokwenda nayo ni *cash budget* na hela haziwezi kwenda zote kwa mkupuo. Lakini nataka niseme kwamba, hapa katikati ukiangalia hata takwimu ambazo nimezitoa hapa, Serikali imeonesha kwamba inapelekea kwa kiasi kikubwa sehemu yote ya fedha ambazo zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nimthibitishie kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba, tutashirikiana naeye Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha kwamba, hela hizi ambazo tumezungumzia hapa, zinapelekwa katika hivyo vituo. Lakini sasa uangalie vizuri kwa sababu, katika hivi vituo ambavyo amevitaja hapa, nime-*check* na Mufindi, nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji, havikutajwa mle ndani. Viko vingine vimefika katika lenta, viko vingine ni kiwanja kimetengwa na kadhalika. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia tena vipaumbele vya Halmashauri upya, ili kuweza kusukuma hizi hela ziweze kwenda katika ule mpango, hayo ndio mawazo ambayo tunayo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu

Waziri, wananchi kwa kiasi kikubwa wanajitolea sana kujenga vituo vya afya na zahanati kwa nguvu zao wenyewe, lakini mara nyingi vikishakamilika Waganga na Wauguzi, inakuwa ni vigumu sana kuwapata. Kwa mfano, mimi nimechangia kwa 80% kujenga zahanati katika Kijiji cha Upendo, ambayo imekamilika miaka mitatu iliyopita, lakini mpaka sasa hivi hakuna Waganga. Je, Serikali, imejipangaje kuwapeleka Waganga na Wauguzi katika vituo hivyo vya afya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTUMISHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu tutaajiri Watumishi wa Afya wapatao 5,000 na vibali vyao vinatoka wiki hii kwa hiyo, kuanzia tarehe 1 Mei, 2013 watakuwa wameajiriwa watumishi wengi sana wa afya. Pia kwa mwaka ujao tumepanga kuajiri watumishi wa afya 11,000. Kwa hiyo, hiyo itakuwa ni faraja na sehemu nyingi, yaani kwa kiasi kikubwa tutawapeleka vijijini badala ya kuwarundika mjini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hizo ni habari njema sana asubuhi hii ya leo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido.

Na. 35

**Upelekaji wa Fedha Pungufu Katika Shule za Bweni**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Serikali, imekuwa ikitoa fedha pungufu katika shule za bweni zilizopo katika maeneo ya Halmashauri za Wafugaji, hali inayosababisha wanafunzi kukosa chakula na hivyo kutoroka shuleni:-

Je, tatizo hilo litarekebishwa lini, ili watoto wasome bila utoro?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, kwa kutambua mazingira ya shughuli za jamii ya wafugaji, iliamua kutoa huduma ya chakula kwa shule zote za bweni za msingi zilizoko katika maeneo hayo, sambamba na shule za sekondari za bweni za Serikali. Halmashauri ya Wilaya ya Longido, ni mojawapo ya Halmashauri zinazofaidika na mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Serikali, ilitoa fedha shilingi milioni 282, sawa na 100% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa shule za msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido na shilingi bilioni 1.5, sawa na 84.5% ya fedha zilizotengwa kwa shule za Sekondari. Kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 hadi kufikia mwezi Machi 2013, ilkuwa imeshatoa shilingi milioni 660 sawa na 97.5% ya fedha za chakula zilizotengwa kwa ajili ya wanafunzi wa bweni wa shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatoa huduma ya chakula kwa wanafunzi kupitia wazabuni ambao wameingia makubaliano ya kutoa huduma kwa kipindi chote cha mkataba. Malipo ya wazabuni yanafanyika kupitia fedha zilizotolewa na Serikali, kila mwezi kadiri ya makusanyo yanavyokuwa yamepatikana. Utaratibu huu unawezesha wanafunzi kupata huduma ya chakula muda wote wa masomo na wazabuni kulipwa kwa kuzingatia huduma iliyotolewa. Aidha, Serikali ipo tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, kupata taarifa za matukio ya utoro wa wanafunzi kwa kukosa chakula katika shule za bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali, inatoa fedha za chakula kwa shule za bweni kwa kiwango cha 1,500/= kwa mwanafunzi kwa kila siku. Mkakati wa Serikali, ni kuhakikisha kuwa, kiwango kinachotengwa katika bajeti kinatolewa kikamilifu, ili wanafunzi waweze kupata huduma ya chakula vizuri na hivyo, kuhudhuria masomo kama inavyotakiwa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali, kwa juhudi kubwa ya kununua chakula, lakini ningependa kuuliza; kwa vile, 1,500/= imepitwa na wakati. Je, Serikali, haiwezi ikaongeza sasa kiwango kufikia 2,500/= kwa sababu, vyakula vimepanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, kulikuwa na viporo vya wazabuni walikuwa wanadai huko nyuma. Serikali, iko tayari sasa kulipa viporo hivyo ili shule zisiwe tena na madeni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA *(TAMISEMI)*:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ni kweli, ukienda katika mambo ya *price index* na nini, ukicheki bei Kariakoo na masokoni, utaona kwamba, bei za vyakula zimepanda. Kwa hiyo, kwamba naweza nikasimama hapa nikapingana na Mbunge, kuhusu wazo hili analolileta hapa itakuwa sio sahihi. Ni kweli anachosema Mheshimiwa Laizer, lakini sasa kupanga ni kuchagua na uwezo wetu sisi kama Serikali, ni huu tunaouzungumza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunalipokea wazo la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, lakini kama tunavyosema bajeti ni mpango wa Serikali, unaoonesha jinsi hela zitakavyopatikana na namna zitakavyotumika, *that is the bottom line,* baada ya hapo unazipata wapi; nikijibu hapa, mzee huyu ataniuliza nimesikia umemwambia Lekule Laizer, zitapanda, utazipata wapi? Ataniuliza hivyo, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba, wazo hili tunalipokea kwa niaba ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulifanyie kazi, lakini kwa sasa hivi kiwango tunachotenga kwa ajili ya watoto walioko katika bweni ni sh. 1,500/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wazabuni ambao wamekuwa wanapeleka vyakula katika shule zetu na kwa upande wa Longido, ni kweli, anachozungumza Mheshimiwa Lekule Laizer, liko deni pale kubwa tu la karibu bilioni 1.4, lakini hili lilijitokeza kwa sababu, tulipoingia katika mpango wa ugatuaji wa madaraka, tulipeleka sisi katika Halmashauri zetu, madeni haya yanayozungumzwa na yale mengine ambayo mtataka kuulizia yalikuwa yamejitokeza wakati tulipokuwa katika Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachofanya sasa hivi ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, anawasiliana na Wizara ya Elimu na tumewaandikia, ili tuweze kwa pamoja kushurikiana kuwasiliana na Hazina, ili hawa wanaodai waweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tunataka kutoa ombi rasmi na maalum kwamba, wazabuni wetu wasiache kuwapa watoto chakula eti kwa sababu, hawajalipwa. Kwa sababu, tuko katika mpango huo wa kuhakikisha kwamba chakula kinapatikana kwa ajili ya watoto na fedha zinalipwa kwa ajili, ya hawa wazabuni.

Na. 36

**Vifaa vya Kutambua Mipaka Katika Ziwa Viktoria**

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA** aliuliza:-

Je, ni vifaa gani vinavyowasaidia wavuvi wetu kutambua mipaka kati ya Wilaya, Mikoa na Nchi ndani ya maji ya Ziwa Viktoria?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya Kitaalam inayotumika kutambua mipaka kati ya Wilaya, Mikoa na Nchi ndani ya maji ni ramani na vipimo vya alama za mipaka, zinazojulikana kama majira ya nukta *(Coordinates). Coordinates* ni vipimo vya kimahesabu vya upimaji vinavyoonesha umbali wa Kaskazini *(latitude)* na Mashariki *(Longitude)* pamoja na mwinuko kutoka usawa wa bahari, hivyo mvuvi au mtu yeyote anayesafiri ndani ya maji kwenye Ziwa Viktoria, anaweza kutumia chombo kiitwacho *Global Positioning System (GPS)* pamoja na ramani kutambua mahali alipo kwa kuona *latitude* au *longitude* ya sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki cha *GPS,* husoma majira ya nukta kwa kutumia mawimbi, yaani *signals* za *satellite,* ambapo humjulisha mvuvi mahali alipofika ndani ya maji. Mfano, anaweza kutambua mpaka wa Tanzania na nchi za Uganda na Kenya kwenye Ziwa Viktoria, uliko kwenye *latitude* moja, kusini mwa Ikweta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wetu na Kenya, unaanzia kwenye kisiwa cha Migingo na kuteremka kuelekea mashariki, eneo la kisiwa hicho kuna mawe yanayoonesha mpaka. Kwa mipaka ya Wilaya na Mikoa, wavuvi wanapaswa kuzingatia alama za asili zilizooneshwa kwenye tangazo la Serikali *(Government Notice),* lililoanzisha Wilaya au Mkoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusaidia wasafiri ndani ya Ziwa Viktoria na maziwa mengine nchini, Wizara yangu inaandaa ramani zenye kuonesha maumbo ya nchi *(Geographical Features)* na *latitude* na *longitude* zote, ili zitumike na wavuvi na wasafiri wengine kwenye maziwa

hayo. Ni matumaini yangu kwamba, wavuvi na wote wanaosafiri kwa vyombo vya majini mara kwa mara watajitahidi kujipatia ramani na *GPS* ndogo za mikononi, ili kuzitumia kuwaongoza wanaposafiri majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, natoa wito kwa Mamlaka za Leseni za Uvuvi na Usafiri Majini, wawe na utaratibu wa kutoa ramani ndogo kwa wote wanaopewa leseni za kutumia kwenye ziwa kwa mdhumuni mbalimbali.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nitoe pole kwa mvuvi wangu kule, juzi ameliwa na mamba na akawa amefariki. Kwa hiyo, natoa pole kwa familia ya marehemu Mchongo Simon.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Naibu Waziri, amekiri kwenye majibu yake ya msingi kwamba, kuna tatizo la kutowapa ramani wavuvi na *GPS,* lakini kwenye jibu lake anawaambia wavuvi kwamba, anatoa wito kwa Mamlaka zinazohusika. Nami suala la kutoa wito kwa Serikali, huwa ni kwenye Makongamano, Warsha na Semina. Kwa nini, asitoe agizo kama utendaji wa Serikali kama utendaji wa Serikali ili mamlaka zinazohusika wachukue hatua mara moja na sio wito unaohusu mambo ya makongamano na warsha? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa kuwa amekiri kwamba vifaa vya kuwasaidia wavuvi hawa majini ni tatizo hasa *GPS* hawana, hata alama za asili, ukiwa ndani ya maji wakati mwingine huoni unakokwenda na unakotoka na mara nyingi wavuvi hawa wakati wa doria Maafisa Uvuvi wamekuwa wanawakamata kule majini katika maeneo ambayo hawajui mipaka na kusababisha walipe ushuru wa leseni na leseni za uvuvi hata mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta risiti hii ni ya mwezi wa Pili, Wilaya ya Ukerewe; risiti hi ni ya mwezi wa Nne, Wilaya ya Ilemela na risiti hii ni ya mwezi wa Tano, Wilaya ya Bunda kwa mvuvi mmoja huyo huyo. Je, kwa nini Serikali isiwe na

utaratibu wa wavuvi hawa kulipa leseni moja kama tunavyolipa leseni za barabara, uwe unasafiri Muleba, Karagwe au Lindi ili kuondoa usumbufu wanaopata wavuvi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu rai yake kwamba, badala ya kutoa wito, ni vema tukaagiza, naamini kabisa kwamba, tunaposema tumetoa wito, maana yake, hiyo kwa Serikali itatekelezwa hivyo. Kwa maana hiyo basi, matarajio yangu ni kwamba *SUMATRA* ambaye ndiyo mamlaka ya usafirishaji majini, Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenye Wilaya zote zinazozunguka Ziwa Victoria, nazo ambazo ni mamlaka za leseni za uvuvi, wamepokea wito wangu na kwamba watatekeleza hilo, kwa kuhakikisha kwamba kila wanapotoa leseni ya kwamba, wewe tumekupa leseni ya uchukuzi basi itaandamana na ramani, tunakupa leseni ya uvuvi itaandamana na ramani ili kuepusha migogoro ambayo inatokea ziwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba, wavuvi wamekuwa wanalipishwa zaidi ya mara tatu kwa mwaka, akitoka hapa akienda pale anatozwa, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanatoka Ziwa Victoria ni kwamba, wavuvi wanashauriwa na mimi kupitia Bunge hili Tukufu nawashauri wavuvi, wanaposafiri ziwani wawe na hizo risiti walizotumia kulipia leseni zao, wakienda kwenye Wilaya nyingine ndani ya ziwa waonyeshe kwamba walikwishalipa ili wasidaiwe mara ya pili.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata Waheshimiwa Wabunge, ni swali la kuelekea Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na litaulizwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai ambaye simwoni hapa, badala yake litaulizwa na Kiongozi aliyeko leo Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, namwona Mheshimiwa Rose, uliza kwa niaba yake.

Na. 37

**Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo**

**MHE. ROSE K. SUKUM (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE)** aliuliza:-

Kuna mipango kadhaa ambayo ilibuniwa na Serikali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo kama vile mpango wa kusaidia uwekezaji mdogo na wa kati vijijini ambayo ilianza mwaka 2007 na inatarajiwa kwisha mwaka 2014, Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo ambayo ilianza mwaka 2007 na inatarajiwa kwisha mwaka 2015 na *program* ya kusaidia huduma za kilimo ambao ni mpango wa miaka 15 kuanzia mwaka 2008, pamoja na kuwa utekelezaji wa mipango hiyo unaendelea na mingine imeanza hivi karibuni:-

(a) Je, ni nini tathimini ya mipango hiyo kwa maisha ya wakulima na wafugaji kwa maeneo ilipotekelezwa?

(b) Je, mipango hiyo hadi sasa imetumia kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM kwa kipindi chote hiki, inatengeneza mipango mikakati inayoweka kipaumbele cha dira ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwenye sekta ya kilimo kama sekta mhimili wa Watanzania walio wengi kulingana na mazingira ya wakati

na yanayokwenda yakibadilika mara kwa mara. Mipango hiyo nayo inakwenda ikiboreshwa ili kuipa ufanisi na mafanikio ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hayo, Serikali ilianza kutekeleza *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme-ASDP*) mwaka 2006/2007. *ASDP* iliandaliwa kutekeleza sera kupeleka madaraka karibu na wananchi (*D by D*) kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans- DADPs*) ambayo huandaliwa na kutekelezwa katika ngazi ya Halmashauri kwa kuwashirikisha walengwa wenyewe. Mipango na miradi yote hiyo chini ya *DADPs* inasimamiwa moja kwa moja na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo imeonesha changamoto, lakini pia mafanikio kama ifuatavyo:-

(i) Kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji kwa hekta 135, 000;

(ii) Kuongezeka kwa uzalishaji na tija kwa zao la mpunga;

(iii) Ujenzi wa barabara za vijijini (*feeder roads*);

(iv) Ujenzi wa masoko ya mazao;

(v) Ujenzi wa maghala ya kuhifadhi mazao ya wakulima;

(vi) Ujenzi wa vituo vya wanyama kazi;

(vii) Ununuzi wa matrekta makubwa 413 na matrekta madogo 3900;

(viii) Ujenzi na ukarabati wa majosho;

(ix) Ujenzi na ukarabati wa malambo; na

(x) Ununuzi wa mashine mbalimbali za usindikaji na uanzishwaji wa mashamba darasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni ukarabati wa Vyuo vya Kilimo na Mifugo na Vituo vya Utafiti, Vituo vya Rasilimali vya Kata *(WARCs)*, kuongezeka kwa upatikanaji na matumizi ya pembejeo, kuboresha huduma za ugani na utafiti kwa kuongeza idadi, vitendea kazi na mafunzo kwa wataalam na kudhibiti milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya kiasi cha fedha kilichokwishatumika katika kutekeleza *program* na miradi hiyo hadi mwaka 2011/2012 ni jumla ya shilingi bilioni 630; ambapo kiasi cha shilingi 373.7 zimetumika kutekeleza miradi ya kilimo kupitia *DADPs*, shilingi bilioni 46 kupitia *DASIP*, shilingi bilioni 49 kupitia *PADEP* na shilingi bilioni 162 kupitia Wizara za Sekta ya kilimo ASLMs *(Agricultural Sector Lead Ministries)*.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, kwa kweli tunafahamu kabisa kwamba Watanzania nchini wapo takribani milioni 44, lakini katika majibu yake ya tathmini aliyoitoa inaonesha kwamba wakulima 680,159 ndiyo walionufaika. Je, hawaoni kwamba hizi fedha au huu mradi haukufanya kazi ipasavyo na fedha ni nyingi bilioni 630 na hela hizo zilitumikaje kwa Watanzania wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nataka kujua kwamba, kwa upande wa mifugo, ni mifugo ya aina gani iliyoboreshwa, kwa sababu nina uhakika kwamba, Watanzania wengi wafugaji wanahangaika na mifugo yao wenyewe wala hawakuboreka hata kidogo. Je, hiyo mifugo iliyoboreshwa ni ya kisasa au ni mifugo yote nchini kwa sababu ukiangalia Hanang hata hayo malambo ni hewa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya *ASDP* ni mapana kidogo, labda nirejee tu kwamba, katika kutathmini au kuweka takwimu za kilimo kwa wenzetu huko, jumla ya takwimu katika sekta ya kilimo ni pamoja na mifugo, uvuvi na kadhalika. Kwa hiyo, ndiyo maana hata nilipokuwa nataja miradi iliyokuwa chini ya *ASDP,* nimetaja miradi mingi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Rose ameniuliza kuhusu miradi *specific* ya Hanang ya ujenzi wa malambo. Nilichosema awali na wenzangu wa Mifugo wangekuwepo wangeweza kufafanua zaidi kwamba, pesa hizi za *ASDP* zimekwenda kwenye sekta ya mifugo, lakini pia zimekwenda kwenye sekta ya uvuvi na pesa zilizokwenda kwenye kilimo ni milioni mia tatu kama na sitini hivi na zimekwenda kupitia miradi ambayo inabuniwa huko huko kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kusema kweli kiwango cha ufanisi cha utekelezaji wa miradi ya *ASDP* ile inayofanywa kule kwenye Halmashauri, kimsingi inabidi tuulizane kule kule kwenye Halmashauri sisi wenyewe Wabunge na Madiwani. Lakini sisi kwenye Wizara ya Kilimo, kwa miradi ya kilimo, miradi ya kufuatilia ugani na miradi hii ya umwagiliaji, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza ameagiza kwamba, sekta ya umwagiliaji iende ikafuatilie chini ijue pamoja na kwamba pesa zile zimekwenda kwenye Halmashauri, lakini na sisi twende tukajue ni nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimthibitishie kwamba, kwa upana huo wa miradi hiyo, utekelezaji unakwenda vizuri na bilioni 630 sio ndogo kama zikipatiwa utekelezaji wenye ufanisi na ndiyo maana tumejipanga kwamba, tushuke chini twende tukasaidiane na Halmashauri kwa kuwasiliana na TAMISEMI Makao Makuu ili tupate ufanisi wa utekelezaji wa pesa hizi kwa maana ya *value for money*.

Na 38

## Kasoro za Mfumo wa Stakabadhi Ghalani (Stakabadhi za maghala)

**MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA)** aliuliza:-

Katika kipindi cha 2010/2011 imedhihirika kuwa mfumo wa stakabadhi za ghalani umekuwa na kasoro na matatizo mengi kwa wakulima hasa wa korosho na ufuta kama vile ucheleweshaji wa kupata malipo ya mwisho ya wakulima na kuathiri sana mipango ya huduma za kijami na urejeshaji wa mikopo ya benki kwa wakulima wa mazao hayo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuviagiza Vyama vya Msingi vya Ushirika kuacha kukopa mazao ya wakulima kupitia mfumo huo, badala yake wawalipe wakulima bei kamili iliyopo sokoni?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwaacha huru wakulima wa korosho na ufuta wauze mazao yao kwenye soko wapendalo badala ya kuwalazimisha wauze kwenye Vyama vya Ushirika tena kwa kukopesha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali la kuanzisha mfumo wa stakabadhi za maghala ni kuweka utaratibu ambao unawawezesha wakulima kupata bei nzuri, ambapo katika utaratibu huo mkulima hulipwa wastani wa asilimia 60 bei ya dira na baada ya mazao yao kuuzwa wakulima hulipwa asilimia iliyobaki. Hivyo, katika mfumo stakabadhi za maghala hakuna dhana ya Vyama vya Ushirika

kuwakopa wakulima mazao yao bali ni utaratibu ambao unaruhusu wakulima kulipwa sehemu ya bei ya mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, pamoja na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi za maghala bado mfumo huo umekuwa na mafanikio pale ambapo kumekuwa na usimamizi madhubuti wa mfumo huo.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia sera ya soko huria ina wajibu wa kuandaa mazingira ya kuwawezesha wakulima wa mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na korosho na ufuta kuyauza kwenye soko kwa kutumia taasisi zao vikiwemo Vyama vya Ushirika ambavyo vipo karibu na maeneo yao.

Hata hivyo, ni wajibu wa Serikali kuwalinda wakulima wadogo wasinyonywe na wanunuzi/walanguzi kupitia bei ndogo vipimo visivyo rasmi na uharibifu wa ubora ambao unafanya bei kushuka na kuathiri bei ya mazao yao kwa ujumla. Ni vyema wadau wote tukajielekeza katika kuimarisha taasisi za wakulima ili visaidiwe katika umoja wao kuongeza ubora wa mazao na kujielekeza katika kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni vyema sote tukatambua kwamba mfumo wa stakabadhi ghalani ulikuja kupambana na mfumo sugu uliokuwepo ambao ulikuwa unawakandamiza wakulima na kutengeneza faida kubwa isiyo na uhalali kwa wachuuzi na walanguzi. Mafanikio ya mfumo huu maana yake ni kupungua kwa mapato haya kwa watu hawa.

Hivyo basi, wakati tukifanya tathmini ya mafanikio na changamoto za mfumo huu wa stakabadhi ghalani ni vyema tusiache kutambua kwamba kuna watu wenye uwezo mkubwa na wasioutakia mema mfumo huu ambao wako tayari kwa jitihada kubwa na kutumia fedha kuufanyia hujuma.

**MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ambayo ndani yake yanawafurahisha zaidi wafanyabiashara kuliko wakulima, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hadi sasa kuna baadhi ya wakulima ambao hawajalipwa fedha zao na baadhi yao wamelipwa nusu tu ya fedha zao, mfano mwingine, ni wa pale Rufiji. Je Serikali ina kauli gani kwa wananchi hao ambao wanategemea mazao hayo kwa ajili ya kuendesha maisha yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba, mfumo huu ulileta mafanikio pale ambapo kulikuwa na usimamizi madhubuti. Usimamizi ni baina ya Serikali na wale walengwa. Je, kwa kuwa malalamiko yamekuwa mengi juu ya suala hili, Serikali ina kauli gani kwa wananchi na kuna njia gani mbadala katika suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme dhahiri kabisa kwamba, majibu yangu hayalengi kuwafurahisha wafanyabiashara, wachuuzi na walanguzi kwa sababu mfumo huu kimsingi umejielekeza kupambana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kabisa na mimi ni mdau wa mfumo huu, lakini pia ni muathirika wa mambo haya yanayotokea ndani ya mfumo huu wa stakabadhi ghalani. Miaka mitatu iliyopita sisi wakulima wa korosho tulipata bei nzuri sana, lakini baada ya hapo, watu wamekwenda wakakoroga na wengine tuliokoroga tumo humo humo ndani ya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba, tulijipanga, kwanza kabisa kufanya tathimini na tumeshafanya, ushirika umeshafanya tathimini kujua, wale wakulima ambao wametoa zao lao wakapewa 50%, wengine hawajapewa hata senti tano, lakini wanaonesha kupewa vikaratasi vya kuonesha kupokea lile zao, watuhumiwa ni nani? Mara nyingi watakuwa ni Viongozi wa Ushirika au wajanja wengine au watendaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametukabidhi mimi, Mrajisi na Katibu Mkuu, tumelifuatilia, tuna orodha ya watu na tunatarajia kama Vongozi wa Vyama vya Ushirika hawatakwenda Mahakamani kwa kupelekwa na wanaushirika wenyewe, basi Serikali itawapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la usimamizi madhubuti, nimesema kwamba, kwenye mfumo huu, sisi sote tunashirikiana kwa kutegemeana na zao lenyewe. Kama ni kwenye korosho ni sisi Serikali, Bodi, Viongozi wa Mkoa na Viongozi wa Wilaya. Sasa kama hapo katikati kutatokea atakayejaribu kuchezea mfumo huu kwa kuwaumiza wakulima, ataharibu ufanisi wa mfumo wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasema, mfumo huu umedhihirika kwamba, unawapatia wakulima bei nzuri, lakini inabidi sisi wote tuwajibike.

Vile vile naomba nikuhakikishie tu Mheshimiwa Rajabu na Waheshimiwa Wabunge, hasa wale wanaotoka kwenye mazao ambayo yana mfumo wa stakabadhi ghalani, tutapambana nao tu hawa watu wanaoharibu mfumo huu, hatuwezi kuwaachia waendelee.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa kulikuwa na mtikisiko wa kiuchumi duniani na wafanyabiashara wengi waliathirika hasa katika nchi yetu, maeneo ya Mikoa ya Kaskazini kule Arusha na maeneo mengine kulikuwa na ukame ambao uliathiri wafugaji wengi na Serikali ilichukua hatua madhubuti kwa kuwapa ruzuku waathirika wa wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wakulima wa korosho wameathirika sana ndani ya mfumo huu mbovu wa stakabadhi ghalani. Je, Serikali ipo tayari sasa kufanya kama vile ilivyowafanyia wafanyabiashara na wafugaji katika maeneo mengine kwa kuwapa ruzuku zao katika athari ambayo iliwakuta?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mtu yoyote atakayesimama akauita mfumo wa stakabadhi ghalani ni mfumo mbovu, basi ama yupo kwenye upande, maana lazima tutambuane. Mfumo wa stakabadhi ghalani umekuja kuwanusuru wakulima na umefanikiwa kufanya hivyo kwa awamu hadi hapo wajanja walipoingia na kuufanyia ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu akiuita mfumo mbovu ama yupo upande mmoja ama ule mwingine, lakini nachelea kwenda huko kwa sababu Mbunge wa Lindi anajua, kwamba, mfumo huu sisi wakulima wa korosho umetupatia manufaa, lakini unahitaji usimamizi na udhibiti wetu sisi wote. Bahati mbaya sana wengine kati yetu sisi viongozi, tuna maslahi na kuharibika kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nirudie kusmea wazi kabisa kwamba, mfumo wa stakabadhi ghalani ukienda vizuri unawapatia manufaa wakulima, tukichanganya na uwezo wa kuongeza thamani utawapatia manufaa zaidi. Kwa hiyo, naomba niseme kabisa, huu mfumo wa stakabadhi ghalani tumejipanga kuudhibiti na watakaoingia katikati yetu hata ukiwa kiongozi ama Mbunge mwenzetu, utaumia tu mzee.

Na. 39

**Kuendeleza Kitengo cha Afya ya Akili**

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR (K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI)** aliuliza:-

Kitengo cha Afya ya akili cha Hospitali ya Muhimbili kilichopo Chamazi – Mbagala Wilayani Temeke ni chakavu sana na hakina maendeleo yoyote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya ya Akili kilichopo Chamazi - Mbagala katika Manispaa ya Temeke ni sehemu ya Idara ya Afya ya Akili ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambacho kilianza kutoa huduma mwaka 1986. Kituo kina uwezo wa kuhudumia wagonjwa 32. Kinatoa huduma za utengamao wa akili kwa wagonjwa ambao wamepata nafuu baada ya kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo kilifanyiwa ukarabati kwa mara kwanza mwaka 2008, ukarabati uliohusisha upakaji rangi, kuweka umeme na kuchimba kisima cha maji. Ukarabati uligharamiwa kwa uhisani wa Daktari kutoka Ireland aliyekuwa anachukua mafunzo ya uzamili, fani ya Afya ya Akili Muhimbili aliporejea kwao. Kwa sasa kituo kina uwezo wa kuhudumia wagonjwa saba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali uliopo ni kufanya ukarabati wa jengo moja na wodi ya wagonjwa ili kuongeza idadi ya wagonjwa wa huduma za utengamao kutoka saba (7) hadi 15. Ili kutekeleza azma hii, jumla ya shilingi milioni 20 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014. Aidha, mpango muda mrefu wa Serikali ni kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya mapitio na tathimini ya kituo ili kutoa mapendekezo jinsi ya kukamilisha ukarabati wa majengo na kuendeleza eneo lote la kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vingine vinavyotoa huduma ya namna hiyo ni kituo cha Hombolo, Dodoma ambacho ni sehemu ya Hospitali ya Mirembe na Rutindi kilichopo Wilayani Korogwe ambacho kinamilikiwa na Shirika la Dini.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, ujenzi huo wa ukarabati wa jengo moja ambalo litaweza kuchukua wagonjwa kumi na tano unatengemewa kuanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mshauri huyo, ameshaanza kazi na kama ameshaanza kazi anategemea kutuletea ushauri huo kipindi gani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza hapa, hizi milioni 20 tumezitenga katika bajeti ambayo itapitishwa hapa ya mwaka 2013/2014. Kwa hiyo, tunatumaini kwamba, hela hizi zikitoka sasa ndizo zitakazokwenda kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niweke vizuri tu, hili swali linalouliza hapa ni kweli kwamba, kituo hiki kinaonekana kwamba kiko katika hali hiyo. Kituo hiki hakitibu wagonjwa, kituo hiki ni kipindi cha mpito kuelekea nyumbani. Yaani unampeleka mgonjwa pale kumwangalia asije akatoka moja kwa moja kule akaenda akampiga mwenzake kisu, akafa huko, ndiyo ukajua kwamba kumbe huyu mtu alikuwa hajapona.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kukagua kituo hiki ili kuangalia kwamba ni kiasi gani cha fedha kinatakiwa kwa ajili ya ukarabati wote, ndiyo tukaona ni shilingi milioni mia mbili na hamsini. Ndiyo maana sasa Wizara, Mheshimiwa Waziri wa Afya akaamua amtafute sasa Mshauri Elekezi ili akaangalie haya yote. Akishaleta sasa ndipo Serikali ichukue hiyo changamoto, ione kwamba itafanyaje ili kuhakikisha kwamba, kazi hiyo itafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwamba, hela hizi milioni ishirini zikitoka, zitafanya kazi hiyo, lakini na

huyu Mshauri Elekezi naye atakapotoa taarifa sasa ndipo Wizara itakapoanza kufanya kazi, kuona kwamba kitakarabatiwaje chote.

Na. 40

**Utengenezaji wa MV. Liemba**

**MHE. DAVID Z. KAFULILA** aliuliza:-

Tangu mwaka 2009 Serikali ya Ujerumani ilionesha nia ya kutengeneza upya meli ya *MV.* Liemba kama fahari ya ushirikiano wa kihistoria baina ya nchi hizi mbili na hivyo kutaka ushirikiano na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya utekelezaji:-

Je, Serikali imekwama wapi katika utekelezaji wa jambo hili?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haijakwama kutekeleza mpango wa kukarabati wa meli ya *MV.* Liemba. Serikali ya Shirikisho la Ujerumani imekubali kuikarabati meli ya *MV* Liemba kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Jimbo la *Lower Saxony* ambako ndiko meli ilikojengwa, Wajenzi wa *MV.* Liemba, Kampuni ya Saruji ya Twiga *Cement* ambao ni wawekezaji kutoka Ujerumani na marafiki wa Liemba watachangia ukarabati wa meli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa ni kwamba, wakaguzi kutoka Ujerumani watafanya ukaguzi wa

*MV.* Liemba kuanzia tarehe 22-27 Mwezi huu (*April*, 2013). Madhumuni ya ukaguzi huo ni kujua hali ya Meli ilivyo kwa ujumla (mwili, mkuku wa meli, mitambo na sehemu zingine zote) na kubaini gharama zote za matengenezo zinazohitajika. Tunatarajia ukarabati wa *MV.* Liemba utaanza baada ya ukaguzi huo.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, ninayo maswali mawili ya nyongeza kwa sababu, moja ya tatizo kubwa la Serikali hii, ni uwezo mdogo wa ku-*respond* matatizo yanayojitokeza katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la Liemba, Ujerumani ilitoa taarifa tangu mwaka 2009 wako tayari kukarabati ili kusudi kwenye maazimisho ya mwaka 2013 ambapo meli hii itatimiza miaka mia moja, mpango huu uwe tayari, lakini mpaka leo ndiyo tunaambiwa wame-*respond* hao wajerumani waje kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kupata majibu ya swali ambalo nimeuliza, ni kwa nini Serikali imechelewa ku-*respond application* ya Ujerumani kuikarabati Meli ya *MV.* Liemba tangu 2009 mpaka 2013 ndipo inakwenda ku-*respond?* Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, usafiri wa Ziwa Tanganyika kimsingi kwa sehemu kubwa umesahauliwa na Wizara hii. Pale Ziwa Tanganyika kuna Gati Kigoma Kaskazini na Kigoma Kusini, Gati ile Mkandarasi tangu mwaka 2009 alijaribu kujenga baadaye akashindwa; amepotea na Naibu Waziri alikuwepo mbele ya Waziri Mkuu tukiwa kwenye Mkutano wa Kanda, Waziri Mkuu akaelekeza hatua zichukuliwe. Ningependa kupata majibu ya Serikali, mpaka sasa Gati za Kusini na Kaskazini kwenye Ziwa Tanganyika zimefikia hatua gani, kuhakikisha kwamba tunapata gati hizi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sio kweli kwamba, Serikali haiuku-*respond* kwa wakati

kuhusu *offer* iliyotolewa na Serikali ya Ujerumani kuhusu matengenezo ya hii Meli ya *MV*. Liemba. Wakati Serikali ya Ujerumani inaleta *offer* hiyo, Serikali ya Denmark kupitia *DANIDA* na wao pia walikuwa wame-*offer* kufanya utafiti kuhusu kiasi cha matengenezo kinachohitajika katika Meli tano zinazomilikiwa na kampuni ya *Marine Services*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwanza waliachwa wale *DANIDA* wafanye huo utafiti wa kiwango cha uharibifu kilichoko katika hizo Meli, halafu watoe mapendekezo kwa Serikali. Baada ya hapo, wao *DANIDA* walisema kwamba, *MV.* Liemba kwa maoni yao, haifai tena kutengenezwa kwa matumizi ya abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndiyo sasa tukawaambia Wajerumani waendelee na *program* yao kwa sababu wao kimsingi wanataka kuifanyia matengenezo, siyo kwa maana ya kusafirisha abiria isipokuwa tu kwa kuifanya iwepo kama *antique* ama chombo ambacho kimetumika, kimekuwa na manufaa makubwa, kwa hiyo, hakifai kupotezwa. Ndiyo maana muda huu ukapita. Sasa tuko *full fledged DANIDA* watendelea na *program* yao ya meli nyingine na Wajerumani kupitia haya mashirika niliyoyataja watafanya ukarabati wa hii *MV.* Liemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Gati katika Ziwa Tanganyika, ni kweli nakubaliana kabisa na Mheshimiwa David Kafulila alivyosema kwamba, kumekuwa na uchelewashaji wa ukamilishaji wa Magati matano yaliyokuwa yajengwe katika Ziwa Tanganyika. Magati hayo yamechelewa kwa sababu ya mwenendo mbaya wa usimamizi uliokuwepo katika Mamlaka yetu ya Bandari na Mkandarasi mwenyewe kuwa mdhaifu katika utekelezaji wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa maelekezo kwa ajili ya hatua za kuchukua. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatua hizo zimechukuliwa, wajenzi tumewapeleka Mahakamani.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kutokana na ajali nyingi za Boti katika Ziwa Tanganyika na vifo vya wananchi vinatokea kila mara. Kwa nini shirika lako lisiongeze hiyo Liemba *trip* ya pili hata kuishia Bandari ya Kipili ili kupunguza vifo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii *MV* Liemba inafanya safari mbili kwa mwezi. Kwa takwimu zilizopo, moja kati ya hizo safari mbili inazofanya kwa mwezi, *MV.* Liemba inapata hasara. Tumejaribu ku-*adjust* hizo ratiba ili kuoana na msimu wa uvuvi wenye faida, lakini bado safari moja kati ya hizo mbili inakuwa ya hasara. Hivyo, kuongeza safari ya tatu, kutazidi kulididimiza zaidi shirika letu la *Marine Services*. Tumewaomba tu kwamba wawe wanakadiria msimu ambao unakuwa na mizigo na abiria wa kutosha *then* wanafanya safari hizo badala ya kuongeza safari ambazo wakati mwingine wanaweza kwenda na kurudi bila ya kupata abiria.

Na. 41

**Vipaumbele vya Ukarabati wa Reli na Bandari**

**MHE. ISMAIL A. RAGE** aliuliza:-

Je, Serikali imepanga vipaumbele vyovyote kuhusu ratiba ya ukarabati na ujenzi wa Reli za nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Miaka Mitano, yaani 2011/2012 – 2015/2016, Serikali imeanisha vipaumbele mbalimbali vya ukarabati wa reli ili kurejesha huduma katika hali ya kuridhisha. Kwa kuzingatia ratiba ya ukarabati, Serikali imepanga kufanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuondoa reli nyepesi za ratili 56.12 kwa yadi na chakavu kati ya Itingi na Tabora na kutandika reli zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi. Hivi sasa Mkandarasi yupo eneo la mradi na kazi inaendelea.

(b) Kukarabati madaraja mabovu na kuyaongezea uwezo wa hadi kufikia uzito wa tani 25 kwa ekseli (25 *tones Axle load)*. Hivi sasa ujenzi wa madaraja matatu kati ya Kilosa – Gulwe (kwenye umbali wa kilometa 293 na Kilometa 303) na Bahi – Kintinku (kwenye umbali wa kilometa 517), unaendelea.

(c) Kuondoa reli nyepesi ratili 56.12 kwa yadi kati ya Dar es Salaam mpaka Munisagara, umbali wa kilometa 298 na kutoka Malongwe – Tabora – Isaka (kilometa 240) kwa kuondoa reli nyepesi ya ratili 60 na 56.12 kwa yadi. Aidha, kutandika reli nzito za ratili kati ya 80 na 95 kwa yadi kati ya Tabora – Kigoma umbali wa kilometa 411, kwa kuondoa reli nyepesi za uzito wa ratili 56.12 kwa yadi.

(d) Kukarabati njia ya reli kutoka Tanga – Arusha, na kuanzia Ruvu – Mruazi, kutoka Kilosa hadi Kidatu na ile ya Kutoka Manyoni – Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda mrefu ni ujenzi wa reli ya Kati na matawi yake kwa kiwango cha kimataifa.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kwanza kutoa taarifa fupi, Mkoa wa Tabora kuanzia jana umetengwa na nchi nzima kwa barabara zote kuchukuliwa na maji. Kwa hiyo, hakuna gari inayotoka Dar es Salaam au Itigi kwenda Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maswali yangu mawili ya nyongeza; Tabora ni katikati ya Reli za kwenda Mwanza, Kigoma, Mpanda na Dar es salaam. Je, ni lini Serikali itahakikisha inawekeza kwenye karakana zake kama

ilivyokuwa wakati wa *East African Community*? Kulikuwa na karakana kubwa Nairobi ya pili ilikuwa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, ni lini Karakana za Tabora zitapelekewa vipuri kwa sababu pale hakuna kipuri hata kimoja? Shahidi nilikwenda na Waziri, Mheshimiwa Mwakyembe alishituka sana alipoona yeye mwenyewe pale.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *station* ya Tabora ipo katikati au njia panda ya reli yetu ya kati kwa maana ya kuelekea Kigoma, Mpanda na Mwanza. Serikali inatambua sana umuhimu wa karakana hiyo. Kwa hiyo, katika bajeti zetu zote, tunaweka fedha kwa ajili ya kuimarisha karakana zote kuu tatu zinazomilikiwa na shirika letu la reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya umuhimu wa sehemu hiyo ya Tabora kwa kuhudumia treni zinazokwenda Mpanda, Kigoma na Mwanza, kipaumbele mahususi kitawekwa kuhakikisha kwamba Karakana ya Tabora inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini vipuri vitapelekwa kwenye karakana hii ya Tabora; niseme tu kwamba, baada ya kubaini upungufu uliopo na kubaini pia kwamba vipuri vingi baada ya kutenganisha *RAHCO* na *TRL*, vilibaki mikononi mwa *RAHCO,* nilikwishatoa agizo na nadhani limetekelezwa, vipuri vyote vilivyokuwa katika karakana ya Morogoro chini ya *RAHCO* wapewe Shirika la Reli, Tanzania *(TRL)* na wao wavisambaze katika Karakana zote hizi tatu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujakwenda kwenye swali la mwisho la Wizara ya Katiba na Sheria, niwape picha tu, kwa kweli swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage lilivyotungwa, ndiyo maswali ya Kibunge yanavyotungwa. Kwa hiyo, nimpongeze na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wengine kuiga utaratibu huu, hakuna haja ya kuandika gazeti, katika kuuliza swali.

Swali la mwisho la leo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya!

Na. 42

**Mahakama Kutumika Kuvunja Haki za Wananchi**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Mahakama ni chombo cha kutoa haki za watu na mali zao:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu chombo hiki kutumika kama sehemu ya kupoteza haki za Watanzania na mali zao?

**MHE. NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Madgalena Hamisi Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu, Mahakama ndiyo chombo chenye Mamlaka ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kutimiza wajibu wake, Mahakama hutoa haki kwa kufuata misingi ya sheria zilizotungwa na Bunge lako Tukufu. Hivyo siyo kweli kwamba, Mahakama hutumika kama sehemu ya kupoteza haki za Watanzania na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo kuna shauri ambalo Mheshimiwa Mbunge anaona haki haikutendeka ipasavyo katika Mahakama yeyote ile, bado kuna haki ya kisheria ya kwenda kwenye Mahakama ya juu ya hapo kwa njia ya rufaa au masahihisho.

Aidha, namwomba Mheshimiwa Mbunge anipatie jina la Mahakama anayoituhumu kutumika kupoteza haki za Watanzania na mali zao na shauri husika ili tuweze kufanya uchunguzi na kuchukua hatua. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki kimekuwa kikitumiwa na baadhi ya watu binafsi, Taasisi na hata Serikali yenyewe kuzima hoja za msingi pale panapotokea kutokuelewana, kutokuridhika na hata madai ya watu. Tumeshuhudia Serikali ikikimbilia Mahakamani kwenda kuzima hoja za madai ya Walimu walipotaka kuandamana kushinikiza kulipwa haki zao. Je, chombo hiki hakioni kukubali mambo kama haya ni kupoteza hadhi yake ya kimsingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa haki iliyocheleweshwa ni haki iliyopotea na kwa kuwa yapo madai yaliyokaa Mahakamani zaidi ya miaka 10 mpaka 20, mpaka wadai wake wanakufa hawajapata haki zao. Je, Serikali ina mpango gani mahususi na wa uhakika kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata haki zao kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama alisikiliza vizuri majibu yangu ya msingi, hata siku moja hakuna Taasisi ambayo imetumika kuzima hoja za msingi na kama ana ushahidi, alete ili uweze kushughulikiwa, lakini kitu kama hicho hakipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusiana na mashauri ambayo yamekaa Mahakamani kwa muda murefu. Kupitia Mahakama, tayari tumeshafanya tathimini ya mashauri yote nchi nzima na yako mengine hivi sasa yataanzaa kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachukua Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya, yale ambayo ushahidi wake umekuwa ukisua sua, ikiwezekana kwa upande wa upelelezi kama umekuwa ukichelewesha, yote yatafutwa. Kwa hiyo, ni imani yangu, baada ya bajeti hii ikishapita, basi mtaweza kuona mashauri yakisukumwa haraka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muwe mkiangalia muda wetu...

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, amesimama.

**NAIBU SPIKA:** Aaa! Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tafadhali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na tuhuma kwamba, Serikali inakimbilia Mahakamani, Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mbunge, tunajua kwamba mambo haya ni mambo ya kisheria, Sheria ya Ajira, ambayo ina utatu, siyo utatu mtakatifu, lakini utatu kwa maana kwamba; kuna Mwajiri, Mwajiriwa na Serikali, sasa Serikali ni mwajiri mnapogombana, hampelekani Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali na yenyewe ina wajibu na kwa Serikali inayofuata Sheria na Katiba, inafuata utaratibu ule, inakwenda Mahakamani kama mwajiri, ikasikilizwa na msimamo wake ukikubalika na Mahakama tusilalamike. Kwa hiyo, si kwamba Mahakama ni Serikali. Mheshimiwa Mbunge atakuwa anafahamu, Serikali nayo imeshawahi kubwagwa Mahakamani, mara nyingi tu. Kwa hiyo, si kweli kwamba, Serikali inatumia Mahakama na Mahakama ya Tanzania kama unafuata historia, ni Mahakama ambayo imesaidia sana kuwa na utaratibu hata wa Vyama vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, si kweli kabisa kwamba, Serikali inakimbilia Mahakamani, Serikali inafuata Sheria, inafuata Katiba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa maswali yenu na majibu ya upande

wa Serikali, najaribu kuchunga muda kama mnavyojua. Sasa tuendelee na matangazo yafuatayo, mafupi sana ili tuingie katika uchangiaji.

Tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimimwa Jenista Mhagama, kwenda kwa Wajumbe wa Kamati hiyo, kwamba, leo tarehe 15 Aprili, 2013 saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, Ukumbi namba 217 jengo la Utawala, saa 7.00 mchana.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mwenyekiti Kamati ya Bunge Nishati na Madini, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini saa 7.15 mchana, Kikao cha Kamati hiyo Ukumbi na. 231 jengo la Utawala.

Mheshimiwa Michael L. Laizer, saa 7.15 mchana, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anawaomba Wajumbe kwamba, wahudhurie kikao Ukumbi namba 227.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kuhusu swali na. 41 ambapo kwa maelezo yako umeliambia Bunge kwamba, Mheshimiwa Ismail A. Rage ameuliza swali zuri sana na Wabunge waige mfano huo, jambo ambalo sina tatizo nalo, pamoja na kwamba majibu ya Serikali yamekuwa ni mabovu kwa sababu suala la Mheshimiwa Rage lilikuwa la ujenzi wa reli katika nchi nzima, lakini majibu yamekuwa ya sehemu moja tu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wabunge wengi wamekuwa wakiuliza maswali kama hayo na huwapi

pongezi, mfano leo hii, swali namba 36, limekuwa ni swali fupi, lenye mistari mitatu kama lile swali la Mheshimiwa Rage, lakini Mheshimiwa Kangi Lugola hujampatia pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huoni kufanya hivyo unaligawa Bunge? (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Filikunjombe nianze kwanza kwa kukupongeza na wewe pia, kwa kuwa sasa umeanza kuyaona yale maswali ambayo kwa kweli, ndiyo ambayo tunasisitiza kila wakati, Waheshimiwa Wabunge tuwe na maswali mafupi, yanayoeleweka na ya moja kwa moja, kwani yanasaidia hata kuokoa fedha za Serikali za wananchi kwa kupunguza *paper work* kubwa sana na *printing* kubwa tunayofanya na inasaidia katika masuala ya muda wetu, lakini Mheshimiwa Rage ana sifa ya ziada, ni Rais wa Simba, jamani! (*Kicheko/Makofi*)

Tunaendelea, wachangiaji wa asubuhi hii watakuwa 18. Kwa hiyo, naomba moja kwa moja tujielekeze kwenye uchangiaji na tuzingatie muda. Niwaambie wananchi ambao wanatusikiliza Bungeni, muda wa kuchangia ni dakika 10 kwa kila Mbunge, lakini kuna Wabunge ambao wamekubaliana wao wenyewe kuchangia nusu ya muda huo, kwa maana ya dakika tano, kwa utaratibu ambao kikanuni tumekubaliana nao. Kwa hiyo, unapoona Mbunge fulani amechangia dakika tano, usichukulie kama Mbunge yule ameonewa, hapana, ni utaratibu wetu wa ndani ambao tumekubaliana.

Tunaanza na Mheshimiwa Vick Kamata atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

Mheshimiwa Vick Kamata!

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa naanza kuunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja, lakini ninapenda kusema kutoka moyoni kabisa kwamba, Serikali hii sasa inatukwaza. Nasema inatukwaza kwa sababu gani? Leo hii ni Bunge la bajeti la tatu mimi Vick ninachangia, nikileta kilio cha wananchi wa Geita kuhusu tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikituahidi ikitupa maneno mazuri, nimeuliza maswali kwenye kipindi cha maswali na majibu kuhusu tatizo la maji na nikajibiwa vizuri sana. Nilishawahi kushika hata vifungu kuhusu tatizo la maji kwenye Wizara husika ya Maji nikajibiwa vizuri sana, lakini hakuna kilichofanyika mpaka leo hii ninavyozungumza. Kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana cha watu wa Geita kuhusu tatizo la maji. Sasa nashindwa kuelewa, hii Serikali kwa nini inatufanyia hivi watu wa Geita! Tuna matatizo gani! Kwa nini inapuuza?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii naomba Waziri Mkuu atakapokuwa anafanya majumuisho, azungumze tatizo ni nini na kwa nini Geita maji hayaji wakati walishatuahidi na ni ahadi ya Rais, ya tangu mwaka 2010, kwa nini mpaka leo maji hakuna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *GGM* tayari wameshasambaza mabomba kutoka kwenye lile *Tank* ambalo waliahidi na wanaelekeza kule Ziwa Victoria tayari kupata maji, lakini Serikali haijaanza chochoche mpaka sasa hivi ninavyoongea, sasa tunashindwa kuelewa tatizo ni nini! Kwa kweli tunaona kama sisi watu wa Geita sasa tunapuuzwa, labda watu wa Geita hatuna maana, sitaki kuamini hivyo lakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie tatizo la wakulima kule Katoma na Nyamalembo, Wilayani Geita. Kuna wakulima ambao wana maeneo yao yamechukuliwa na *GGM* kwa uchimbaji, maeneo haya yameshafanyiwa *evaluation*. *Evaluation* imefanyika kwa kufuata taratibu zote, kwa maana ya kwamba, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Katoma ameshiriki, Mwenyekiti wa

Serikali ya Mtaa wa Nyamalembo ameshiriki, Maafisa Ardhi wa Wilaya wameshiriki, mwakilishi kutoka *GGM* ameshiriki, Wathamini kutoka Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali wameshiriki na Wakulima wenyewe wanaomiliki hayo mashamba wameshiriki na walikuwa wakitoka asubuhi wanakwenda kwenye yale mashamba, wanafanya *evaluation,* wakirudi jioni wanasaini zile *field forms*, siku ya kwanza wamefanya hivyo kwenye shamba la mtu mmoja, siku ya pili, mpaka wakamaliza mashamba yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamemaliza mashamba yote, Mthamini Mkuu wa Serikali amesaini, kwamba sasa hawa wakulima wanatakiwa walipwe kiwango hiki cha fedha. Wamepelekewa *GGM* wamekataa, wanasema kiwango hiki ni kukubwa sana, hakiendani na uhalisia, wanasema *over cropping, over cropping!* Wakati nalima mazao yangu kienyeji hamjaja kunipa elimu ya kilimo cha kisasa, leo hii ninapotaka haki yangu mnaniambia habari ya *over cropping*! Inatoka wapi hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe sasa huyu mwakilishi wenu wa *GGM* tumekuwa naye tangu *day one*, tunakwemda kwenye mashamba haya tunahakiki, kama shamba la mkulima fulani lina miembe 100, imeandikwa kabisa hapa tumekuta miembe 100. Leo hii mnakuja kusema kwamba kuna *over cropping*, kwa nini hukunifundisha kilimo cha kisasa kabla, leo hii nataka haki yangu ndiyo uniambie kwamba hapa mmelima kiholela, kwa hiyo, hamstahili kulipwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya hitimisho, azungumzie tatizo hili la wakulima wa Nyamalembo na Katoma, kwani wanahitaji haki yao. Tangu mwaka 2010 haya mashamba hawajalima, hivi Serikali imeshajiuliza hawa wakulima wanaishije au wanakula nini, imeshafikiria jambo hilo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba sana Serikali iingilie kati, hawa *GGM* wamezoea. Miaka saba

walikuwa hawalipi hata ile dola 200,000/= ya kila mwaka ambayo walikuwa wanatakiwa wailipe Halmashauri yetu, mpaka Kamati yetu ya Nishati na Madini iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Januari Makamba, *by then*, tulivyokwenda pale ndiyo tukayavumbua hayo kwamba, kuna dola 200,000/= ambayo ilikuwa haijalipwa kwa muda wa miaka saba. Hivyo sasa wanadaiwa dola milioni 1.4, wanatakiwa wailipe Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wameshatuona sisi hatuongei, tunakaakaa kimya tu, tumezubaa zubaa tu, ndiyo maana wanatuchezea namna hii. Naomba hawa wakulima wapewe haki zao, haraka iwezekanavyo, toka 2010 hawajalima, wanaishi kwa tabu sana. Naomba sana kwa niaba ya wananchi wa Geita, tatizo hili litatuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa nizungumie tatizo la wafugaji kule Bukombe. Yaani sasa ufugaji umekuwa kama ni msalaba, ni mateso wala siyo tena ni utajiri kama ambavyo mfugaji anatakiwa aishi. Hawa wafugaji wananyanyaswa sana kule Bukombe. Jana usiku saa mbili nimepigiwa simu na mfugaji mmoja analia kwamba, Maaskari kutoka kwenye Hifadhi ya Kigosi, wamekwenda saa mbili kasorobo usiku wakachukua ng'ombe wake wakawapeleka kwenye Hifadhi, wanataka huyu mtu awalipe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kulipa fedha, bado wananyanyaswa, ng'ombe wanapigwa risasi, wanakufa. Wale wafugaji wakionekana wanapita tu katika maeneo yale, wanafungwa kwenye miti wanachapwa. Hiki kitu naongea nina uhakika kabisa, naongea kitu ambacho nakifahamu ni cha ukweli.

Mheshimiwa Naibu Sipka, nataka niulize swali moja, hivi hawa wafugaji wana dhambi gani? Kwa nini Serikali isiwatengee maeneo yanayostahili wao kwenda kufanya kazi zao za ufugaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo hifadhi ya Serikali tunaiheshimu, ni sawa na hao Maaskari pengine wanafanya kazi yao, lakini najiuliza sana, hivi hawa Maaskari kuwanyanyasa hawa wafugaji wanaona ni sawa? Kwa sababu ukiangalia, mle ndani ya Hifadhi, kuna watu wanaingia wanakata miti, wanachoma mkaa, hawafanywi chochote, hatujasikia wamefanywa chochote. Kwenye hiyo hiyo Hifadhi, kuna watu wanaingia, wanakata miti, wanakata mbao, wanafanya vitu vya uhalifu, hatujawasikia hawa Maaskari wamewafanya kitu chochote.

Kuna watu wanachimba mpaka dhahabu kwenye Hifadhi, tunajua, lakini hatujasikia hawa Maaskari wamewafanya chochote, huyu mfugaji ana dhambi gani akipita na ng'ombe wake pale ananyanyaswa kiasi hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiulize Serikali, kwa nini inataka kuwafanya wafugaji waone kwamba ukiwa mfugaji wewe sasa umejiweka kwenye Jahanamu hapa duniani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mtanzania ana haki ya kuishi na kufanya shughuli ambayo Mungu amemjalia kwa furaha na amani. Naomba sana Serikali iwaangalie wafugaji wa Mkoa wa Geita, hususan hawa ambao wananyanyaswa sana kule Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijagongewa kengele, ningependa nizungumze tena suala la mwisho hapa haraka haraka, linalohusu ahadi ya Serikali. Serikali ilikuwa imeahidi kwamba, itafanya uhakiki wa Leseni za wachimbaji wakubwa, ili wale wakubwa wanaohodhi maeneo bila kuyafanyia kazi wanyang'anywe, wapewe wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri Mkuu alivyoongea kwenye hotuba yake, yeye amesema kwamba, wana mipango mizuri na nimeisoma, mipango mizuri sana ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, lakini ikumbukwe

kwamba, uchimbaji mdogo unachangia sana pato la mtu mmoja mmoja, pato la Taifa na unachangia sana kuongeza ajira kwa Watanzania wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa wachimbaji wadogo wasipopewa maeneo, wasipopewa nyenzo za kufanyia kazi watawezaje kujipatia pato lao na wataishije?

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijagongewa kengele, naomba kuunga hoja hii mkono, lakini naomba Waziri Mkuu, atakaposimama leo atueleze tatizo la maji Geita linakwisha lini, aeleze hawa wakulima wa Katoma na Nyamalembo lini tatizo lao na *GGM* linakwisha. Naomba pia azungumze kuhusu hawa wanaonyanyaswa kule Bukobe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi siku ya leo ili niweze kuchangia. Kabla sijasahau naomba niseme tu kwamba, naunga mkono hoja hii ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja, lakini *with my observations. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia masuala machache sana kwa ufupi, lakini ningeomba sana, niseme kwamba, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukweli, iko *very brief*, haiko *detailed* tofauti na mwaka jana, kwa hiyo, hiyo inatupa shida sana kuchangia. Vile vile haijaelezea vipaumbele vya Taifa kwa mwaka 2013/2014. Hiyo ingeweza kutupa picha, tumetoka wapi na tunaelekea wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie suala la uchumi. Uchumi wetu tunaambiwa unakua kila mwaka kwa asilimia saba. Sasa nashangaa, ndugu zangu wa kule Mbeya wanaokula *nguniani* kila siku, pato la dola moja kila siku. Uchumi huu ambao unakuwa kila mwaka kwa asilimia saba, na Watanzania wenzangu wananchi wa kawaida, pato lao ni dogo sana. Mtanzania najiuliza hata

sukari ndani ya nyumba haipo, sasa uchumi huu ni uchumi wa aina gani ambao kila mwaka tunaambiwa unakua, lakini Mtanzania wa kawaida hana pesa!

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni uchumi unaokua ambao unamrudisha nyuma Mtanzania maskini? Ningeomba wataalam wetu, Wachumi, wajaribu kufanyia utafiti suala hili ili hakika uchumi unapoongezeka, unapokua basi na maisha ya Mtazania yaweze kuboreka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye TAMISEMI. Katika ukurasa wa tano na wa sita, imeelezea mapato yake ni kidogo sana, asilimia 38.4 sasa sielewi ni kwa nini! Vile vile kwenye ukurasa wa 31 tumeambiwa kwamba *TAB* mikopo itatoka, nawapongeza katika hilo na vile vile nawapongeza kwa ku-*introduce JS,* lakini katika bajeti ya mwaka jana, nilielezea kwa uchungu sana, kule Mkoani Mbeya kuhusu Makatibu Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani kwangu Mbeya nina Makatibu Tarafa 27. Nilimhoji Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, kwenye hotuba yake alizungumzia vitendea kazi na nikasema Makatibu Tarafa wangu wa Mkoa wa Mbeya hawana vitendea kazi, wana pikipiki 18 tu ambazo zilitolewa tangu mwaka 2002 na zote hizi hazifanyi kazi. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na ukiangalia wao ndiyo wanaofanya kazi za Halmashauri kwa muda mrefu lakini maisha yao ni magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri anayehusika atakapokuwa ana-*wind up* anipe majibu ya kina na ya usahihi kuhusu Makatibu Tarafa wangu 27wa Mkoa wa Mbeya, suala la vitendeakazi limefikia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia nikiwa hapo hapo TAMISEMI ni kwamba, katika Halmashauri zetu sijaona mahali

panapoelezea fungu la vijana na wanawake, angalau kwa uchache tu, kwa sababu najua kuna mafungu yanatolewa *unless* tuambiwe kwamba, katika Wizara husika tutaelezwa hilo. Hilo ningependa pia nijue kwa sababu wanawake na vijana ndiyo Taifa la leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kama unavyoelewa kuna bomu la ajira. Kwa hiyo, hili jambo lisipoelezwa kwa kina, upana na marefu tutashindwa kujua. Nilipokuwa nachangia hotuba ya bajeti mwaka jana niliulizia sana suala la nishati *Kiwira Coal Mine* hususani ule Mlima wa Kaburu. Ningeomba tuelezwe mpaka sasa hivi *situation* ama *status* ikoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sina fadhila nisipozungumzia suala la kwangu Mbeya, ingawa hili jambo naelewa lipo kwenye *RCC,* lakini naomba Serikali Kuu na nimekuwa nikichangia mara nyingi hapa Bungeni, suala la *diversion* ya barabara kutoka Uyole iende mpaka Songwe ipite uwanja wa ndege. Hii itasaidia sana kupunguza msongamano wa magari na ajali zisizo za lazima na mimi mwenyewe nikiwa mhanga mmojawapo kwa sababu nilipata ajali mbaya sana ya kifo kwenye mlima Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii yote ni kutokana na haya magari makubwa ambayo yanakwenda mipakani Tunduma. Kwa hiyo, naomba Serikali Kuu itusaidie kwa ajili ya kuweka *diversion* kutoka Uyole hadi Songwe kwa sababu pia kuna Uwanja wa Kimataifa na itapunguza sana misongamano na ajali zisizokuwa za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nikiwa hapo hapo, naomba Mwanjelwa kwangu kuwepo na *round about* ambayo itakuwa inaelekea Mjini, kwa sababu vile vile *traffic jam* ni kubwa sana na ajali ni nyingi sana ambazo hazina ulazima. Kwa hiyo, naomba sana kama sio hapa kwangu Mwanjelwa basi lile eneo la ma-*fiat* liwekwe kama siyo *traffic light* basi kuwekwe *round about* ambayo pia itapendezesha Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuongea mengi sana, lakini kwa leo, yangu ya uchache ni hayo tu na nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Henry Shekifu atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mungu na kukushukuru wewe, nilipangwa juzi Ijumaa lakini sikuweza kuzungumza kwa sababu nilikuwa Mkoani Tanga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi inayotekelezwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa kule kwa ajili ya kuzindua barabara kutoka Tanga kwenda Horohoro. Napenda sana kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri; "aliye na macho haambiwi tazama." Mara nyingi inatisha sana zinapotoka kauli ambazo hazioneshi shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini mtu unaposema Katiba inaandaliwa ya ki-CCMCCM, sielewi kwa kiongozi kulitamka hilo. Maana humu ndani hata kama ungesema tusimame mstari Chama cha Mapinduzi kina 78% ya Wabunge na Vyama vingine vina 22%. Hata ungesema tusimame kwenye mstari mlengo utakwenda kwenye Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kwenye Mabaraza wameonekana wengi ni wa Chama cha Mapinduzi, sasa unahitaji kwenda shule kuelewa uwakilishi maana yake ni nini? Kwa hiyo, sihitaji kujielekeza huko, lakini nataka kuwaonya tu na kuonyana sisi wenyewe kama Wabunge, haipendezi kuwapotosha wananchi kuwaambia mambo ambayo si ya kweli na mambo ya kuvuruga amani. Watanzania wako macho sana kuangalia watu wabaya wenye nia ya kutaka kuleta mapambano ili nchi hii iingie kwenye janga, wamejifunza, si watu ambao hawaelewi, bali wanaelewa sana. Nawaomba wale wote wenye malengo ya kuleta mvurugano katika nchi yetu, waache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ya utangulizi, naomba nijirudishe katika kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwenye mambo madogo matatu. La kwanza, ni migogoro inayotokana na ardhi. Naiomba sana Serikali, kuna migogoro mingi sana kwa sasa ambayo inazuka kati ya wakulima na wafugaji. Hii migogoro isipoangaliwa na kutafutiwa ufumbuzi, tunatafuta tatizo kubwa ambalo kwa kweli hili nasema linaweza kutuvunjia amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali na hasa ofisi ya Waziri Mkuu kwamba, ni muhimu kuchukua hatua za kupanga matumizi bora ya ardhi. Maeneo ya malisho yajulikane na maeneo ya kilimo yajulikane. Tusiogope kutenga fedha nyingi tukafanya kama *operation* ili wananchi wetu katika vijiji vyetu waelewe, maeneo ya akiba ni yapi kwa ajili ya uwekezaji, maeneo ya kuwekeza katika ufugaji ni yapi na maeneo ya kilimo ni yapi, hili naliunganisha na hati miliki za kimila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wadogo wadogo kama wa Lushoto ambao tumewatamka katika ukurasa wa 30, kuhusu kilimo cha matunda na mboga, sisi kule tunaishi kwa ajili ya kilimo cha matunda na mboga. Hatuna maeneo makubwa, raslimali yetu ya ardhi ni ndogo, ila ikipimwa itaweza kutupa sisi uwezo wa kukopa. Sasa naomba bas,i tupewe upendeleo maalum, wananchi wa maeneo madogo madogo ya kilimo cha matunda na mboga hawapati pembejeo za ruzuku na hao wanaishi huko juu milimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwaangalie. Huwezi kuuza matunda yenye ubora katika soko la Kimataifa bila kuyakuza kwa utaratibu unaoeleweka; unahitaji dawa, mbolea na vifaa vingine ambavyo kwa kuvitumia hivyo zao lako litakuwa na soko katika Soko la Dunia. Sasa wakulima wadogo wadogo bila kupewa msaada hawataweza

kumudu au kushindana katika soko la mbogamboga na matunda ambapo kwa wananchi wa Lushoto kwa kweli ndiyo tegemeo letu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika suala lingine ambalo linaleta matatizo na tusipoliangalia litatuletea migogoro, nalo ni maji na mazingira ambavyo ni vitu vinavyokwenda kwa pamoja. Tumeanza kupata matatizo ya uhaba mkubwa wa maji na usimamizi wa vyanzo vya maji. Naomba Serikali ichukue jukumu, kuna maeneo rasmi ambayo Serikali inapaswa kutenga fedha za kuboresha mazingira, kwa mfano, Wilayani Lushoto, ni eneo ambalo kulikuwa na misitu mingi sana, misitu ile sasa haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo kweli ya ukataji miti hovyo, lakini pamoja na kudhibiti kurudishia uoto wa asili, ni lazima Serikali iwekeze na iwekeze katika miti na katika kulinda vyanzo vya maji. Sasa hatuoni juhudi za moja kwa moja katika hili japo lazima niseme ni kweli maeneo ya Shume, Magamba miti inapandwa, lakini kuna maeneo ambayo miti ilipandwa mwaka 1978, uoto wa asili umetoweka. Tunaomba Serikali iyachukue maeneo haya ili yapandwe miti na bahati nzuri ni maeneo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni kuhusu uchumi wa wananchi wa kawaida. Ni kweli uchumi wetu unakua, uchumi mkubwa unakua na mtu yeyote asiyeelewa ambaye kwa kweli hatutakii nia nzuri katika nchi hii, atalaumu. Nani asiyekubali kwamba barabara zimejengwa? Nani asiyekubali kuhusu upatikanaji wa maji juhudi zinachukuliwa? Lakini tatizo letu kubwa vitu hivi vinaonekana kwa wakubwa wenye magari, kwa wakubwa wenye uwezo, lakini kwa wananchi wa kawaida maisha yake ya kawaida ni duni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama alivyotamka kwamba, sasa tunaanza kuangalia maisha ya mwananchi wa kawaida, apate mahitaji yake kwa bei nafuu, mahindi yapatikane bila kumnyima mwananchi haki ya kupata chakula. Bei zidhibitiwe

kama mlivyofanya mwaka huu, mmefanya vizuri sana, kwani mlipoona bei imepanda, haraka mmetafuta mahindi katika maeneo yenye mahindi mengi yakapelekwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mfumuko wa bei umeshashuka kwa kasi sana, ni ule utundu wa kupeleka mapema, hatutaki muwazuie wananchi wasiuze mazao yao yaani wakulima. Hilo ni jambo baya katika uchumi kwani ukimzuia ataacha kulima, lakini ukimwekea zile *physical policies* na zikiwekwa vizuri utaona maendeleo yatakuja. Kwa hiyo, nashauri na leo nimeambiwa Rukwa gunia la mahindi limefika shilingi 90,000/=, ni ukweli mkulima amenufaika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini basi mazao haya yanunuliwe mapema ili yasambazwe katika maeneo ambayo bei zimepanda sana, pia mwananchi apewe uhuru katika kilimo chake, tusiwabane wakimaliza kulima. Naamini Waziri wa Kilimo ananisikia, suala la kuwabanabana wakulima tuliache! Wapeni motisha, walime, kisha nunueni mazao yao, yawekeni akiba, yagawanywe wakati ambapo tunaona kuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nisigongewe kengele, naomba nizungumzie kwa mara ya mwisho, najua elimu imezungumziwa sana. Juzi katika kuchangia kwangu nilisema kwamba suala la elimu kwa leo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shekifu!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono mara mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niweke sawa pale ambapo Mheshimiwa Mnyaa juzi alizungumzia suala zima la usafirishaji wa gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam. Nataka niiambie Serikali kwamba imetaka kujenga bomba la gesi la kilomita 290 kutoka Somanga Fungu kwenda Mnazi Bay ambayo gharama yake ni dola *379 millions.* Lakini waangalie kwamba ujenzi wa *power line double socket* kutoka Kinyerezi mpaka Mnazi Bay ambao una 487 *kilometers* gharama yake *is only 282 millions.* Sasa hebu angalie *difference* hapo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunataka Serikali ikae iliangalie na ilifikirie hili ambalo nataka kuwapa wazo. Ujenzi wa *power line per kilometer is only 600 thousands,* popote utakapokwenda, lakini ujenzi wa bomba la gesi, unagharimu *almost 1.309 million dollars per kilometer*. Sasa tuangalie hii *difference,* halafu tuone namna gani tunafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze sasa moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 14, anaanzia na suala la Muungano, kuhusu Kamati ya pamoja ya SMT na SMZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna moja ya kero ambazo zimeongezeka katika Muungano, basi ni Kamati hii na Kamati hii imekuwa ni kero kwa sababu ya utashi wao wa kuziba au kutokutoa taarifa kwa wananchi kwa yale ambayo wanayazungumza. Wanakuwa wanayazungumza tu kijuujuu, kama hapa Mheshimiwa Waziri kasema kwamba, wamezungumzia suala la gesi asilia, ushirika wa Zanzibar katika Taasisi za nje, lakini je mmefikiaje na mnawaambiaje wananchi? Tamko gani mmeondoka nalo hapa ili wananchi waelewe kwamba sasa suala la gesi na mafuta, ni suala la wenyewe Wazanzibar halitahusiana tena na masuala ya Muungano. Tunaomba muwe wazi katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba hii Kamati

ambayo mnaitumia haiko kihalali, wala haiko katika masuala ya Muungano, bali imeundwaundwa tu kimagumashi, basi inaendelea kufanya kazi zake. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu muwe wazi na muwaambie wananchi yale ambayo mmeyafikia ili wananchi waelewe, msiongeze kero zaidi za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili, katika ukurasa wa 20, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia *presidential of delivery bureau* na hii alisema kwamba hawa Mawaziri ambao wamepewa hili jukumu walitoa kauli. Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano, ndiyo wawakilishi wa wananchi na kauli za Mawaziri tumezizoea, zinakwenda mbele na kurudi nyuma, *time* nyingine hazieleweki, hebu hawa Mawaziri waje ndani ya Bunge na wale kiapo katika hili, hapo tutawaelewa kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo tu wao wenyewe wamekaa huko waseme wamemwahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapana! Hii ahadi haitoshi, bali waje hapa mbele ya Bunge letu, wale kiapo, ndiyo tutajua kwamba kweli wamekusudia kufanya kazi. Lakini vilevile mfumo mzima wa bajeti unahitaji nao kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 40 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu suala la sekta ya utalii. Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema kwamba, wameandaa mpango mkakati wa kufanya Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Tanga kuwa vivutio vya utalii wa ufukwe. Hawa washauri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanamdanganya, hivi Dar es Salaam kuna fukwe gani ambayo imebaki? Fukwe zote zimeshachukuliwa na wawekezaji, ipi iliyobaki? Hakuna fukwe iliyobaki Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu wamwambie ni Mheshimiwa Waziri Mkuu ni namna gani ya kuendeleza utalii Dar es Salaam, hususani utalii wa ndani, lakini siyo

wamwambie katika fukwe kwani 99% ya fukwe za Dar es Salaam zimejaa. Tunaomba wanapompa hizi taarifa wampe taarifa za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kama tunataka masuala haya ya kuendeleza Miji hii ya Lindi na maeneo mengine, tusiende moja kwa moja tu katika fukwe. Fukwe zinakuwa na watu maalum ambao wanakwenda kule, lakini huku juu kuna Halmashauri zetu ambazo nazo zinahitaji mapato kutokana na huu utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Nachingwea katika Kata ya Ruponga..

**MJUMBE FULANI:** Ruponda!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Ruponda! Kuna mapango ya Kilimarondo, ni mapango mazuri tu yapo pale, ambapo kuna popo ambao zaidi ya kule Jimboni kwangu Ole, basi sehemu nyingine ambapo utawakuta ni katika mapango hayo, dunia nzima hakuna sehemu nyingine. Sasa hayo ndiyo maeneo ya kuwekeza zaidi katika utalii. Tukisema kwamba, twende tu katika fukwe, fukwe watakwenda watalii wawekezaji wa kubwa lakini hawa watu wa kawaida hawatakwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, naomba nizungumzie katika hotuba ya Waziri, Mheshimiwa Ghasia. Waziri Mheshimiwa Ghasia katika ukurasa wa nne anazungumzia suala la nidhamu katika matumizi ya fedha. Nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, haya ambayo ameyaeleza hapa, si kwamba tu yanatia kichefuchefu, lakini hebu atueleze hali halisi ilivyo katika Halmashauri zetu. Katika Halmashauri zetu kumeoza, wizi umekuwa wa hali ya juu. Kipindi kifupi nilichokaa kama Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* nimeyagundua haya. Leo watu wawili ndiyo wamepelekwa Mahakamani. *What is that?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zimeoza, nidhamu imeondoka katika matumizi ya fedha. Hii nataka nimwambie Mheshimiwa Ghasia kwamba, hili linatokana na Wizara yenyewe ya TAMISEMI kuwa iko mbali na Halmashauri zetu, kuna *vacuum* katikati. Kilichopo hapa baina ya Halmashauri na TAMISEMI ni mtandao wa wizi. Huu mtandao ndiyo unaziadhibu Halmashauri zetu, leo Wakurugenzi wanakuwa na *power* wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Wizara ipo! Hili halikubaliki kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mifano hai ya kutokuwa na nidhamu katika matumizi na haya Waziri lazima atupe majibu. Kuna suala la ukopaji uliokithiri wa wafanyakazi. Wafanyakazi wanakopa mishahara yao *almost* yote na sheria zipo kwamba, mfanyakazi asikope zaidi ya *two third* (2/3) ya mshahara wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafikira huyu mfanyakazi anapozikopa fedha zake zote atapata wapi kujikimu katika mahitaji yake mengine, litakalobaki ni kuiba tu. Hii sheria ipo, lakini Wizara mnashindwa kuzisimamia Halmashauri wakati ninyi ndiyo walezi wa, mnawaachia Wakuu wa Mikoa na Wilaya peke yao, hawawezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna hulka na tabia moja mbaya kabisa ambayo imejengeka katika Halmashauri zetu, ya kutokutekeleza mapendekezo ya *CAG*. Hii ndiyo inasababisha utovu wa nidhamu katika matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rajab naambiwa ni kengele ya pili.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Anne Malecela ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Kapteni John Komba!

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi ya kuzungumza, lakini kabla sijachangia naomba niongee na Watanzania kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais au Urais ni taasisi ambayo ina majukumu makubwa sana. Jukumu la kwanza la Rais au taasisi hii ni kwamba, ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais hawezi kuwa mahali pote kwa wakati mmoja. Hawezi kuwa kwenye Mikoa yote kwa wakati mmoja. Hawezi kuwa kwenye Wilaya zote kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, Rais anamweka Mkuu wa Mkoa ili aende kuwa Mwenyekiti ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ule ili wananchi wa Mkoa ule waishi kwa usalama. Lakini Rais pia hawezi kuwa kwenye Wilaya ya Same, akawa kwenye Wilaya sijui ya Igunga, akawa Wilaya ya Kisarawe, hapana! Rais anaweka Wakuu wa Wilaya ili waweze kuwa Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama kwenye Wilaya zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi wanasiasa tunazungumza ooh, Wakuu wa Wilaya sio muhimu, Wakuu wa Mikoa siyo muhimu, sasa wananchi wataishije? Usalama wao utakuwa mikononi mwa nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge, nimechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Same Mashariki, kazi yangu, naunganisha wananchi wa Same Mashariki na Serikali Kuu. Mimi nawasemea wananchi wa Same Mashariki masuala yao humu ndani, siwezi kufanya kazi ya *DC*. Kwa hiyo, wananchi msidanganywe na wanasiasa, *DC* ni muhimu, Mkuu wa Mkoa ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuchangia.

Naomba nianze kuchangia, hapo nilikuwa naongea na Watanzania wajue wajumbe wao.

Mheshiwa Naibu Spika, nitaanza kuchangia kuhusu umeme vijijini. Tanzania asilimia 80 ni vijiji, asilimia 80 ya Majimbo yako vijijini, lakini wananchi kwa Tanzania nzima ambao wameunganishiwa umeme, ni asilimia 21. Katika hiyo asilimia 21 wananchi wa vijijini ambao wameunganishiwa umeme ni asilimia saba, siyo haki. Wananchi ni asilimia 80, lakini wao wanapewa asilimia saba, hawa ambao wako chini ya asilimia 20 wanapewa asilimia 14, siyo haki. Ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuangalia umeme vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo limenisikitisha sana, bajeti ya 2012/2013. Bajeti ya umeme vijijini ambayo ilipangwa, iliyopelekwa ni asilimia 13 tu. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba anisikilize na Waziri aliyekaa pale aondoke. Naomba Waziri Mkuu anisikilize maana yake linamhusu na yeye pia ana Jimbo la Vijijini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 13 tu katika bajeti ya mwaka mzima ndiyo imepelekwa kwenye umeme wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisaidie kwa sababu mimi naongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa endelea unaongea na mimi, endelea moja kwa moja.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Hapana, nataka Waziri Mkuu anisikilize, siyo haki. Siyo haki anavyofanya Mheshimiwa Lukuvi. Hapana, siyo haki. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ameacha kuongea.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Umeme vijijini, asilimia 13 ya bajeti ya mwaka 2012/2013, basi niache kuzungumza! Asilimia 13 tu ndiyo iliyokwenda vijijini, siyo haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi utamwona Waziri wa Nishati na Madini anazunguka huko nchi za nje. Amekwenda Norway, Ubelgiji na Ujerumani, anatafuta fedha za umeme vijijini. Tunawashukuru Serikali ya Norway wametupa bilioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize vizuri, hizi bilioni 200 zote ziende kwenye umeme vijijini na bajeti iliyotengwa kipindi hiki yote iende kwenye umeme. Mkitaka tusielewane, fedha ya umeme vijijini ipelekwe mahali pengine, hapatatosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la ulinzi wa rasilimali za Taifa. Ulinzi wa raslimali za Taifa ni hafifu. Serikali hapo haijaweka mkazo kwa sababu madini yanapotea katika njia mbili; ya kwanza, ni mikataba mibovu na pili ni wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze mifano miwili tu, Wizara ya Nishati na Madini iliweka dawati kwenye viwanja vya ndege vitatu, Kilimanjaro, Mwanza na Dar es Salaam. Kati ya Oktoba, 2012 na Februari, 2013, miezi mitano tu, tuliweza kukamata madini yanayotoroshwa na wafanyabiashara wawekezaji wa ndani ya nchi na nje ya nchi, kumi na moja, lakini madini hayo yalikuwa na thamani ya bilioni 13, ndani ya miezi mitano tu. Sasa mwizi siku zote anakamatwa siku ya 40, wezi hawa walikuwa kumi na moja, siku 39 walikuwa wanaiba na hawa ni mfano mmoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi mmeona hapa, tani 200 za madini ya shaba, zilizochimbwa Wilaya ya Mwanga zikitoroshwa, Watanzania hatukupata hata kitu kimoja. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu atupe mkakati maalum ambao Serikali sasa imeamua jinsi watakavyofanya kulinda rasilimali za Watanzania ili Watanzania wawe na uhakika kwamba, rasilimali zao haziendi mikononi mwa watu wachache na haziendi kwa wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze

jambo la tatu, sijui kama muda utaniruhusu, kuhusu upatikanaji wa gesi nchini. Niliongea na waungwana wawili wakaniambia, *success is always an enemy*. Haya mafanikio ya kwamba Taifa hili sasa tumepata gesi ni *success*, lakini hapa hapa kwenye hii *success* ndipo uadui ulipo na ndipo adui alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuwe makini, Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na Serikali, hili suala la gesi ndiyo litakaloondoa Taifa letu kwenye hii hali na kutupeleka kuwa *at least* Taifa la katikati. Hapa tushirikiane na Serikali vizuri, tusije tukayumbishwa na Mataifa makubwa, tuwe makini Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali waelewa mikataba ya gesi itakayoingiwa, tutakuwa wakali sana kama haitawasaidia Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba nisikilizwe vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango. Mheshimiwa Kapteni John Komba atafuatiwa na Mheshimiwa Mustaafa Akunaay.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niunge mkono bajeti hii ya Waziri Mkuu. Lakini nianze na hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Nimeisoma yote, hotuba hii imejaa mapepo matupu, imejaa dharau kwa Serikali, imejaa dharau kwa Waziri Mkuu, imejaa dharau kwa Chama cha Mapinduzi, imejaa dharau kwa Tume ya Katiba na imejaa dharau kwa Jeshi la Polisi. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka ni- *quote* kauli ya Mao Tse- Tung, Kiongozi wa China na mwasisi wa Taifa lile.

**MBUNGE FULANI:** Zungumza kichina!

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Siongei kichina wewe. (*Kicheko*)

Alisema hivi, na- quote kizungu: *"If your enemy criticizes, attacks and hates you, be happy because you are doing the right thing. But if your enemy prays, it's time to be very much careful."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wapinzani hawa hasa CHADEMA wameshasema kwamba, wao kila kitu watapinga. Sasa kama kila kitu watapinga leo tutashangaa kama watatusifu, watatushukuru. Kwa hiyo, nawapa pole Jeshi la Polisi, Waziri Mkuu na wote ambao wametukanwa katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme katika nchi yetu hii, sisi siyo kisiwa, sisi ni miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki na wanatusikiliza na wanatuona na sisi ni mfano wa amani katika Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, CHADEMA walifikiri hawasikilizwi, wakaenda Kenya kufanya kampeni na fujo kule. Kule wameondoka usiku, wameshindwa vichwa chini, wamemtukana yule Uhuru Kenyatta..

**MBUNGE FULANI:** Una ushahidi?

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:**, Ninao sio kwamba sina ushahidi, lakini leo Kenyatta ndiye Rais pale na mtu wao hoi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Wakenya wanajua, unafikiri Watanzania hawajui? Mtaipata. Hawa wakitaka kujua wasubiri mwakani, siyo 2015, mwakani katika chaguzi za Serikali za Mitaa, mtaona jinsi mtakavyoondoka hapo mlipo na kushuka chini. Mtagaragazwa na nasema kwa sababu ya hii hotuba. Nazungumza kwa sababu najibu hoja iliyoko humu ya Wapinzani. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye suala la mipaka. Nimeangalia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu mipaka imetulia, lakini nasema mpaka wa Malawi na Tanzania ni hatari sana, ni bomu ambalo litalipuka. Ukiona upande wa Tanzania na upande wa Malawi yule Rais wa Malawi anahubiri kila wiki, anasema, ninyi Wamalawi mliopo kando kando ya huko upande wa Tanzania vumilieni baada ya muda mfupi tu tutawakomboa. Kwa hiyo, hii ina maana na Mbunge naye atakombolewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ni maneno ya uchochezi na ni hatari, lakini watu wanaona pale kwamba sehemu ile imetengwa sana. Sehemu ile kama ni mahitaji ya vyakula, inapata kutoka kule, kama ni chai inapata kutoka kule, kama ni sukari inapata kutoka kule, huku kwetu yako mazao ndiyo tunalima kahawa, tunavua samaki, lakini samaki wengi wanavuliwa kule kwa nini? Kwa sababu kule wenzetu wanasema nini, kulikiza samaki, kulisha, yaani, wanalisha wale samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu tunathamini tamko la Kimataifa kwamba huruhusiwi kulisha samaki katika Maziwa. Wenzetu wanavunja hiyo wanalisha samaki na samaki hawana mpaka wanakwenda kula kule, wanavuliwa kwa wingi sisi huku tunakosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nchi yetu iangalie jambo hilo. Yule jamaa ametutega kule na anatusema kila siku, kwa sababu wale wananchi wa kwetu kule hawana mawasiliano na Serikali yao. Hata *TBC* leo haiko kule, kwa hiyo yale anayotamka Rais wetu, Mawaziri wetu, anayetamka nani, kule wanamwona Mbunge tu na Mkuu wa Wilaya akipatikana, basi, labda na Mawaziri wanaokuja kutembelea, lakini kitu kitu tunasikia kutoka Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muimarishe mitandao hii hasa ya TEHAMA, hasa ya habari, habari ziende kwa wananchi kule mpakani, haziendi. Naomba muimarishe. Nimeangalia kwenye bajeti ya Wizara ya Habari, *TBC zero*, hakuna fedha na nyie mnasema kwamba kule Nyasa mpaka

uko katikati, wale habari ya kwamba mpaka wa Ziwa Nyasa uko kando kando wanaipata kutoka Malawi kila siku, kila wiki. Ninyi mnasema mkiwa Dodoma, Dar es Salaam, habari haiendi kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wale wanakuwa *induced* na maneno ya Malawi kwamba kweli sisi ni watu wa Malawi na wanatamani, unajua kwa nini? Huku kwetu sasa hakuna usafiri wa ziwa, zilikuwepo meli Tatu; *MV.* Mbeya, *MV.* Songea na *MV.* Iringa. *MV.* Mbeya ilizama, *MV.* Iringa ilikufa, *MV* Songea inazimika zimika ziwani na sasa haifanyi kazi kabisa. Sasa wanatamani meli zile zinazopita Malawi, zingepita huku, huku hakuna kitu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Nyasa kwa upande wetu sisi ni ziwa peke yake linalotumia mitumbwi, duniani ni wapi wanatumia mitumbwi? Lakini ukifika Mbamba Bay, Lituli, Liuli, Ngumbo, fika maeneo yote hayo, wanatumia mitumbwi ya kuchonga. Wenzetu Malawi wanatumia boti na Rais wao anahubiri tuna boti hapa, tunataka kuwasaidia wenzetu Watanzania, lakini tutaelewana tu, mvumilie kidogo. Anasema mwanamke yule, tuvumilie kidogo. Sasa nafikiria hivi akishinda na mimi niende Malawi jamani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika hotuba ya Waziri Mkuu Maziwa yametajwa, lakini Ziwa Nyasa halipo. Kwa hiyo, tunadhihirisha namna gani ambavyo Rais, yule mama anavyozungumza mambo ya ukweli na wananchi wanaona. Hawana barabara ya lami, hawana umeme, hawana tone, wanasikia tu kuna jambo la umeme duniani, lakini hakuna umeme, uwe ni wa vijijini, iwe ni wa gridi ya Taifa au mwingine na katika bajeti nzima hakuna hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi namuuliza Mkuu wa Kitengo cha *REA,* anasema tumefungua tenda lakini hatuna fedha ya kupeleka umeme kidogo tu Mbamba Bay, haizidi bilioni moja (1) lakini hawana fedha. Yule mama kule

ameweka umeme Ziwa zima kutoka Mangochi mpaka huko anakopakana na Waziri, Mheshimiwa Mwakyembe, umeme mtupu kama nasema uongo na yeye yuko hapa anasikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu giza totoro, halafu mnasema hiyo ndiyo nchi yetu, nchi yenu vipi? Kwa hiyo, watu wanasema acha mama huyo achukue nchi, tutapata umeme, boti na kadhalika kwa sababu hatuhangaiki na watu wale, anahangaika Mbunge tu. *(Makofi/Kicheko)*

Tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kutufikiria...

**NAIBU SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Kapteni Komba.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Eeh, alitupa Wilaya, ahsante sana. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wanaofuata ni Mheshimiwa Mustapha Akunaay na Mheshimiwa Joseph Selasini, wao watagawana dakika tano tano. Baada ya hapo, ajiandae Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Mheshimiwa Akunaay!

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ili niweze kusimama mbele ya Bunge hili kutoa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, napenda kumtaarifu mzungumzaji aliyepita kwamba CHADEMA ilialikwa kama chama katika uchaguzi wa Kenya, wala haijahutubia isipokuwa Waziri mmojawapo wa Chama cha Mapinduzi alihutubia kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea, chama cha CHADEMA hakipingi kila kitu, kwa mfano, saa hizi ni mchana, hakipingi kwamba saa hizi ni mchana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na Baraza la Katiba. Tunachozungumza ni kwamba, kuna matatizo yaliyotokana na kutokuwa na kifungu cha sheria katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kinachotoa mwongozo jinsi ya kufanya uchaguzi wa Wawakilishi katika Baraza la Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachosema, uchaguzi umefanywa vibaya, kwa sababu Wawakilishi wamechaguliwa na Wajumbe wa *Ward Council,* huo ni uchaguzi kwa *proxy* kwamba, imevunja haki ya mtu kuchagua Kikatiba Ibara 5 *Universal suffrage* imevunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachoshauri Serikali ni kwamba, uchaguzi huo ufutwe ili wananchi wafanye *direct election.* Kwa mfano, katika Wilaya ya Mbulu, Kata ya Dongobesh wamefanya uchaguzi mpaka Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo walichagua watu. Hicho ni kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda niende jambo la pili, nataka kuzungumzia kukosekana madawa katika hospitali kutokana na fedha kuchelewa kutoka Hazina. Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, fedha zilitoka Hazina mwezi wa Desemba, kwa hiyo, kukawa hakuna dawa na vifaa tiba hospitalini kwa miezi zaidi ya sita. Tunaishauri Serikali kwamba, fedha zitoke kama ilivyopangwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuzungumzia kuhusu Serikali Kuu kuingilia umiliki wa ardhi ya Halmashauri. Halmashauri katika Sheria ya *Local Government Act*, ndiyo mmiliki wa ardhi katika sehemu zake, lakini baada ya Serikali Kuu kuuza nyumba zake, inaonesha kwamba, ardhi za Halmashauri zinaingiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano, katika Wilaya ya Mbulu ziliuzwa nyumbani za Serikali Kuu mpaka ikafanya hospitali ya Wilaya ya Mbulu kushindwa kufanya *expansion* kwa sababu eneo la eka 42 linamilikiwa na watu wanne kandoni mwa hospitali. Kwa hiyo, imefanya hospitali

ishindwe kufanya *expansion* pamoja na Chuo cha hospitali kilichopo pale. Kwa hiyo, tunataka kujua je, Kati ya Serikali Kuu na Serikali ya Mitaa, nani mmiliki wa ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, katika Jimbo langu tunalima vitunguu swaumu, tuna tatizo la soko. Sasa tunayo Wizara ya Kilimo na Ushirika ambayo inahusika na masoko, tunaiomba Serikali ituletee soko katika eneo hilo, badala ya wananchi kulanguliwa ambao hawana soko na hawajui bei ya dunia kwa leo ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kutaka kujua kwamba kazi ya Mkuu wa Wilaya katika Halmashauri hasa kwenye Baraza la Madiwani, nafasi yake ni nini? Kwa sababu inaelekea kuna mwingiliano wa kazi baina ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri, Mkurugenzi anaingiliwa kwenye kazi zake na Mkuu wa Wilaya saa nyingine anachukua kazi ya Baraza la Ardhi ya kugawa mipaka ya vijiji. Kwa sababu sasa hivi tunakwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka kesho, tunaomba mipaka ya vijiji ijulikane kwa kutumia *GPS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kengele haijalia pia ningependa pia kuzungumzia juu ya kufeli kwa wanafunzi wa kidato cha nne mwaka jana. Nashangaa Tume inaundwa kuangalia kwa nini wamefeli, badala ya kuunda Tume kwa nini wamefaulu. Kwa sababu kutokana na misingi ya elimu yetu ilivyokaa mwanafunzi anaingia *form one* akiwa tayari amefeli maana ana alama ya 70, kwa hiyo, huyu lazima afeli. Kwa hiyo, Tume hiyo ingechunguza kwamba, elimu yetu *quality* yake ikoje? Tunafundisha nini, siyo kufaulu, kufaulu hakusaidii, mtihani unaweza ukatungwa rahisi, lakini wanafunzi bado watakuwa hawana *knowledge.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajasema ninachotaka kusema, nataka niwakumbushe Wabunge

wenzangu na wanasiasa wote wa nchi hii kwamba nchi hii ni yetu sote na kwa hivyo, tuache mbwembwe na maneno ambayo yanaamsha hisia za kuvuruga nchi yetu. Kwa sababu amani itakapotea wote tutaathiri na kutafuta pa kukimbilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema haya kwa sababu, nataka nizungumze kwa kina suala la udini ambalo limekuwa likizungumzwa. Katika kuzungumza hilo nimekuja hapa na kada na naitaka Serikali itoe majibu ya nitakayoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukizungumza suala la udini na nimesikia Serikali inataka kutengeneza kikao cha viongozi wa dini kuzungumza. Nataka niiambie Serikali hakuna haja ya kikao cha viongozi kwa sababu suala hili la udini, limepandikizwa na linasimamiwa na baadhi ya viongozi ndani ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu, mengi yanayofanyika katika nchi hii kuhusu udini ni uvunjifu wa sheria za nchi. Nashangaa kwa nini hatua hazichukuliwi kwa wanaovunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano michache; *UDOM* kama ninavyojua mimi ni Chuo cha Serikali, lakini *UDOM* chuo kinaendeshwa kana kwamba ni Chuo cha kidini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili nitaweka mezani hii kanda, ni kanda ambayo wanafunzi wa *UDOM* wa dini fulani pamoja na Wahadhiri wa dini fulani ndani ya *UDOM,* walikusanywa wakapewa siasa za chuki dhidi ya wenzao wa dini nyingine na ikafikia mahali mmoja kati ya waliopewa huo mhadhara wakauliza katika mhadhara, mtasikia katika hii kanda kwamba kule kwenye mabweni tunalala na wale wa dini nyingine, tuwafanyeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie hii kanda, itoe majibu yanayostahili kwa sababu kanda hii ikiangaliwa

na kusikilizwa na wengine, itakuwa ni hatari. Kwa hiyo, nasema Maaskofu na mashekhe wakakae kufanya nini? Serikali ichukue hatua dhidi ya wachochezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niiambie Serikali, tumefikia hatua mbaya, sasa hivi ukienda Dar es Salaam kuna Mashirika, kuna Makampuni ya watu binafsi yanaajiri kwa misingi ya kidini. Sasa hivi tukienda Dar es Salaam kuna baadhi ya Walimu ambao wanaita wanafunzi wa dini fulani wanawafundisha wenyewe tu, wakaguzi wa elimu wako wapi? Kwa hiyo, tusiwe wanafiki na tusiendelee kuhubiri amani katika mioyo yetu wakati ndani mwetu kabisa kuna chuki na kuna ubaguzi wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wahubiri wanasema waziwazi Askofu chinja, Mchungaji chinja, ukiona Mkristo chinja. Hivi Jeshi la Polisi tunalolisifia, kanda hawazioni mitaani, wanangojea kwenda kuvizia watu kwenye *you tube* na kuwakamata. Wakati kuna watu ambao kabisa wanaua misingi, wanaua amani ya nchi hii na wanaachwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mimi nasema Serikali katika suala la udini ijitathmini, wakati wa Mwalimu Nyerere tuliishi kama ndugu, tulipendana, tulisaidiana, tulioleana, vipi baada ya Mwalimu Nyerere suala hili liibuke. Halafu Serikali inasema inawaita viongozi wa dini. Tatizo halipo kwa viongozi wa dini, tatizo lipo Serikalini katika kusimamia sheria zilizopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka niwaase wanasiasa wenzangu. Mwaka 2005 tulisikia kuna majambia yaliletwa na *CUF container* nzima, *CUF* Chama cha Kigaidi, *CUF* chama cha Kidini, kesi hiyo iliyoishia wapi? Ni Mkuu wa Jeshi la Polisi wakati huo Omar Mahita alisema jambo hili. Kama ilikuwa ni uongo, huyu alikuwa kiongozi mzito katika nchi, alichukuliwa hatua wakati gani huo? *CUF* iliombwa radhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mwaka 2010 CHADEMA

tulisikia ni Chama cha Wachaga, CHADEMA ni chama cha wakristo, hivi hao waliosema wamechukuliwa hatua gani na nini kinafanyika? Haiwezekani viongozi badala ya kutafuta hoja za kisiasa tukazizungumza, tukaendelea kuzungumza hoja za kugawa Taifa letu. Hoja kwa msingi wa udini, ukabila na rangi, ni hoja ambazo sisi wanasiasa baada ya kukosa hoja tunazijenga ili tupate uungwaji mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke mezani kanda hii, iangaliwe na Serikali na Serikali ilete majibu yake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni. Makatibu chukueni kanda hizo. Kwenye orodha yangu Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu ili nami niseme ya kwangu machache niliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia fursa ya uhai ili tuweze kukutana katika Bunge hili kujadili masuala muhimu yanayohusu nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape pole wananchi wa Jimbo la Mtera, wakazi wa Kata ya Mloa barabarani kwa kupata maafa ya mafuriko. Mafuriko yaliyosababishwa na wajenzi wa barabara ya lami kutoka Dodoma kwenda Iringa, Wachina wale kuziba njia zinazopita maji siku zote, na hivyo mvua kubwa ilivyonyesha maji yakarudia wananchi na kubomoa nyumba 45. Nafikiri Ofisi ya Waziri Mkuu tumeshaitaarifu, waende wakaone namna ya kuwasaidia wananchi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uvumilivu

wa kisiasa alionao. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa malezi mazuri aliyopata toka kwa wazazi wake na kwa kweli aendelee kuwa na msimamo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma hii hotuba sijui siku hizi Mheshimiwa Freeman Mbowe ana tatizo gani, nasema sijui kuna shida gani? Hotuba yake imejaa uchochezi mtupu. Hotuba yake inamlazimisha Waziri Mkuu atoke kwenye msimamo wake na ustaarabu wake aige tabia za Mbowe hivi inawezekana jamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka niseme, hii hotuba ingawa nimeshangaa sana Mwanasheria mmoja wiki iliyopita, Mheshimiwa Tundu Lissu, anatuonya kwamba eti hatuna madaraka ya kuichangia, ila wao wana madaraka ya kuchambua hotuba ya Waziri Mkuu, lakini sisi hatuna madaraka ya kuichambua hii hotuba ya Mbowe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utashangaa, wakipata Serikali hawa watakuwa watu wa namna gani. Kama leo unaweza kusimama Bungeni, ukasema Wabunge wengine wote wa vyama vyote wasitoe majibu wala kuichambua hotuba ya Mheshimiwa Mbowe ila wachambue ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hao ndiyo wasomi wetu tulionao sasa, wakipata Serikali hao watakuwa wakatili kupita kiasi. Kwa hiyo, unaweza ukashangaa kuona hao ndiyo viongozi leo hii wanasifiwa kwenye mitandao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Alhamisi silaha ya msaada ilipiga sana, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba ambaye sisi wote tulikuwa naye JKT, alipiga vizuri. Leo tu nataka kutumia *machine gun* kumaliza maliza na sana sana nitatumia singe kwa ajili ya kumaliza wachache waliobaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanasimama hapa wanazungumzia habari ya ugaidi. Tena kuna Mbunge mmoja wa Mkoa wa Singida, yeye ndiye mfadhili mkubwa wa wananchi wake baadhi wasiokuwa waaminifu wanatengeneza magobole. Serikali imeshaanza kuchukua hatua pale, lakini akisimama humu fulani gaidi, fulani gaidi,

Serikali hebu shughulikeni na watu wa namna hiyo. Hakuna sababu ya kupoteza muda, tushughulike na watu wanaotaka kuvuruga amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema mwanzoni niliwambia na leo niwakumbusheni, nilisimama kwenye Bunge hili nikasema, kipo Chama kinapewa fedha na wafadhili, wakaseme ooh Lusinde siyo mtafiti, juzi si mmeona wenyewe, wanapokea hela hadharani kwa ajili ya kufanyia kazi zao hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kwa uchungu mkubwa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Aah tayari dozi imeshaingia. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa muda mfupi sana Mheshimiwa Wenje, nina wachangiaji wengi, endelea!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa bwana Lusinde kwamba ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje kanuni zinatulazimisha kabisa na kututaka kila mtu humu ndani aitwe Mheshimiwa.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa kwamba, katika nchi hii vyama vyote kikiwemo Chama cha Mapinduzi kina mahusiano na Vyama vingine vya nje. Msaada tuliopata ni wa *capacity building* siyo msaada wa kufanya hayo mawazo finyu anayofikiria yeye. Msaada wa kufanya *capacity building* na ndiyo tulipokea hadharani, siyo msaada wa kufanya vitu ambavyo vipo kwenye giza. Nampa hiyo taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo. Mheshimiwa Lusinde unapokea taarifa hiyo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani huyu mtu bado amechanganyikiwa na uchaguzi wa Kenya. Uchaguzi wa Kenya umemchanganya kwa sababu hakuna sehemu niliyotaja CHADEMA. Nimesema kuna Vyama vya Siasa vinapokea fedha, kama Vyama vya Siasa na CCM ni Chama cha Siasa. Sasa sijui anawasha na kitu gani, anajua yeye mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Kuna vitu vya msingi ambavyo tunataka kuzungumza. Tunataka tuzungumze habari ya uendeshaji wa nchi, tuzungumzie maendeleo ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Serikali kwa kutupatia umeme kwenye Jimbo la Mtera kwenye baadhi ya vijiji vitatu, tumepata umeme Kijiji cha Iringa Mvumi, Mloa barabarani na tumepata umeme kwa mara ya kwanza katika Kijiji cha Makano. Hata hivyo, tuendelee kuisihi Serikali iendelee kusambaza umeme kwenye Jimbo la Mtera. Tumetuma maombi Wizarani tukiomba umeme utoke Mvumi *mission* upite Ndegwe, uende Handali, uende ukaishie katika Kata moja inayoitwa Ng'ahereze.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini awamu ya pili, tukasema utoke pale Muungano uliopo porini uende kwa wananchi na ukitoka pale uende Kijiji cha Ilolo ili wakazi wa Jimbo la Mtera wanufaike na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine, nilisema wakati tunaanza Bunge na sasa nataka niwakumbushe Serikali, hebu wakubwa wengine wote fanyieni kazi ya kuendesha nchi. Mawaziri msishughulike na hawa watu ambao hawaoni, wanaona lakini wanajifanya hawaoni. Kazi hii tuachie mimi na Mheshimiwa Mwigulu, hawa tunawamudu, shughulikeni na kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna watu wanataka kuvuruga amani kwenye nchi hii, wakati wana watoto wachanga. Nashangaa, mtoto wangu wa mwisho ana

miaka nane, mtoto wa Slaa wa mwisho sijui ana wiki ngapi, amezaliwa juzi, lakini bado mnataka kuvuruga amani ya nchi hii. Ni mambo ya ajabu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hebu simamieni amani, watu wafanye maendeleo. Juzi hapa kuna watu wanauliza swali, ooh kuna akinamama sijui walemavu wanapewa mimba zisizotarajiwa, kuna Wabunge hapa wana mimba zisizotarajiwa na itafika mahali tutawataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka tuseme kwamba, ikifika mahali tutasema, msizungumze tu watu wa nje, tunawasingizia bure wananchi wakati wapo Wabunge wamebeba mimba zisizotarajiwa hivyo hivyo. Sasa kwa hawa tutachukua uamuzi gani? Kwa hiyo, tusitake kuwadanganya wananchi kwamba, wao ndio wanaishi kwenye mazingira magumu wakati hata humu ndani kuna mazingira magumu vile vile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie kuhusu maji ya Benki ya Dunia. Maji ya Benki ya Dunia yasisubiri wafadhili, pale ambapo wamechimba sisi tuendelee kwenda mbele ili wananchi wetu wapate maji. Kwa hiyo, nataka nichukue fursa hii kuiomba Serikali, iongeze bajeti kwenye bajeti ya maji badala ya kusubiri Benki ya Dunia tuhakikishie na sisi tunawapatia wananchi wetu maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie barabara ya lami. Inajengwa barabara ya lami kutoka Dodoma Mjini kwenda Iringa, lakini tukubaliane kwamba Hospitali Teule ya Wilaya Chamwino ambayo ipo Mvumi *Mission,* baada ya barabara ile kukamilika hatuombi Mungu, lakini ajali zitakuwa nyingi sana. Watu wengi watakaopata matatizo pale watakimbilia hospitali ya Mvumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amwagize Waziri wake wa barabara, achepue barabara ya lami kutoka Kijiji cha Mloa ili ipite Makang'wa ije Mvumi *mission* ili iwe tayari kwa ajili ya kupokea mambo mbalimbali yatakayotokea kwenye

barabara kubwa ya ile lami. Tuna hospitali kubwa pale ya macho, watu wengi wakishatibiwa pale macho wengine wanapata upofu kwa sababu ya vumbi. Ndiyo maana tunasisitiza, Serikali itutengenezee hiyo barabara lami kwenda kwenye Kijiji cha Mvumi *mission* ambako kuna Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za ruzuku. Nataka nimuunge mkono kwa mara ya kwanza mdogo wangu, Mheshimiwa Mbunge wenzangu hapa, Mheshimiwa Felix Mkosamali alisema Serikali ifanye *audit* kwenye Vyama na mimi nasema ifanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi tumesoma magazeti hapa Katibu Mkuu wa Chama kimoja cha Siasa amejikopesha, watu wamegeuza *SACCOS*. Halafu hao hao ndio wa kwanza kupiga kelele. Kwa hiyo, fanyeni *audit* tujue, hizi fedha zinatumika kweli kweli au watu wamegeuza *SACCOS* ya kukopeshana. Kwa hiyo, kuna watu wanatumia vibaya hizi fedha. Mheshimiwa Mkosamali nakuunga mkono, ulizungumza kitu cha maana. Nina hakika Mheshimiwa Kinana hawezi kukopa fedha hizi. Chunguzeni tupate majibu, hawa wanakopa hizi fedha kwa kutumia sheria gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwenye hotuba hii ya Kambi ya Upinzani, imezungumza habari ya Mawaziri kujiuzulu zaidi ya mara saba. Kisa, ni kwa sababu mambo mabaya yametokea. Hapa nataka niseme kwa utaratibu, hebu mnisikilize, ukimwambia mwenzako kwa kidole kimoja, vitatu vinakwambia wewe. Hivi wenzetu nyie ambao kila siku likitokea tatizo mnasema tujiuzulu, nyie alijiuzulu nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo moja ambako kumetokea fujo Tunduma, Mbunge ni wa CHADEMA mbona hajiuzulu ili kuwajibika au mnataka tuwajibike sisi tu! Maana yake wakati mwingine hawa watu wanazungumza vitu ambavyo wao hawawezi kuvifanya, kila siku jiuzuluni, jiuzuluni. Juzi tuliingia kwenye uchaguzi, Kata 28, CCM

tumeshinda Kata 25, nyie Kata tatu, mbona hamjiuzulu kwa kushindwa ili mtekeleze hayo. Kazi yenu yenu jiuzuluni, jiuzuluni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema Waheshimiwa viongozi wa Serikali yetu fanyeni kazi za wananchi, kazi ya hawa tuachieni sisi tunawamudu, hakuna kitu. Nyie mnapita kwenda kuwajibu hawa, mnawajibu kitu gani? Hawa msiwajibu, tuachieni mimi na Mwigulu tunatosha. Hii nchi wanatuelewa na hawa wanatuelewa tukiwaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni kuhusu fedha, nimeendelea kusema na sasa nasema, fedha yetu tukitaka ishindane na fedha nyingine, tuondoe wanyama ndani ya fedha. Tuondoe nyoka, tuondoe chura, tuondoe samba, tuweke sura ya Mwalimu Nyerere na Karume kwisha. Pesa yetu itapata nguvu, itashindana vizuri na kuna viongozi ambao hata hawa Wapinzani hawabishi, ukimtaja Nyerere wote wanakaa kimya, kwa hiyo, tukimweka kwenye hela mle, tumemaliza biashara. Hakuna nchi inayoweza kuendeleza pesa yake ikiwa na picha ya nyoka jamani. Nyoka ni alama ya shetani, mnawekaje kwenye hela, toeni hivi vitu. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli tumefika mahali tunashindwa kuwaenzi viongozi wa nchi yetu tunamuenzi nyoka! Habari ya utalii tulishashauri hapa Wabunge na mimi narudia kushauri, msitangaze utalii kwenye pesa. Tumieni matangazo mengine, kwenye fedha tuweke waasisi wa nchi yetu, viongozi waliostaarabika, wanaoheshimiwa na kila mtu. Leo hii kwenye fedha zetu ukimweka Mwalimu Nyerere na Karume tutakuwa tuna njia na tuna uchumi mzuri na tutakuwa hatugombani na Mungu, lazima tukubaliane kwamba, unajua wakati mwingine hata Mungu anashindwa kutubariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matangazo mengine narudia kuyasema tena hapa, ukiangalia *TV* inakuambia urithi

wetu Safari *Lager*, yaani Tanzania sisi tumerithishwa bia. Sasa kama tumerithishwa bia, Mungu atatupenda kweli? Haiwezekani, sisi tumepata nchi nzuri, nchi ya amani na utulivu. Kwa hiyo, naishauri Serikali...

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kengele ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, kabla sijaanza kuchangia nitoe maelezo mafupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Katiba ya nchi yetu, wote tulijadili vizuri katika Bunge hili, sasa leo nashangaa baadhi ya watu wamekuwa wakizungumza kwamba wana-CCM ndiyo wamepitishwa wengi. Wenzangu wamezungumzia hili jambo, sisi ndio wengi na hata kwenye uchaguzi ujao mtaona ushindi ni wa CCM. Mfano mdogo upo katika Mkoa mmoja tu wa Njombe, tulikuwa na Vijiji vya uchaguzi 42, Chama cha Upinzani kimechukua Kijiji kimoja, sasa leo mtashinda wapi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga sekondari nyingi tu katika nchi hii na baadhi ya watu wakasema hizi ni yeboyebo. Hivi tusingejenga hizi sekondari kwa kushirikiana na wananchi, leo hawa watoto wangekuwa wapi? Mkoa wa Iringa nilisema mwaka jana, uko nyuma, historia inatuonesha tulikuwa na sekondari moja, leo tuna sekondari 248, lazima tujipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze katika kuchangia; kuhusu sekondari naomba sana Serikali ihakikishe angalau inapeleka fedha kwa ajili ya kujenga maabara zote katika sekondari zetu, katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo, naishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo ilivyokuwa ikipeleka pembejeo katika vijiji vyetu na Wilaya zetu. Lakini niseme tu kwamba, mpango ambao Serikali imeweka kwa msimu huu unaokuja ni vizuri tukapeleka elimu mapema ili wananchi hawa watakapopata elimu hii iwawezeshe kukopesheka kama Wizara ya Kilimo inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Afya juu ya ugawaji wa dawa wa zahanati na vituo vya afya, mfumo huu umepitwa na wakati. Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana na hili ninalosema. Zahanati kwa nchi nzima zinapata dawa bila kujali wingi wa watu. Zaidi ya miaka 20 mfumo ni ule ule na vituo vya afya hali kadhalika ni hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ya Afya ibadilishe mfumo. Leo hii kituo cha afya cha Makambako, dawa wanazopata ni hizo hizo walizokuwa wanapata zaidi ya miaka 20, wakati ule kulikuwa na takribani watu 15,000, leo wako zaidi ya watu 150,000, mgao wa dawa ni ule ule. Niiombe sana Serikali ibadilishe mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Wizara hii ya Afya kupitia Waziri Mkuu, Makambako pale tumekuwa tukiomba sana kituo hiki kipandishwe hadhi na kuwa hospitali. Rais alipokuja alikubali jambo hili, sijajua linakwama wapi, nimefuatilia mara nyingi. Naomba sana kituo hiki kipandishwe hadhi na kuwa hospitali. Kwa sababu vile vitu ambavyo walituagiza tumeshatekeleza, Waziri wa Afya yuko hapa, naomba sana tupate kibali cha kuwa hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pale Lupembe pia tumepata fedha ya kujenga hospitali kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, ujenzi kwa maana ya miundombinu. Naishukuru sana Wizara hii kwa namna ambavyo tumekuwa tukiomba sana barabara ya kutoka Njombe kwenda Lupembe kwenda Ikondo mpaka Morogoro,

sasa tumepata fedha kazi itakapokamilika, barabara hii kwa sababu ni barabara ya kiuchumi sana katika Wilaya ile na katika Mkoa wa Njombe kwenda Mkoa wa Morogoro ni kiunganisho, tupate fedha za kuweka barabara ile iwe barabara ya lami. Watu wa kutoka Songea badala ya kuja Iringa watapita njia ile ya mkato kutokea Morogoro itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni tete sana katika Mji wetu wa Makambako na Mkoa wetu wa Njombe. Mwaka jana tumepata matatizo makubwa sana kuanzia mwezi Septemba, Oktoba, Novemba na Desemba, hatukuwa na maji kabisa. Naomba sana katika bajeti ya Wizara hii tutenge fedha za kutosha ili tuweze kupata maji ya kutosha katika Mji wa Makambako na Mkoa mzima wa Njombe. Kwa sababu vyanzo vipo vya kutosha, tatizo tu ni miundombinu ambayo ni ya siku nyingi. Wakati ule walikuja wasanifu, gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni 57. Niombe sana Wizara hii iweze kutenga fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la usalama na ulinzi, jambo hili Serikali inatakiwa isimamie vya kutosha, wako watu ambao kazi yao ni kuvuruga amani ya nchi hii kwa maslahi yao. Niiombe sana Serikali isimamie, tusiwe na kigugumizi, watu wanapovuruga amani wachukuliwe hatua bila kujali wadhifa wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie umeme, katika Mji wetu wa Makambako, tulibahatika kupata umeme wa *MCC*. Naibu Waziri yuko hapa, alishatuahidi kwamba, kufika mwezi Mei umeme huu utakuwa tayari, mpaka leo hakuna kinachoendelea. Wananchi wana imani kutokana na Naibu Waziri alipopita pale na kuzungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mpango ule wa mradi mkubwa wa kutoka Makambako kwenda Songea, umepita kwenye vijiji vyangu, mradi huu uanze maana unapitia Madaba pale unakwenda Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafao ya wastaafu; mafao haya ya wastaafu yamepitwa na wakati kwa sababu mafao aliyokuwa anayapata zaidi ya miaka kumi mpaka leo bado anapata hayo hayo. Niombe sasa yaendane na wakati kwa sababu gharama zinapanda kila kunapokucha. Kwa hiyo, naomba sana mafao haya ya wastaafu yaendane na wakati, itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, unajua unapolea mtoto yatima, wengi hapa tunakaa na watoto yatima au watoto ambao sio wewe siye uliyemzaa, siku zote hata ungemhudumia kiasi gani, atalalamika kwamba sihudumiwi. Sasa ni sawa na wenzetu hawa, hawaoni mambo yanayotendeka. Mambo ni makubwa sana, Serikali ya CCM inayafanya, hawasikii, hawaambiliki hivi ni kwa nini? Lazima tumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi zuri anayoifanya kama Mwenyekiti wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya, nimalizie kwa kusema kama nilivyosema mwaka wa jana, wako Mashehe humu na Wachungaji, mtuombee ili tuishi kwa upendo na amani. Sisi ni kitu kimoja ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na CCM itaendelea kutawala. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Mheshimiwa Mohamed Missanga atafuatiwa na Mheshimiwa... Mheshimiwa Magdalena Sakaya, samahani sikukusikia.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 64(1)(g), Mheshimiwa aliyeongea kabla ya Mheshimiwa Sanga, Mheshimiwa Livingstone Lusinde ametumia kauli ambayo sio sahihi ndani ya Bunge...

**NAIBU SPIKA:** Hebu soma hiyo 64(1)(g) inasemaje?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, inasema kwamba kwa kuokoa muda "Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine".

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lusinde alivyochangia, ametamka ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba, wapo Wabunge ndani ya Bunge hapa wana mimba ambayo haikutarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ni viongozi na tunaomba athibitishe ni Mbunge gani ambaye amebeba mimba ambayo haikutarajiwa, vinginevyo afute kauli. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sikutarajia kama Waheshimiwa Wabunge mnataka kuvuana nguo hadharani, nitatoa Mwongozo wangu baadaye. Mheshimiwa Mohamed Missanga atafuatiwa na Mheshimiwa Kandege.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba, nilitaka nichangie kwenye hotuba hii ya Wapinzani, lakini baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Mwigulu, sina sababu ya kuharibu raha zote ambazo zimesemwa hapa, niwatakie kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia bajeti ya mwaka 2013/2014. Kabla ya kufika huko ni vizuri kuangalia tumefanya vipi katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Kwa kiasi kikubwa hatukufanya vizuri na moja ya sababu kubwa ambayo imefanya tusifanye vizuri ni kwamba, fedha kwenda kwenye Wizara zetu ambazo zilikuwa na miradi kadhaa, fedha kwenda kwenye Halmashauri zetu ambazo zilikuwa za miradi kadhaa, hazikwenda na wala hazikwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa kwenye Kamati, tumekuta Wizara nyingi tu mpaka wakati mwezi Februari walikuwa wamepata asilimia 20 au 30 na mpaka sasa bado ziko Wizara ambazo zina asilimia 30, Halmashauri asilimia

40, wachache walipata asilimia 50. Halmashauri yangu ya Wilaya ya Singida mpaka sasa wamepata asilimia 50. Kwa hiyo pamoja na kupanga mipango ya mwaka 2013/2014, tunajifunza kwamba, yale ambayo tunapanga kwenye Bunge, wenzetu hawayatekelezi. Kuna sababu gani ya kukaa hapa miezi miwili au mitatu tukapitisha mambo, halafu Serikali haiendi kutekeleza, inawezekana kuna Bunge lingine huko linakaa kusema kwamba mpe huyu, mpe yule, mnyime huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Bunge hili liheshimiwe, yale ambayo tumekubaliana kwenye Bunge hapa yatekelezwe. Nasema hivyo kwa sababu katika taarifa ya Waziri wa Fedha, mapato ya ndani kupitia *TRA* mpaka mwezi Februari ilikuwa asilimia 96. Nina hakika mpaka sasa imefika zaidi ya asilimia 100, misaada na mikopo ilikuwa imevuka asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama fedha zimepatikana na hazikwenda Halmashauri na wala hazikwenda Wizarani zimekwenda wapi? Kwa hiyo, nasema hili sio zuri, ndiyo maana miradi inachelewa kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zinaanzishwa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla, kuharakisha kuanzisha Halmashauri ya Ikungi, kwa sababu Halmashauri ya sasa ya Wilaya ya Singida ina Waheshimiwa Madiwani zaidi ya sabini.

Kwa hiyo, ni vigumu sana kufanya kazi kwa mafanikio na hasa ikizingatiwa kwamba fedha zenyewe haziendi kwa wakati kama nilivyokuwa nimesema. Niombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamjali, tunamheshimu na katika hali hiyo pia atuone ili Halmashauri ya Ikungi ianzishwe kuondoa tatizo lililoko kubwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Mkoa wa Singida una barabara nzuri, lakini suala la uwanja wa

ndege ni jambo muhimu, tunakosa baadhi ya wafadhili kwa sababu hatuna uwanja wa ndege. Mfadhili na mhisani hawezi kutoka Dar es Salaam mpaka Singida masaa kadhaa, yeye ana muda mdogo, anataka afanye arudi. Ningeomba sana uwanja wa ndege wa Singida ukamilishwe kama ambavyo imeelezwa siku moja na Mheshimiwa Waziri hapa kwamba katika viwanja 10 ambavyo vitafanyiwa kazi na kiwanja cha Singida kiwemo katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile reli ya kutoka Manyoni kwenda Singida ni kwa muda mrefu haifanyi kazi hadi sasa. Ningeomba sana Serikali ihakikishe kwamba, reli hii ambayo Mwalimu Nyerere aliihangaikia na akahakikisha mpaka ikajengwa, nayo ifufuliwe ili kusudi wananchi wafaidike na kazi nzuri ambayo ilifanywa na hayati mzee wetu Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha *RCC* tumewasilisha maombi Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu daraja moja linaloitwa daraja la Minyuhe. Ni daraja kubwa na refu ambalo linahitaji fedha nyingi. Halmashauri yangu ya Wilaya ya Singida haina uwezo hata kama ni kwa miaka kumi. Niombe sana maombi yale ambayo yamewasilishwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya daraja la Minyuhe ambalo kwa hivi sasa mvua inanyesha sana Singida, wananchi wa Kijiji cha Mtavila na wengineo hawaendi kabisa mjini, hawaendi Singida, hawaendi Makao Makuu ya Kata kwa sababu ya tatizo la daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri haiwezi kufanya kitu kama hicho. Kwa hiyo, naomba maombi yale ambayo yamewasilishwa na ambayo yamebarikiwa na *RCC,* Ofisi ya Waziri Mkuu iyashughulikie, daraja hili lijengwe ili wananchi wale wajione ni miongoni mwa wananchi ambao wanastahili kupata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianzisha hapa Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Toka tumeanzisha Bodi hii sijaona kazi ambayo imefanywa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko na sijasikia chochote kabisa. Sasa tunaanzisha vitu humu ndani,

lakini havifanyi kazi. Yako mambo sijui ya *mortgage financing* ambayo tunaanzisha humu, lakini ukiuliza mpaka leo hamna kitu. Tumeanzisha *lease financing,* hamna kitu, sijui *unit title* hamna kitu. Sasa vitu hivi vilianzishwa ili kusaidia Mtanzania apate maisha bora. Rais aliposema kwamba wananchi wapate maisha bora ni kwa kutengeneza sheria, sera na taratibu nzuri kama hizi ambazo tumefanya. Lakini kama tunatengeneza, tunatunga hapa na hazifanyi kazi, ni jambo la kusikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko imekufia wapi, sijasikia chochote. Tulitegemea Bodi kama hii hasa sisi watu wa Singida ambao tunalima alizeti, ufuta, dengu, karanga, vitunguu na tuna asali, hiyo ndiyo Bodi ambayo ingetusaidia sana. Lakini haijatusaidia chochote katika upande wa mbegu, utaalam na hata upande wa masoko wananchi wengi wanalanguliwa na baadhi ya watu. Ningependa sana Bodi ya Mazao ya Mchanganyiko ifanye kazi yake sawa sawa ili kusudi tuweze kunufaika na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi majuzi tumekamilisha zoezi la sensa. Sensa imetumia fedha nyingi na matokeo yake yamepatikana. Moja ya faida ya sensa ni kupanga mipango. Katika mipango mingine ambayo itapangwa na Serikali, naomba, Serikali iangalie kasi ya ongezeko la watu. Kasi ya ongezeko la watu haiendani sambamba na kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa hapa na hata msemaji mmoja alisema hapa asubuhi, uchumi unakua kwa asilimia saba, lakini ongezeko la watu ni kubwa sana, ndiyo maana hata mwingine amesema hapa, ingawa uchumi unakua, lakini mifukoni mwa wananchi, hakuna kitu. Hakuna kitu na inawezekana moja ya sababu ni kwamba, wakati uchumi unakua lakini watu nao wanaongezeka zaidi. Kwa hiyo, kinamezwa kile ambacho kingepatikana, kingegawiwa kama idadi ya watu ingebaki ile ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii ningeomba sana, moja ya kazi ambayo ningeomba Serikali ifanye ni kuangalia kasi ya ongezeko la watu, ni kubwa sana. Wataalam wa sensa wanasema ikifika miaka 26 ijayo tutakuwa watu milioni 90. Hebu niambie milioni 90 na uchumi wenyewe unavyokua hivi si ndio hali itakuwa mbaya zaidi!

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanasiasa si rahisi kwenda kwenye Mkutano wa hadhara, mimi kama Bwana Missanga Mwanasiasa na Mbunge unasema jamani eeh tunaongezeka sana ebu tupunguzeni mambo yale, haiwezekani, siwezi kusema kitu hicho, nitakuwa nimejimaliza mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe viongozi wa Serikali, Mawaziri, lakini niwaache Mawaziri kwa sababu na wao wanachaguliwa kama sisi wengine, lakini Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi watusaidie kuieleza hii athari ya kuongezeka kwa kasi kubwa kwa watu, sisi wanasiasa pengine si rahisi sana unaweza ukajimaliza wenyewe. Lakini kubwa ni kwa Serikali ijizatiti kutunga sera, kutengeneza Sheria ambazo kwa kweli zitaangalia suala zima la kukua kwa kasi kubwa na kuongezeka kwa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Zarina Madabina na baada ya hapo Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi na mimi nichangie hoja iliyoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye suala la kilimo. Ukitoka Rukwa bila kusemea kilimo, itakuwa kama vile umesahau umetoka wapi. Naipongeza Serikali kwa kubaini kwamba, utaratibu uliokuwa unatumiwa wa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima, umetufikisha

mahali ambapo haufai tena. Kuanzia sasa hivi Serikali imesema itaandaa utaratibu wa kuhakikisha kwamba, wananchi wanakopeshwa. Rai yangu kwa Serikali; jambo hili jema ni vizuri vikundi vikaundwa mapema na pembejeo zikasambazwa kwa wakati ili ziwafikie wananchi. Pia isije ikawa inalenga wananchi wakulima wadogo, bali wakulima wa kati na wale wakubwa. Kwa sababu kama tunataka kufanya mapinduzi ya kilimo maana yake lazima tuwalenge wakulima wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilima mahindi ya kutosha, bahati nzuri soko la uhakika lipo. Majirani zetu wote wanategemea sisi tuwalishe. Sasa ni vizuri tukatumia fursa hii kuhakikisha kwamba tunazalisha chakula cha kutosha. Niiombe Serikali pamoja na kuanzisha utaratibu huu wa kukopesha pembejeo, lakini ule mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba matrekta yanakuwepo mbona siusikii, umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ifanywe sensa kujua ile Mikoa inayozalisha na hasa ukianzia na Rukwa matrekta mangapi yameenda na Kalambo yamefika mangapi ili kuweza kuhakikisha kwamba *mechanization* inafanyika ili tufanye kilimo kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuongeza thamani ya mazao. Haitafaa tukiishia kuzalisha tu mahindi bila kuongeza thamani. Utakumbuka katika swali langu niliuliza je, Serikali ina mpango gani wa kufanya tathmini kujua bei halisi ya mahindi pamoja na bei ya sembe? Mwananchi wa kawaida anayeuza mahindi kwa shilingi 35,000/- ikipanda sana inafika 50,000/- analazimika kuja kununua gunia moja kwa shilingi 90,000/- na wakati huo huo sembe inafika mpaka shilingi 1,300/- na zaidi kwa kilo, nini tafsiri yake? Ni kwamba huyu mkulima wa kawaida, hafaidiki na kilimo anachokifanya na wala haoni tija ya kufanya kilimo. Kwa hiyo, ninachoomba kuwe na kuongeza thamani ya chakula kwa maana ya kwamba, tusage mahindi tuuze yakiwa tayari yameongezwa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangazwa sana na mambo mazuri ambayo yalibuniwa na waasisi wetu, jinsi ambavyo wachache wanatafuta namna ya kujinufaisha. Namaanisha nini? Ulikuwa mpango mzuri sana juu ya kuanzisha Shirika la Usagishaji la Taifa *(NMC)* na bei za unga zilikuwa controlled, sisi wote mashahidi. Lakini leo ukienda Arusha, Shirika la *NMC* lililokuwa linafanya kazi nzuri sana, utashangaa unaambiwa kwamba eti kuna mwekezaji ambaye amepewa mali ya Watanzania, asage yeye na hata *milling charge* halipi. Hili Serikali mnalijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mali ya Watanzania anapewa mtu mmoja, kwa hiyo wala hana uchungu kwa Watanzania ataweka bei yoyote ya sembe kwa sababu yeye amechukua bure. Lakini ukienda katika mipango unaambiwa kwamba tuanze kujenga *godowns na* ***silos****.* Hizi zilizopo tunazitoa bure leo tunalazimika kujenga godowns nyingine. Naomba Serikali ihakikishe kwamba mkataba huu ambao haupo usitishwe mara moja na *NMC* Arusha itumike kusaga sembe ambayo itakwenda Magereza, itakwenda kwenye Majeshi yetu na sio kumsaidia mtu binafsi peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee suala la sekta ya mifugo na uvuvi. Uvuvi *contribution* yake kwa *GDP* ni ndogo sana, aibu! Tunachoambiwa asilimia inayotokana na uvuvi sana sana inategemea Ziwa Victoria na kwa kiasi kidogo sana Ziwa Tanganyika. Ukienda katika Bahari Kuu, *contribution* yake ni ndogo sana. Naitaka Serikali ihakikishe kwamba, maliasili hizi tulizonazo zinatumika kwa kuwawezesha wavuvi wavue kisasa na kuhakikisha kwamba, tunapata mazao ya samaki na kuongeza *GDP* ya Serikali na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika ukienda kwa upande wa mifugo, wapo ndugu zangu Wasukuma wako wengi kweli kwetu kule. Lakini nini ambacho tunapata faida kutokana na mifugo hiyo? Hakuna, kwa sababu thamani ya kwenye ngozi haiongezwi, lakini pia hata hiyo nyama, mpaka waje wasubiri mnyama anategemea kufa ndiyo anapelekwa

kwenda kuchinjwa. Hatuwezi kwenda kwa mtindo huu, tuhakikishe kwamba thamani inaongezwa kwa ngozi na hali kadhalika kwa nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kiwanda kimoja tu ambacho nakifahamu cha kusindika nyama cha ndugu yangu Mzindakaya pale. Tungekuwa na viwanda vingi na bei ya ng'ombe ikawa nzuri, maana yake faida ya mifugo hii tungeiona. Lakini si kwa mtindo huu. Natoa *challenge* kwa Waziri anayehusika, ahakikishe kwamba anatoa *contribution* kama anajihakikishia kuwepo kwake, vinginevyo tutakuwa hatuna sababu ya kuwa na Wizara ambayo haina mchango kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala la miundombinu. Wengi wamekuwa wakiongea, wanalalamika kwamba Serikali inakopa sana, lakini mimi nadhani *essence* sio Serikali kukopa sana, cha maana Serikali inakopa kwa ajili ya nini? Hayo ndiyo ya msingi ya kujiuliza. Ni busara kubwa sana kwa Serikali yetu kukopa na kuhakikisha kwamba inawekeza kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati na Reli ya TAZARA. Lazima tuhakikishe kwamba tunawekeza kiasi cha kutosha ili kuzinusuru barabara zetu. Wenzetu upande wa pili Zambia, reli ya *TAZARA* wameshaanza kuchangamka wanajenga kwenda Mpulungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niisihi Serikali ihakikishe kwamba na sisi tunaanza ujenzi wa *extension* kutoka Tunduma kwenda mpaka Kasanga *Port,* maana yake tutakuwa tumejihakikishia kusafirisha mazao ya kutosha na tuta-*take* ile *opportunity* ya kuwa karibu na *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalia, hii habari ya kukarabati njia ya *central line* kwa vipande vipande hatuwezi kufika. Hebu twende tukakope tuhakikishe kwamba *central line* inafanya kazi kwa ajili ya kuinua uchumi wa Taifa hili. Wala haji mtu kutulaumu kwamba kwa nini tulikopa kwa sababu tutakuwa na sehemu ya kumwonesha kwamba

tumekopa tukafanya hili. Hilo litakuwa na maana kubwa sana katika kukuza uchumi. Kwa hiyo, tusiogope kukopa, cha msingi tukope kwa ajili ya kufanyia kazi ya maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kwenye upande huo huo wa miundombinu. Nilikuwa nashangaa juzi jinsi ambavyo Serikali inavyotaka kutuchonganisha sisi wananchi wa Rukwa na wa Katavi. Ni muda mrefu sana alisema ndugu yangu Mheshimiwa Keissy pale kwamba uwanja wa ndege wa Sumbawanga haufai na juzi tulikuwa na viongozi, si lazima nitaje. Lakini tunachonganishwa pale ambapo kiongozi akitaka kuondoka kwa ndege, eti inabidi atembee kwa gari mpaka Mpanda ndiyo akapande ndege. Hii ni aibu, sisi ndiyo tumeizaa Katavi, haiwezekani mwendelee kutuchonganisha. Naomba katika viwanja vichache hata kama ni viwili vya kuanza kuweka lami, cha Sumbawanga kianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uanzishwaji wa maeneo mapya ya kiutawala, jambo jema sana...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Baada ya Mheshimiwa Kandege nilisema atafuata Mheshimiwa Zaynab Madabida na Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae. Mheshimiwa Zaynab Madabida!

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jina langu naitwa Zarina Madabida.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana, narekebisha Zarina Madabida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu. Katika mchango wangu nitajielekeza katika kitabu cha Waziri Mkuu ukurasa wa 52 na 53 ambao

unazungumzia usafiri wa barabara katika Jiji la Dar es Salaam na hususan nataka kujielekeza katika kuondoa msongomano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala ambalo linaeleweka kwamba msongamano wa Dar es Salaam kusema kweli ni mbaya sana na pia hatuwezi kukataa kwamba Serikali imefanya kazi nzuri sana kujaribu kuondoa msongamano huo. Lakini niliposoma kitabu hicho mwanzo mpaka mwisho nimeona kuna upungufu mkubwa sana kwa sababu pamoja na kuondoa msongamano huo inakuwa kama Wilaya ilikuwa inaangaliwa kivyake. Lakini ukiangalia miundombinu iliyopo Dar es Salaam na ofisi zetu, haipo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Wilaya ya Kinondoni, kazi kubwa sana imefanyika katika kupanua barabara na kufungua sehemu mbalimbali. Lakini daraja la *Surrender* liko vile vile. Huku nyuma kuna barabara nyingi zinakuja *Surrender Bridge* na mbele kuna barabara nyingi zinatoka. Inakuwa kama vile unajaribu kuyalazimisha maji ya kwenye chupa kubwa kupita kwenye mdomo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile ukienda katika daraja la gerezani pale relini kwa watu wanaotoka Kurasini na lenyewe lina tatizo hilo hilo. Sasa nimeangalia humu sikuona kusema kweli mahali panapoelezea hiyo. Vile vile katika makutano ya barabara mbalimbali. Bila kupanua *Surrender Brigde* hata kama tutafanya kazi gani, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu, hatutaweza kuondoa msongamano, halikadhali kwenye daraja la gerezani. Kwa hiyo, naomba masuala haya ni nyeti sana, Dar es Salaam watu wanapoteza muda mrefu sana kufika maofisini na kurudi majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu msongamano wa Dar es Salaam kama ambavyo tunauona barabarani ndio na msongamano ulivyo katika kutoa huduma. Dar es Salaam ina wakazi takribani milioni 4.3 kufuatana na sensa iliyofanyika

hivi karibuni. Lakini pia Dar es Salaam inachangia zaidi ya asilimia 80 ya makusanyo. Lakini najua kwamba, Dar es Salaam inaweza ikatoa mchango mkubwa zaidi kuliko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam ina Wilaya tatu tu na kwa kuona kwamba kweli Dar es Salaam ina tatizo ndiyo maana unakuta watu kama Polisi wameanzisha Kanda Maalum. Maana yake kuna Mkoa wa Ilala, Mkoa wa Kinondoni na Mkoa wa Temeke. *TRA* ina Kanda Maalum; Temeke, Ilala na Kinondoni na sehemu nyingi sana wanajaribu kufungua kwamba wapate mikoa mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo inamaanisha ukichukua na *population* ya Dar es Salaam kwa idadi ya watu, inamaanisha kwamba aidha tunahitaji Mikoa mitatu au angalau basi tuongeze Wilaya ili kuweza kukidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mtu anayetoka Pemba Mnazi mpaka kufika kwenye Wilaya ya Temeke inamchukua si chini ya masaa manne. Maana yake kutoka pale mpaka *ferry* ni saa moja na nusu kwenda. Kutoka *ferry* mpaka aje kufika Temeke au kama akizunguka Kongowe hali ni hiyo hiyo wakati anazikuta foleni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, mtu anayetoka Mvuti anakwenda Ilala anachukua muda mrefu sana halikadhalika na Kinondoni, Jiji ni kubwa sana. Matokeo yake ni nini? Serikali inapoteza mapato mengi sana na makubwa sana ambayo hayakusanywi. Nani anakusanya kodi za majengo? Mpaka leo, wote tunakiri kabisa kwamba, kuna hela nyingi sana za kodi za majengo ambazo hazikusanywi kwa ajili ya *centralization* ambayo kama tungeongeza Wilaya zingeweza kumudu kufanya masuala ambayo yanafanywa *centrally*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe rai, ukichukua *population* ya Dar es Salaam ukalinganisha na *population* ya Tanzania, ina asilimia 10. Ungefikiria basi Dar es Salaam ingekuwa na Wilaya asilimia 10, ambazo ni Wilaya 16. Lakini tunasema tufike huko, basi angalau tufike hata

Wilaya tisa ama kumi. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI waliangalie hilo kwa uzito wake na kwa manufaa ya Watanzania wote kwa sababu itasaidia kwenye makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nigusie kidogo, nataka Waziri Mkuu akija atueleze suala la UDA limefikia wapi? Maana tunajua tu kwamba, UDA ilipelekwa kwa *CAG* na alitoa ripoti, hii ripoti inasemaje? Suala la UDA likoje? Naomba kupata majibu ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nataka nigusie kidogo ajira kwa vijana. Tungeweza kutengeneza ajira nyingi sana kwa vijana kama kilimo kingetumika kusaidia hilo na kingetumikaje? Leo hii huwezi kumwambia kijana nenda kalime kwa sababu kilimo hakina tija na huwezi kumwambia alime kwa kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isiende kutengeneza na kutayarisha maeneo makubwa pamoja na kuwapatia mbegu na pembejeo zote, halafu wakawakatia wale vijana walime. Lakini baada ya kuwapa mbegu, mbolea pamoja na chakula kwa kipindi cha mpito ili kusudi watakapovuna na mavuno yakawa na tija na wengine watakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi juzi juzi kuna vijana wa kutoka Chuo Kikuu ambao waliji-*organize* wao wenyewe wakaenda kushiriki kwenye kilimo na matokeo yake tumewaona; vijana wengi wapo wasomi, ambao wangeweza kujishughulisha na masuala kama hayo, lakini hawawezi kwenda kwa sababu hakuna tija. Naomba hilo tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee suala la elimu. Naona tunalumbana, lakini nafikiri hili suala la elimu ni suala mtambuka kwa mzazi, Mwalimu na Serikali. Wazazi tumeacha sasa hivi kushughulika na elimu ya watoto wetu. Hivi unampeleka mtoto wa mwaka mmoja *boarding* akafanye nini, kama sio mzazi kushindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba nipatiwe majibu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Zarina Madabida. Mheshimiwa Juma Nkamia atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu ya Bajeti 2013/2014. Nianze tu na jambo ambalo limetokea leo hapa ndani kuhusu suala la Chuo Kikuu cha Dodoma. Naamini haya yaliyokuwa yanasemwa humu ndani kuna kanda, kuna nini *let us think forward* kwamba, chuo kile kimetulia. Kama tatizo la Chuo Kikuu cha Dodoma ni Profesa Kikula na Mlacha kwa sababu ya dini zao, tusilete jambo hili tukaharibu mazingira na mandhari nzima ya Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasoma pale pia. Kwa hiyo, jambo hili linalosemwa humu sijalisikia hata kidogo. Lakini kama *issue* ni Mlacha na Kikula kwa sababu ya dini zao, pengine hatuna utamaduni wa kujua kwamba hawa nao wanaweza kuongoza, ndiyo tunazusha maneno haya. Sidhani kama angekuwa Lyimo kungekuwa na maneno maneno ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri jambo hili tuliache, chuo kile kimetulia, vijana wanasoma na kina maendeleo makubwa. Hizi kanda za kutengenezea vichochoroni, tuachane nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili naomba nizungumzie barabara kidogo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** La Lwakatare?

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Sugu naomba uwe na heshima mimi ndiye ninayeongea na wewe unajua kabisa mimi siongei na mbwa, naongea na mwenye mbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Serikali barabara yetu kutoka Iringa – Dodoma, Dodoma – Arusha inakwenda vizuri. Naamini kabisa kwamba baada ya muda, Mkoa wa Dodoma utaendelea vizuri sana. Lakini naomba nishauri tu, tunapotengeneza barabara hii kufungua *central corridor* nadhani upo umuhimu sasa wa Serikali kufikiria zaidi kwamba upo umuhimu wa kuifanya Dodoma kuwa *Dry Port*.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Machali kwa dakika chache sana kwa sababu muda wetu upo kwa ajili ya wachangiaji, kwa hiyo, kila dakika tunazozichukua tunawapunguzia hawa wanaojiandaa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kuomba kuhusu utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68, lakini ninajielekeza kwenye Kanuni ya 64(1)(g) kwamba: “Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine”. Mheshimiwa Mbunge, Juma Nkamia amezungumza kuwa hazungumzi na mbwa anazungumza na mwenye mbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri ambayo tunaipata hapa mwenye mbwa inaonekana ni Kiti na kwa kuwa amemtaja Mheshimiwa Sugu pale ambaye ni Mheshimiwa Mbunge kuwa ndiye mbwa, ina maana kwamba, sisi Wabunge wote humu ndani ni mbwa. Lugha hii ni ya maudhi na ni lugha ambayo inadhalilisha, mimi binafsi siyo mbwa, nimwombe Mheshimiwa Juma Nkamia aombe radhi kwa kauli yake na asahihishe ili tuweze kuendelea.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**WABUNGE FULANI:** Hujaitwa bado, hujaitwa bado!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nkamia endelea kuchangia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, tuna tatizo sana la kuelewa lugha. Kwa hiyo, nadhani kuwa, mdogo wangu pale haelewi lugha tu, ingetolewa na mtu makini,

ningeweza kuichukua lakini aliyetoa lugha hii kwa kuwa siyo makini, siwezi, ni tatizo la uelewa wa falsafa ya lugha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri kuhusu eneo la Dodoma, mimi natoka Mkoa huu, kwa hakika tunatengeneza barabara ya Iringa - Dodoma na Dodoma – Arusha, nitoe ushauri tu kwa nia njema in *future,* kwamba hebu tuifanye Dodoma kuwa *dry port*. Tuimarishe reli kutoka Dar es salaam mpaka Dodoma, mtu wa Iringa na wa Arusha hawezi tena kwenda kufuata mafuta Dar es salaam, atakuja Dodoma kwa kuwa ni karibu. Kwa hiyo, nashauri hilo *in future* hebu tazameni, muone ni namna gani mnaweza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye jambo la pili kuhusu Makao Makuu Dodoma, tangu tamko la Chama cha *TANU,* nilipokuwa nina miaka miwili tu toka nimezaliwa, hakuna Sheria inayo-*govern* kuwa Dodoma ndiyo Mji Mkuu wa nchi hii. Akaja Rais mwingine wa ajabu ajabu hivi, akasema Makao Makuu tuyapeleke Bukene, hakuna Sheria inayomzuia au akaamua yaende Serengeti au Kibaigwa, anaweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilete Muswada ili Dodoma itambulike Kisheria kuwa ndiyo Makao Makuu ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lijalo nitaleta hoja binafsi hapa kuhusu jambo hili la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi itambulike Kisheria. *CDA* imefanya kazi nzuri sana, lakini pia ina upungufu wake. *CDA* inasukuma watu nje ya Dodoma, lakini hawalipwi fidia. Sidhani kama jambo hili linafanyika Dar es Salaam, Arusha au Mwanza, *why* Dodoma peke yake? Tukiwa- *push* watu nje ya Dodoma, nje ya Mjini, basi tuwalipe fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa kidogo atanisamehe sana Mheshimiwa Lukuvi, yeye ndiye Mwenyekiti wa *CDA* na yeye ni Waziri. Ni utamaduni wa zamani sana, tubalidilishe hicho kitu ili *CDA* iwe *independent.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama ni *fair* kwamba Waziri wa Nchi ndiyo anakuwa Mwenyekiti wa Bodi ya *CDA* na Makatibu Wakuu wa Wizara ndiyo wanakuwa Wajumbe wa Bodi, twende kama zilivyo taasisi zingine. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye kilimo; Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Kongwa na Gairo kwa upande mmoja, wakulima wanaolima kule Wilaya ya Kiteto wanapata matatizo sana. Alikuja Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni, akasema wananchi waishi bila kujali kuwa anakwenda wapi ili mradi anafuata Sheria, kama anakwenda kulima Kiteto alime, lakini afuate taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu sasa limekuwa ni tatizo. Kwa mfano, ukija katika Wilaya ya Kongwa, wananchi wa Mkoka, Ngomayi, Njoge, Kibaigwa, Mtanana; ukienda Wilaya ya Chemba; Mrijo, Kiteto, Jangalo na Itolwa wakienda kulima kule wanafukuzwa. Nina barua hapa iliandikwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kwa ruhusa yako naomba kuinukuu.

"Kibali cha kuchangisha fedha za kuendesha operesheni ya kuondoa wavamizi katika Hifadhi ya Emborolei Murtangos shilingi milioni 150".

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niikabidhi barua hii. Mkurugenzi wa Halmashauri wakati huo, aliyeisaini hii barua anaitwa Jane Mutagurwa, aliwataka wananchi wa vijiji takribani 12 wachange fedha ili kuwaondoa watu wanaodaiwa kuvamia mapori haya, inadaiwa ni Hifadhi, Hifadhi gani watu wanachunga ng'ombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni Hifadhi, basi ibaki ni Hifadhi ya wanyama, lakini unapokwenda kuwaondoa watu wale wa Kondoa, Chemba na Kongwa ili watu wakachunge n'gombe, *it's not fair*. Nadhani upo umuhimu wa Serikali sasa kuliangalia jambo hili limezungumzwa muda mrefu sana. Tatizo la mipaka hii kwa nini tugombane? Nadhani jambo la msingi ni sisi wote kuishi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, namkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu ile ahadi yake ya kutupatia 3.8 bilioni kwa ajili ya mradi wa maji wa Ntomoko. Tunasubiri kwa hamu sana, tunasubiri pia utekelezaji wa miradi ya visima vya maji katika baadhi ya vijiji, vile vya *World Bank*. Tutafarijika sana ikikamilika na katika maeneo ya utawala, tunashukuru tumepata Wilaya ya Chemba. Tunaomba sasa mtuletee Mkurugenzi ili tusimame kwa miguu yetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima ya pekee sana, najua watu hawapendi kushukuru kwa mujibu wa Kanuni, lakini Waarabu wanasema *Jitihada Wajadala,* namshukuru sana Naibu Waziri wa Kilimo Shemeji yangu Adam Malima kwa kazi nzuri aliyofanya ya kutuletea chakula, kwani tulikuwa tumeathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya naunga mkono hoja*. (Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa!

Waheshimiwa Wabunge, Miongozo ningeomba sana tuipunguze kadri inavyowezekana, kwa sababu inapunguza muda wenu wa kuchangia. Kuna jambo la uwiano hapa, itafika mwisho wa siku itaonekana kwamba watu wa Chama fulani wamechangia wengi kuliko wengine kwa sababu ya masuala ya miongozo. Kwa hiyo, ningewaomba sana kama ni jambo ambalo siyo la lazima sana tusisimame. Mheshimiwa endelea na huo Mwongozo.

**MHE. PAULINE P.GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 68(7), naomba Mwongozo wako kuhusu...

**NAIBU SPIKA:** Isome.

**MHE. PAULINE P.GEKUL:** Kanuni ya 68(7) inasema: “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote

ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo." Lakini naomba Mwongozo kuhusu Kanuni ya 64 na vifungu vyake vyote ambavyo vimekuwa vikivunjwa kwa muda mrefu humu ndani na Kiti kimekuwa kiko kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji aliyepita ametoa lugha ya matusi kwa Wabunge wote, Mheshimiwa Machali akasema kuwa Wabunge wanaitwa mbwa, lakini kama halitoshi amezungumzia kuhusu Mbunge Machali kukosa umakini. Nimeona kuwa kinachokosewa hapa ni kifungu hiki cha 64 na Kiti kimekuwa kikipendelea waziwazi. Bila kuwaambia hawa Wabunge wafute kauli, humu ndani hakutatawalika na wengine wakiamua kutukana hatutafika. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu gani Wabunge kukaa na hizi Kanuni, wakati Kiti kinaangalia Kanuni hii inavunjwa na Kiti kiko kimya? Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hao unaodai wanatoa matamshi yasiyokuwa mazuri, wametumia utaratibu wa Mwongozo na utaratibu wangu ni kwamba, Miongozo yote nitaitoa baadaye kusudi nisitumie muda wa Wabunge kuchangia kwa sababu mna haki ya kuchangia na mmelalamika sana kwamba mngependa kupata haki ya kuchangia. Hizi dakika zimegawanywa na nafasi zenu ziko hapa, mnatakiwa watu 18 mpate nafasi asubuhi hii, hapa tunakula muda wa Mbunge mwingine hapa.

Kwa hiyo, wale wote ambao mliotumia nafasi ya Miongozo, nitaitolea kwa wakati wake. Naomba sana tabia ya kufikiri kuwa Kiti kiko hapa kwa kupendelea kinampendelea nani? *Unless* Kiti kinamtuma mtu atukane au mtu akashifu mna uhakika huo? Naomba Mheshimiwa Rashid Abdallah endelea, miongozo nitaitoa baadaye. Atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa na Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kusimama hapa, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kuwa Waziri Mkuu ndiyo Mtendaji Mkuu wa Serikali na ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli zote za Serikali. Nimepitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kutafuta mikakati ya kupambana na wizi na matumizi mabaya ya fedha za Serikali, lakini sikuona kitu chochote, inaonekana labda hii hali yeye inamridhisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri zetu kuna wizi na matumizi mabaya ya fedha za Serikali, uniruhusu nitaje kidogo baadhi ya maeneo ili ionekane ni jinsi gani fedha za Serikali zinatumika vibaya. Kuna zaidi ya shilingi milioni 109, fedha hizi zimetumika kinyume na mipango kazi. Kuna zaidi ya milioni 23, katika fedha hizi kumetokea ubadhirifu na sehemu ambayo imetokea ubadhirifu ni Halmashauri ya Muheza. Kuna zaidi ya milioni 113, Songea zimetumika nje ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha zaidi bilioni 1.6, zimetumika nje ya bajeti bila kupata kibali cha Hazina. Kuna zaidi ya milioni 82, zimelipa wafanyakazi hewa na kuna zaidi ya shilingi milioni 275 ni mishahara ambayo haikulipwa, lakini haijareshwa. Kuna baadhi ya watendaji wa Serikali za Mitaa wanatumia vitabu vyao wenyewe kwa kulipa kodi ya Serikali. Lakini pia kuna zaidi ya shilingi bilioni 16, zimetumika kununua mafuta kwenye magari mabovu ambayo kwa sasa hayatumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hofu kuwa sasa tunapitisha bajeti na tunapopitisha bajeti kuna watu wanatusikiliza ipite tu waende kuivamia. Ukiangalia bajeti

ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imepangiwa trilioni 4.1. 58% ni mishahara na 23% ni matumizi mengineyo, nitakamata hapa kwenye matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nilipitia zile *Vote* moja baada ya nyingine katika Mikoa yote inayohusu vyakula na viburudisho na nime-*collect* zaidi ya bilioni 1.3 kwa matumizi ya vyakula na viburudisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule Zanzibar tunapewa 1.2 bilioni kwa maendeleo ya Majimbo yote 50, lakini sehemu ya Tawala za Mikoa tuna zaidi ya 1.3 bilioni za vyakula tu na viburudisho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kidogo tu katika uchangiaji wako, sina nia ya kuingilia, lakini ningeshauri kuwa endapo kama unagusa mambo ambayo yako katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo imewekwa juzi mezani, na bado haijaletwa kwenye Kamati ambayo wewe ni Mjumbe, itakuwa si sawasawa. Endelea kuchangia.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kasma hizi kuna haja ya kuzifanyia marekebisho, hakuna haja ya kuweka vyakula na vinywaji katika maofisi mbalimbali, haya ni matumizi mabaya ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii inaonesha kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshindwa kusimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Serikali na kwa sababu hii sitaunga mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu aeleze ni kwa vipi atadhibiti matumizi mabaya ya Serikali na ni vipi atadhibiti makusanyo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa, Mkuu wa Mkoa ameshindwa kupata ushuru wa

viwanda hadi hivi leo, sababu nilijua kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ana nia nzuri tu, lakini labda viwanda vile vimetawaliwa na watu ambao hawadaiki, kwa hiyo, ameshindwa kabisa na hizo ofisi hawasimamiii kabisa ushuru huo, Serikali itakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu anipe mikakati yake ya kupambana na matumizi mabaya ya fedha za Serikali ili nchi hii huko tunakokwenda twende salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, suala la mwisho, ni kuhusiana na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, katika ukurasa wa 11 *paragraph* ya pili na ukurasa wa 13, katika hotuba yake, alikerwa na kuwepo kwa idadi kubwa ya Wazanzibari kushiriki katika Katiba mpya kwa ajili ya mambo yasiyokuwa ya Muungano, kinyume na kwamba na wao hawapati fursa hiyo huko Zanzibar. Akatishia kuwa kama hakuna Sheria itakayoletwa hapa na kuwaondoa Wazanzibari hawa katika Muswada wa kupitisha Katiba mpya basi watagomea zoezi zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limeundwa chini ya Ibara ya 92 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ina Kanuni zake katika kuendesha Bunge hili. Tume ya Marekebisho ya Katiba iko chini ya Sheria namba nane (8) ya mwaka 2011 ambayo ilijadiliwa ndani ya Bunge na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alikuwepo na kama hakuwepo, basi alitumia maamuzi yake mwenyewe, haki hiyo alikuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyojua, kwa mujibu wa Katiba, Serikali ya Bara hakuna, kwamba wakae Wazanzibari wasijadili mambo ambayo siyo ya Muungano, wakae wa Bara wajadili mambo ya Muungano, ninavyojua kuna Serikali

mbili tu ambazo tutaendelea kujadili mambo ambayo si ya Muungano na yale mambo ya Muungano ndani ya Bunge hili na nje ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limenikera sana, hii ni ile mbegu ya ubaguzi. Ukianza kumbagua mwenzako, utaendelea kubagua Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Nasema kuwa, Tanzania ina Katiba yake na lazima tuifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wazanzibar wameteuliwa kwa mujibu wa Sheria hii namba nane (8) na imepitishwa ndani ya Bunge, sasa leo wanasema waondolewe, hawa watu walikuwa wapi katika Bunge hili? Nadhani ni vizuri kuweka hali ya utulivu na mshikamano baina ya Watanzania. Wao walipewa muda wa kuchangia maoni yao...

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rashidi. Sasa ni *Miss* Bunge, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nizungumze kidogo kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote niseme, hotuba ya Waziri Mkuu ni ndefu na urefu wake unatokana na sababu kwamba, inagusa karibu Wizara zote. Pia nimpongeze tu kwa kuwa anajitahidi sana, imejikita katika mambo mengi sana na inahitaji kichwa chenye busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, naelekea moja kwa moja Mwanza. Mwanza kama mnavyoisikia ni Mji wa Pili kwa ukubwa na ni Mji pia wa pili kuwa na watu wengi zaidi ukitoa Dar es Salaam, inahitaji huduma hasa na inatakiwa kuangaliwa kwa mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza ni eneo la Viwanda, kuna viwanda vingi Mwanza lakini viwanda hivyo ninavyovisema vyote vipo hoi bin taabani, vinahitaji aidha kufufuliwa na vingine kujengwa upya kabisa. Tungekuwa na viwanda vilivyo hai, suala la ajira lisingekuwa linatupa tatizo hasa kwa vijana wetu. Viwanda ndiyo hutoa ajira nyingi, lakini karibu viwanda vingi tu havifanyi kazi kabisa vikiwepo vya Mwanza. Naiomba Wizara, kama Waziri yupo hapa ajaribu kuja Mwanza, afanye ziara Mwanza, kwa haya ninayoyasema, mkitufufulia viwanda, suala la ajira litapungua maana vinatoa ajira nyingi sana kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza mwisho tunakuwa na matatizo ya fujo kwa vijana mitaani, yote hiyo ni kwa sababu wanakosa ajira, wafanye nini, waende wapi? Mngewaweka mle wakawajibika, fujo zote zitakwisha, sisi ni watu watulivu lakini ni kwa sababu ya kukosa ajira mwisho vijana wanaingia katika matatizo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni maji. Mimi nimetembelea kituo cha Ihelele kule Misungwi, kuna pampu ambazo zinasubiri huduma ya Serikali. Msione tumezungukwa na Ziwa mkadhani maji yapo tu, jamani Mwanza hatuna maji; mabomba yamechakaa ni ya miaka ya mkoloni. Nadhani sasa tunahitaji mabomba mapya ili tuyatumie maji yanayotuzunguka Mwanza. Ziwa lipo pale lakini maji yanahitaji kuvutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamevutwa maji yakapelekwa Shinyanga mpaka Kahama, sisi tunayaangalia yanapita tu, hatutaki fujo. Narudia, Mwanza siyo watu walioumbwa kwa fujo, tukisema tutoboe lile pipa mtasema nini? Tunaomba Waziri wa Maji, afanye ziara Mwanza aone tunavyohitaji maji ya bomba, siyo maji ya kubeba vichwani,

akina mama wanatengeneza nywele zao mtubebeshe maji ya kitu gani! Tunahitaji maji ya bomba yafike majumbani mwetu. Msituhukumu kwa Ziwa, Mwenyezi Mungu, katupa Ziwa lakini tunataka basi Serikali itupe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, naomba niongelee kwa ufupi tu kuhusu Reli ya Kati. Mimi bila kuzungumzia Reli ya Kati watu hawatanielewa. Nashukuru, kwanza, Wizara walau tumepiga kelele tumeona treni ya abiria, lakini tunataka iongeze siku za kuja Mwanza, kwa sababu gharama hiyo ndiyo tunaitegemea inaweza ikawa ya nafuu kwetu. Tunataka pia treni inayobeba mizigo, barabara hizi mnazotengeneza bila ya kuwa na treni ya kubeba mizigo, hiyo lami itabomoka siku mbili, tatu. Ukiwa barabarani unakumbana na malori mengi ya mizigo, tunaomba kama kweli, kuna Msemaji mmoja humu amesema kwamba, kama kuna kuthubutu kukopa tukope tupate hivyo vichwa vya treni viweze kubeba treni za mizigo, pekee ndiyo unafuu wa nchi hii wa kunusuru barabara zetu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea hili mara kwa mara lakini sijui uzito upo wapi kufanya maandalizi ya kukopa, ni nani anayeishi bila kukopa, hata humu ndani tumekopa; sasa kama ndiyo hali halisi hiyo Serikali inaogopa nini kukopa? Ukikopa mkopo kuurejesha ni lazima, lakini hebu labda kuna mahala pazito Ofisi ya Hazina, lakini ukweli ni kwamba, tunahitaji treni ya kubeba mizigo ili kunusuru barabara zetu mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naongelea suala la UKIMWI. Hakuna hata mmoja humu katika familia zetu ambaye hajaguswa, lakini tatizo la Serikali kumbe ni asilimia karibu 95 tunategemea fedha kutoka nje ili tuwe na kinga halisi au tuweze kupata dawa zenye kutibu magonjwa nyemelezi. Asilimia 95 mpaka 98 tunategemea wafadhili, tunakabidhi uhai wetu kwa wafadhili; hivi ni halali jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tufike mahali sasa tubadilike, maana hata maisha yetu nayo tunayakabidhi kwa

wafadhili; hapana hata kidogo! Tubadilike, tuutafute mfuko wa ufadhili kwa hela zetu za ndani kuanzia sasa. Tena ni mambo ya ajabu, yaliyo mengi mambo yenye huduma ndiyo tunawakabidhi wafadhili, hata maji yapo kwa wafadhili! Sasa katika hali hii hebu tuone mambo ya huduma yanachangiwa kwa fedha zetu za ndani ikiwemo UKIMWI, vinginevyo, wakijitoa wafadhili hao, kwanza, wameshaanza kujitoa! Tukibaki hivi hivi si ndiyo tunaanza haya ya UKIMWI? Naomba katika hili itakapofika wakati, mkakati ukitoka wa kupata fedha, fedha za ndani zitumike tuweze kupata mfuko wa kupambana na suala la UKIMWI na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, najua kengele ya pili inagonga sasa hivi, ahsanteni kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kama nilivyosema sasa anafuata Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi atafuatia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kusema kwamba, humu ndani tunaweza kuwa na ufahari wa maneno mengi ya kutuponda na kutudhalilisha lakini ukweli unabaki pale pale kwamba, maisha ya Mtanzania yanaendelea kuwa magumu kwa sababu ya Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kulalamika jinsi gani Kanuni ambavyo zinavunjwa lakini bado hakuna maamuzi yanayotolewa. Kuna kauli ilitolewa na mchangiaji mmoja hapa akituita mbwa na kusema mambwa humu ndani lakini hakuna kinachofanyika. Tunaomba haki itendeke, la sivyo, huku ndani hatutaelewana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwakumbusha Watanzania na Wabunge humu ndani kwamba, wajibu wa Kambi ya Upinzani Bungeni ni kuikosoa Serikali iliyopo madarakani, hatuwezi wote kusema ndiyo mzee; haiwezekani, ndiyo wajibu wetu na tunapaswa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niongelee suala la matokeo ya upimaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, umegusa jambo ambalo nimekwishalitolea *ruling* kwamba, nitatoa mwongozo baadaye, kuendelea kuliongelea ni kuendelea kudhalilisha tu Kiti. Nilifanya hivyo kulinda muda ili wewe na wenzako mpate nafasi ya kuzungumza. Sasa kama hilo ndiyo kosa langu, basi, lakini endelea kuchangia, siyo vizuri kuendelea kubishana tu kila wakati kwa mambo ambayo ni kupoteza muda. Mheshimiwa endelea.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu ulindwe. Matokeo ya upimaji kwa Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alieleza kwamba, kwa Halmashauri zilizofanya vibaya zitakatwa asilimia 25 ya fedha za Miradi ya Maendeleo, lakini huku ni Serikali kukwepa kutimiza wajibu wa kuwaadhibu watendaji waliosababisha suala hili kwa Serikali. Maana hatuwezi kuwaadhibu kupeleka asilimia 25 ambayo inaenda kuwaathiri Wananchi na waliosababisha suala hili wanaachwa wakiendelea kuwa katika Halmashauri hizo. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali itimize wajibu wake wa kuwawajibisha watendaji wote ambao wamesababisha suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema kwamba, suala la Madiwani nchini ni nafasi ya kisiasa ambayo imesahaulika kabisa. Mara nyingi tumepigia kelele suala la ongezeko la posho za Madiwani na tukiitaka Serikali isiwe posho iwe ni mishahara. Wabunge sisi ni mashahidi, kiasi gani Madiwani wanavyofanya kazi kubwa kuliko hata sisi Wabunge. Madiwani muda wote wapo na Wananchi kule, lakini leo wamesahaulika. Serikali ituambie kuhusu suala la Madiwani kulipwa mishahara na siyo posho. Madiwani hawahawa wananyimwa hata safari za kwenda kujifunza mahali pengine katika Halmashauri zingine na hili tamko lililotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Madiwani siku hizi hawapati nafasi ya kwenda kujifunza katika Halmashauri zilizofanya vibaya, mpaka kibali kipatikane kwa Waziri Mkuu.

Kwa nini tunarudi kwenye urasimu wa namna hiyo? Tunataka Ofisi ya Waziri Mkuu iliangalie suala hili; Madiwnai wapate mafunzo, Madiwani wapate mikopo, kuna Halmashauri zingine Madiwani wamepata mikopo na Halmashauri zingine hawajapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mchakato wa utungaji wa sheria ndogo. Mchakato huu umekuwa na urasimu mkubwa sana katika Halmashauri zetu. Halmashauri wanamaliza kazi yao ya mchakato wa utungaji wa sheria ndogo lakini inakuja kukwama kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, inakuwa haipitishwi kwa wakati. Kunakuwa na sheria ndogo nyingi za Halmashauri zipo katika Ofisi ya Waziri Mkuu hazijapitishwa na zina muda mrefu. Kwa nini kama tunasema dhana ya ugatuaji wa madaraka isirudishwe mamlaka hayo kwa mikoa? Tunaitaka Serikali iliangalie suala hili irudishe mamlaka hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso, nakushukuru sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Kulikoyela Kahigi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia machache lakini mengine nitayaandika ili niwape wayajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitachangia kuhusu matatizo ya wafugaji huko Bukombe na mahali kwingineko. Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Kamata, amechangia, ningependa tu kusisitiza kwamba, tatizo hili limekuwa ni sugu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni mimi nilishauliza swali na kupendekeza kwa Waziri aliyekuwepo kwamba, iundwe Tume ili matatizo haya ya wafugaji na migogoro baina ya wafugaji na wakulima yatafutiwe ufumbuzi. Mheshimiwa Waziri akatoa jibu jepesi akasema kwamba, Serikali inashughulikia, lakini tatizo bado liko pale pale. Mifugo ya hawa wafugaji inaendelea kupigwa risasi, wakati mwingine mifugo inasukumizwa kwenye hifadhi na

hawa hawa Askari, makusudi kabisa inapigwa risasi na wakati mwingine wanadaiwa pesa nyingi sana. Naomba Serikali iliangalie suala hili kwa sababu nchi hii ni yetu sisi sote, ni nchi pia ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naenda haraka haraka. Kumekuwa na ukiukwaji wa makusudi, kumekuwa na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu. Nilimwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu barua kuhusu Wananchi wa Nyamagana, Wananchi wa huko Magu na Kaniha, Wilaya ya Biharamulo, ambao walikuwa wanasumbuliwa, walichomewa nyumba zao, walifukuzwa kwenye makazi yao kwenye maeneo ya vijiji ambavyo vimesajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kaniha ni kwetu, angalia umri wangu, naomba Serikali iliangalie suala hili, Wananchi wa maeneo hayo wamechoka na ninaomba ichukue hatua za kuwapatia maneno ya faraja na kuwafidia mifugo ambayo imepotea kwa sababu katika kuwahangaisha wengine walipoteza mifugo yao. Naomba suala hilo pia lishughulikiwe kwa sababu ni la aibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la tatu ambalo ningependa kulizungumzia ni la pensheni kwa wazee. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa kauli ya faraja hapa kwa wazee, sasa muda mrefu umepita, naomba katika majibu yake atueleze hapa Bungeni huu mpango wa pensheni kwa wazee umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Bodi za Maji ambazo zinapaswa kufanya kazi katika Miji Midogo kama Ushirombo. Bodi hizi huwa zinateuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpaka sasa toka mwaka 2010 hakuna Bodi za Maji katika Miji hii midogo; naomba atoe kauli kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwapatia Wananchi wa Ushirombo, alipotembelea huko, hata mimi nilikuwepo na nilisikia hiyo ahadi kwamba angewapatia shilingi bilioni moja ili kupanua mtandao wa maji katika Mji

Mdogo wa Ushirombo. Naomba atupatie kauli kwa sababu Wananchi wa Ushirombo wanauliza kuhusu suala hili kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu umeme Bukombe, tuliahidiwa kwamba, umeme ungeanza kutekelezwa mwaka jana Oktoba lakini mpaka sasa Wananchi wa Bukombe hawaoni chochote kinachoendelea. Tunaomba Serikali itoe kauli kuhusu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu matokeo ya Kidato cha Nne ya mwaka jana; mimi ni Mwalimu, najua kwamba mfumo wetu wa elimu una matatizo mengi, lakini swali ambalo Watanzania wanajiuliza; kwa nini Wizara ya Elimu haikufanyia kazi yale mapendekezo yaliyotolewa na Tume iliyoundwa mwaka 2010? *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi. Mheshimiwa Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Kapteni John Chiligati.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wa Pwani wanasema; "Mchelea mwana kulia hulia yeye." Haya nitakayoyazungumza nina nia njema kabisa ya kukisaidia Chama changu na kuisaidia Serikali yangu ili iweze kufanya vizuri katika maeneo ambayo mimi natokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ilianzisha dhana ya KILIMO KWANZA na ilielekeza Wizara zote zijikite kuhakikisha kwamba, KILIMO KWANZA kinafanikiwa. Kitu cha kushangaza na kwa masikitiko makubwa, jambo hili halijaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa hasa kwa maeneo yetu ya Kusini. Sisi watu wa Kusini na Mikoa ya Pwani, zao letu kubwa la biashara ni korosho, lakini kwa miaka miwili mfululizo zao hili la korosho limedhalilishwa kwa kiasi kikubwa sana. Haya ni masikitiko makubwa sana kwa Wakulima wa korosho, miaka miwili mfululizo. Maana tulitegemea kwamba, labda mwaka wa kwanza kulikuwa na makosa fulani ya kiutendaji yamefanyika

Serikali itajifunza, lakini miaka miwili mfululizo jambo hilo limekuwa likitokea. Wananchi wamezalisha korosho kwa wingi, matokeo yake miaka miwili mfululizo korosho hizo zimenunuliwa kwa kusuasua na wakulima wengine mpaka leo hii hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza, msimu huu korosho vilevile zimeshindwa kununuliwa, wananchi wameuza kwa Kangomba, kilo moja shilingi mia tano badala ya shilingi 1,200. Je, dhana hii ya KILIMO KWANZA kweli itaweza kufanikiwa kwa mtindo huu? *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa zaidi, wakati korosho hizi zinataka kununuliwa, kulikuwa na majadiliano kati ya wanunuzi, benki pamoja na wawakilishi wa wakulima. Cha kushangaza, wanunuzi waliweka masharti kwamba, watanunua korosho zile zikiwa Mtwara; yaani watu wa Namtumbo, wasafirishe korosho zao zipelekwe Mtwara na watu wa Tunduru wapeleke Mtwara. Sasa hofu yetu wanasema kwamba, Tunduru Namtumbo ni mbali, Masasi ni mbali. Sasa umbali huu kutokea wapi; kutokea *Mbamba Bay* au kutokea Bombay huko India ambako zinapelekwa korosho hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hofu yetu, kesho na keshokutwa hawa wanunuzi wanaweza wakaleta masharti tena mengine kwamba, korosho za Tanzania tutanunulia India; nina hofu Serikali inaweza ikakubali. Kwa sababu kama wamekubali sharti hili dogo ilhali Serikali yenyewe imeshindwa kujipanga kuhakikisha kwamba, inatafuta soko zuri na la kudumu la korosho; tuna masikitiko makubwa sana juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Serikali imeshindwa kujipanga, kuegemea kwa wakulima na kuamua kuegemea kwa wafanyakazi, hata ile dhana ya KILIMO KWANZA, sasa tuna mashaka nayo. Tuna hofu kwamba, dhana sasa inabadilika kutoka kwenye KILIMO KWANZA na kuwa BIASHARA KWANZA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili limedhihirishwa juzi baada ya kuona kwamba, Wananchi wengi wamevuna mpunga na upo kwenye maghala, Serikali kwa makusudi ikaagiza mchele ku-*suppress* bei ya wakulima. Jambo hili nalo ni masikitiko makubwa sana, kwa sababu vitu vingi vya madukani vinapanda bei, lakini hatujawahi kuona Serikali inaagiza vitu vingi ili ku-*supress* bei ya vitu vya madukani. Leo mchele umepanda bei, ambayo ni neema kwa mkulima, Serikali inaagiza mchele mwingine kutoka nje ya nchi ili kumfanya mkulima apate bei ndogo ya mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee suala la Kituo cha Afya Nalasi. Moja ya ahadi za Mheshimiwa Rais, wakati anaongea na Wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini, ilikuwa ni kujenga Kituo cha Afya cha Kata ya Nalasi. Ni namna tu ya kumkumbusha kwamba, kuna haja ya kutenga fedha maalum kwa ajili ya ujenzi wa Kituo hiki. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba, katika bajeti hii ya fedha, Wananchi wa Nalasi, wanatarajia wapate fedha ili Kituo kile kianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mawasiliano ya mnara katika Kijiji cha Nalasi; hii vilevile ni moja ya ahadi za Mheshimiwa Rais, kwamba, Wananchi wale wapewe mawasiliano ya haraka ili waweze kuwasiliana na Watanzania wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana katika Bunge hili Tukufu, tulikubaliana kwamba, kutatengwa fedha kwa ajili ya *pension* ya wazee wote wa Tanzania. Katika Hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijaona mahali ambapo linaelezwa hilo. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika mambo ambayo tutafanya makosa katika Serikali yetu, ni pamoja na kuwasahau wazee ambao ndiyo walioilea nchi hii mpaka sasa hivi sisi tunajivunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaombeni sana, fanyeni chochote mtakachoweza kufanya kabla bajeti hatujaipitisha, tuhakikishe kwamba, hawa wazee wetu wa Tanzania wanalipwa *pension.* Hakuna ugumu wenzetu wa

Msumbiji wamefanya hivyo, wenzetu wa Uganda wamefanya hivyo, sisi tunashindwaje? Nasikia mpaka Zanzibar, nao wanafanya hivyo. Nawaombeni sana tuhakikishe kwamba, *pension* ya wazee ambayo mwaka jana tulikubaliana tutaanza kulipa mwaka huu, fedha hizo zitengwe bila kukosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo vilevile nataka nilizungumzie ni juu ya Daraja la Mto Maholela pale Mbesa. Niwahakikishie tu Wananchi wa Mbesa kwamba, mwaka huu, Serikali yenu Tukufu ya Chama cha Mapinduzi, imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha michoro ya daraja hilo ili tuanze kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga. Haya ndiyo maelezo ambayo tumepewa na Wizara ya Ujenzi na bahati nzuri kasma hiyo nimeiona mwenyewe, kwa hiyo, kikubwa tuendelee kuiombea Serikali hii, iweze kufanya vizuri siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo niliyotaka kuzungumza ni hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kapteni Chiligati.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza, nataka nianze kuchangia suala la mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naishukuru na kuipongeza Tume ya Katiba, inayoongozwa na Jaji Warioba. Mpaka sasa wanafanya kazi yao vizuri, kwa uaminifu na kwa uadilifu, kwa hiyo, tunawatia moyo. Wale ambao wanawabeza, nadhani wana ajenda ya siri tu; ni Tume ambayo inafanya kazi vizuri mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonishangaza ni kusikia kwamba, kuna baadhi ya vyama ambavyo ama wamejitoa au wanakusudia kujitoa kwenye huu mchakato.

Nashangaa, kwa sababu tumekuwa pamoja, mchakato tulianza pamoja, Tume tumeunda pamoja, ndani ya Tume kila chama kilipeleka wawakilishi mle, safari karibu inakwisha; maana wakishamaliza haya Mabaraza ya Wilaya, itabaki sasa Bunge la Katiba na Kura ya Maoni. Karibu safari inakwisha, sasa katikati ya safari wenzetu wanasema wanajiondoa. Sababu kwa nini wanataka kujiondoa, wanasema mchakato huu sasa umetekwa nyara na Chama cha Mapinduzi; ni sababu ambayo haina mashiko, kwa sababu, haya Mabaraza ya Wilaya yanatoa Wajumbe wanne kutoka katika kila Kata. Wanasema *WDC,* Kamati ya Maendeleo ya Kata, Tume imekosea kuipa madaraka haya. Kamati ya Maendeleo ya Kata, ndilo Bunge la Kata. Watu wanne katika kila Kata waende kwenye Wilaya, unawapataje bila kutumia Bunge la Kata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama sisi humu ndani ambavyo huwa Bunge hili tunachagua wawakilishi kwenda kwenye Bunge la Afrika Mashariki au tunachagua Wabunge wanakwenda katika Bunge la Afrika. Hii ndiyo *WDC* ya Kata, kama ingekuwa ni Kata hii ndio *WDC* yenyewe. Kwa hiyo, sababu kwamba, Kata, *WDC* kuchagua Wajumbe kwenda kwenye Baraza la Wilaya ndilo kosa la Tume na ndiyo sababu ya kujiondoa, nasema haina mashiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiondoa hayo Mabaraza ya Kata, yako na Mabaraza mengine ya Katiba. Yako Mabaraza mengine ambayo vilevile nayo yatakaa, yatazungumza Rasimu ya Katiba na kupeleka maoni. Yako Mabaraza ya Makundi Maalum; Wafugaji watakuwa na Baraza lao na wao watapeleka. Watu wenye Ulemavu watakuwa na Baraza lao nao watapeleka, huko nako *WDC* inachagua. Wanajitoa kwa sababu gani? Je, wanapojitoa na wanachama wao katika makundi hayo vilevile hawatashiriki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza vilevile yatafanywa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs),* nao watakuwa na Mabaraza yao ya Katiba nao watapeleka.

Vyama vya Siasa, nasi tutakuwa na Mabaraza yetu, tutatoa maoni na tutayapeleka. Sasa wanajitoa kwa lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wanatishia kwamba Tume wasiporekebisha hili; Tume wala msitishike, mnafanya kazi vizuri, endeleeni. Suala la kujitoa, wanataka kufanya fujo tu na Wananchi wajue kabisa, mtu anayejitoa saa hizi huyo hatutakii mema, ni chanzo cha fujo na wamkatae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema wataandamana nchi nzima; wanaandamana kwa lipi? Mabaraza kila mahali yamemwagwa, ninyi mnaandamana kwa lipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili suala la maandamano, hebu tufike mahali tuliwekee utaratibu; hii ndiyo nchi peke yake duniani mtu yeyote, siku yoyote, saa yoyote, anatangaza maandamano, tutafanya kazi saa ngapi? Mheshimiwa Waziri Mkuu, lete Muswada hapa tuweke utaratibu wa maandamano; kuandamana kweli ni haki, lakini kuwe na utaratibu. Siyo mtu yeyote, saa yoyote, mahali popote, anaitisha maandamano, tutafanya kazi saa ngapi? Itakuwa ni nchi ya maandamano hii. Lete Muswada, tuweke utaratibu tuseme maandamano tufanye siku ambayo siyo ya kazi; siku ya kazi tufanye kazi, siku ambayo hakuna kazi ndiyo maandamano yafanyike. Tuweke Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine nyingi zina Sheria, ambayo inaweka utaratibu wa maandamano na siyo tu siku na mahali pa kuandamana. Zile sehemu za uzalishaji, hapana maandamano pita huko, sehemu watu wana biashara zao, hapana maandamano; wawekewe na utaratibu siku ya kuandamana na mahali pa kwenda kuandamana; nchi nyingine zinafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende suala la elimu. Juzi msemaji wa upande wa pili, alikejeli sana habari ya elimu ya sekondari, akaiita Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete ni janga la Elimu, kana kwamba, Serikali yake haijatoa

mchango wowote katika nchi hii kwenye suala la elimu. Nasema hili nalo siyo sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni upi? Wakati Mheshimiwa Kikwete, anashika madaraka, tulikuwa na sekondari 1,745 nchi nzima. Hapo ndipo alipotukuta Mheshimiwa Kikwete na Serikali yake.

Wakati huo, wanafunzi katika sekondari walikuwa 401,596 halafu wanaokwenda *Form I,* Darasa la VII, chini ya nusu ndiyo walikuwa wanapata nafasi ya kwenda Sekondari, zilikuwa hazipo. Tukakaa tukasema ni kwa nini watoto wetu wanafaulu halafu hawaendi sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake cha miaka sita hii, Mheshimiwa Kikwete, sekondari chini yake zimeongezeka kutoka 1,700, mpaka sasa tuna sekondari 4,102, ambazo sasa zinachukua watoto zaidi ya milioni moja na nusu ndani ya sekondari. Kuwapeleka watoto milioni moja na nusu toka laki nne, hilo ni janga? Jamani, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Kikwete, karibu takriban katika kila Wilaya, kila mtoto anayefaulu Darasa la Saba, anakwenda sekondari. Ni Rais, ambaye akitoka madarakani, atatoka na sifa kwamba, aliwezesha kila mtoto anayemaliza Darasa la Saba anakwenda sekondari. Hilo ni janga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko changamoto; ni kweli tumepanua sekondari kutoka 1,700 mpaka 4,000 kwa kipindi kifupi sana. Ziko changamoto; hizi sekondari nyingi ni changa, tuzilee. Sisi Watanzania kwa pamoja tufanye kazi ya kuzilea ili zikue. Tuzilee kwa kuziongezea walimu, ndiyo kazi inayofanywa na Serikali sasa hivi madarasa, maabara na kadhalika, zipo tuziimarishe. Zipo ametuachia sekondari zaidi ya 4,000 na kila mtoto anakwenda Sekondari. Kwa hiyo, nasema kwamba, wale wanaombeza Mheshimiwa Kikwete, hawamtendei haki. Huyu ni Rais, ambaye amewezesha kila

mtoto kwenda sekondari, sasa kazi yetu sisi kuziimarisha hizo sekondari zitoe elimu bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi Jimboni kwangu Manyoni, nadhani bado nina dakika chache. Ukurasa wa 47 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia suala la upungufu wa chakula, hali ya njaa katika Wilaya 47. Wilaya ya Manyoni na Jimbo langu la Manyoni Mashariki, ni moja katika hayo maeneo. Niseme tu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika jambo ambalo linanisumbua moyo wangu mimi nakosa raha, ni kila mwaka kuja kupanga foleni ofisini kwako, kuomba chakula cha njaa. Ni jambo ambalo linanisumbua, ni jambo ambalo ni fedheha, lakini chanzo chake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Manyoni, nusu iko katika Bonde la Ufa, hili ni eneo kame; si kwamba, watu ni wavivu, watu wanalima, lakini mazao yote yanaungua na jua, shida yetu sisi ni maji.

Tunazo *scheme* za umwagiliaji katika eneo la Bonde la Ufa karibu tano, miundombinu ipo, lakini maji ya kumwagilia hayapo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili kuondoa tatizo la njaa katika Wilaya ya Manyoni na hasa Bonde la Ufa, tunachoomba ni bwawa, ili haya maji machache yanayopita wakati wa mvua tuyahifadhi mahali, tuyachukue hayo maji tuweze kufanya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshapata *site* pale kuna eneo linaitwa Mbwasa, ni *site* nzuri ambayo bwawa kubwa linaweza likapatikana pale. Upembuzi yakinifu unaweza kufanyika, tunaomba hela...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Chiligati. Dakika zilizobaki hazitoshi kwa mchangiaji yeyote. Tumeweza kupata wachangiaji 19 kwa asubuhi ya leo, kwa hiyo, tunaenda vizuri na tunaendelea na ile Kanuni yetu ya Uwiano na kila mmoja wetu anapata haki sawa. Kwa upande huo, natumaini kabisa hatutailaumu Meza.

Sasa niishughulikie ile Miongozo; kama nilivyosema, utaratibu ambao tunajaribu kuutumia sana awamu hii ni kuhakikisha kwamba, fursa na haki ambayo mnakuwa mmeipata ya kwamba, utachangia, ni kweli utachangia, kwa sababu muda ambao tuna kuwanao tunaugawanya kwa idadi ya wachangiaji na kwa uwiano wa vyama na kadhalika. Tusipofanya hivyo, itaonekana kuna baadhi ya watu ambao tumewaonea. Tukipata dakika mbili, tatu kama hizi ambazo zimebaki hapa, ndiyo tunashughulikia mambo mengine ambayo yamejitokeza.

Sasa nianze na lile jepesi zaidi nalo ni la lugha ambayo haikueleweka humu ndani kutokana na maneno ya Mheshimiwa Juma Nkamia. Mheshimiwa Nkamia, ulisikia kilichosemwa, kabla sijatoa Mwongozo wangu ningependa kukusikia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Labda nilitumia nahau zaidi wakati ule, nilichokuwa ninamaanisha ni kwamba, kwanza, ni nini kilichonifanya mpaka nikasema vile? Wakati umenipa nafasi ya kuchangia kulikuwa na maneno ya chinichini ambayo rafiki yangu kipenzi, Mheshimiwa Sugu, alikuwa anayasema. Sasa *as a human being,* nina *character* tatu pia kama binadamu mwingine yeyote. Kwa hiyo, ile ikani-*drive, you know,* nikafika hatua nikatumia lugha ambayo nilikuwa na maana kwamba, mimi ninaongea na baba yako siongei na mtoto, ndiyo ilikuwa maana yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naongea na Kiti. Nilikuwa namfahamisha tu kwamba, naongea na Kiti, ambaye ni baba yake, lakini nilikuwa siongei na yeye kama mtoto.

**MBUNGE FULANI:** *...*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo lugha kama hii unayoisikia sasa. Wakati mimi bado naendelea, anaendelea tena kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *anyway,* niseme tu kwamba, nasikitika kwa hilo. Mheshimiwa Sugu, ni rafiki yangu na nyimbo zake ninazo, kwa hiyo, ninamwomba radhi, nitaendelea kusikiliza nyimbo zake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Nkamia na kwa kweli, mimi ninavyowafahamu Waheshimiwa wawili hawa, ni marafiki wa karibu sana.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli!

**NAIBU SPIKA:** Na walikuwa kwenye Kamati moja kwa miaka miwili na nusu hii tuliyoianza, Mheshimiwa Nkamia, akiwa Makamu wa Mwenyekiti na Mheshimiwa Sugu, akiwa Waziri Kivuli, ndani ya Kamati hiyohiyo moja. Ni watu ambao wamefanya kazi kwa karibu, wamesafiri maeneo mengi; wanajuana, ni Waarabu wa Pemba hawa, lakini kwenye Bunge letu hapa, wajitahidi kuangalia lugha zao zisitufikishe hapa ambapo wamejaribu kutufikisha. *(Kicheko)*

Vilevile, nitoe Mwongozo sasa kwa Wabunge wote; jamani, dakika tunazochangia ni chache, kila mmoja akisimama tunarudia lilelile. Kama Kiti tujitahidi kuona kwamba, lugha zetu haziwakwazi wengine kwa kadiri inavyowezekana, tujitahidi Waheshimiwa.

Maneno ya namna hii yako mengi pande zote na umesikia wengine wakisema Serikali hii pumbavu na hakuna aliyejibu, kwa hiyo, tuchukue muda huu kurekebishana. Narudia yaleyale aliyoyasema Mheshimiwa Spika, isije kuwa mkuki kwa nguruwe; hilo limeishia hapo.

Mwongozo wa pili uliombwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kuhusu maneno ambayo Mheshimiwa Lusinde aliyasema. Nashukuru Mheshimiwa Sakaya, ameniandikia kwamba, amefuta ule Mwongozo wake na mimi naungana mkono na yeye. Maana siku hizi bwana mambo haya, kuna *DNA* na nini; tunaweza kufikishana mahali ambapo sasa haya mambo haya, lakini kafuta Mwongozo wake, kwa hiyo, namshukuru sana kwa uono huo. Hii ndiyo faida ya kusema kwamba, nitatoa Mwongozo baadaye, natoa nafasi ya watu kufikiri upya; kuliko ningekurupuka saa ileile ningeweza kusema maneno ambayo labda siyo sawasawa sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mwisho Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie Wabunge wote kuwa, kuna Wabunge 65, bado hawajachukua Vitambulisho vyao vya Uraia. Vimeshaletwa, viko pale Msekwa na nafasi ya kuvichukua ni leo na kesho tu. Tangazo hili nimepewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Nchimbi, kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote, ambao hamjachukua Vitambulisho vya Taifa, mwende kuvichukua vitambulisho hivyo.

Baada ya maneno haya, naomba sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo pia ina masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Tunao wachangiaji wa kutosha kabisa, naomba tuwape nafasi, tutaanza na Mheshimiwa Hussein Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda na Mheshimiwa Leticia Nyerere ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameniwezesha kunipa afya njema kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kidogo niwaeleze Watanzania kuhusu tatizo ambalo liko mbele yetu, ambalo linaleta maafa katika nchi hii walielewe. Hili ni tatizo la migogoro ya dini, tunaliona kama vile ni la kuigiza lakini matokeo yake siyo mazuri sana kwa sababu kila mmoja ana imani yake; imani, amani na ushabiki ni vitu vitatu tofauti. Amani ni kitu ambacho kinategemewa na huyo ambaye ana imani yake, kwa sababu huwezi ukafanya ibada zako pakiwa hapana amani na wewe mshabiki huwezi ukawa una ushabiki wako bila kuwa na amani, kwa hiyo, tukienzi kitu kinachoitwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, kwa sababu mara nyingi tumesikia pembe nyingi za nchi yetu migogoro hii imetokea, sasa tunaomba Serikali ilichukulie umakini sana jambo hili na kuweza kuwatia nguvuni ambao wanataka kuleta janga kubwa katika nchi yetu. Lazima tuangalie chanzo ni nini, tusiwe tu tunaangalia kwamba kuna migogoro ambayo inajitokeza, tuangalie chanzo ni nini; kwa sababu kuna mambo ambayo yanasemwa na hawa ambao wanaitwa waanzilishi wa migogoro, ni ya kweli.

Nitazungumzia jambo moja; leo Watanzania tumeambiwa urithi wetu ni *Kilimanjaro* na *Pilsner lager.* Nina imani kwamba, kuna Wakristu ambao hawatumii pombe, kuna Waislamu ambao hawatumii pombe na kuna Waislamu ambao wamekengeuka wanatumia pombe na kuna Wakristu ambao wamekengeuka wanatumia pombe; lakini tumerithishwa kwamba, wote sisi urithi ni wetu, mtu akizungumzia analikemea hilo inaonekana kwamba huyu analeta matatizo na mambo mengine yako mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nalitolea tahadhali na ushauri kwa Serikali yetu ni la wafugaji na wakulima. Hili nalo linafukuta karibu pembe zote za nchi yetu, ninaiomba Serikali ichukue ushauri huu kwamba, iwatengee wafugaji maeneo yao rasmi ya ufugaji na mashamba ili waweze kuotesha nyasi, waweze kufuga mifugo yao kwa utulivu na wakulima nao wawe na maeneo yao ili kuepusha mgogoro ambao unaweza ukajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo linazungumzwa sana ni janga ama maafa yanayotokana na madawa ya kulevya. Naiomba Serikali ichukue ushauri huu, suala hili liwahusishe Wananchi wote wa Tanzania, kwa kuwapa motisha wanaotoa taarifa na kufanikisha kukamata vitu hivyo ambavyo vinaitwa madawa ya kulevya; kwa sababu bila kuwashirikisha Wananchi na tunafahamiana, hatuwezi tukafanikiwa kupambana na vitu kama hivyo ambavyo tunavizungumza hapa. Wananchi wakihusishwa, wakapewa motisha kwamba mali itakapokamatwa hii ikapigwa thamani yake labda milioni moja, asilimia 50 apewe yule ambaye amefanikisha kutoa taarifa; hili nalo linaweza likafanikisha kupunguza ama kumaliza kabisa tatizo hilo la madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, uharibifu wa mazingira nalo ni janga kubwa katika nchi hii. Leo misitu imekwisha, miti imekwisha, vyanzo vimeharibiwa na Watanzania wenyewe. Ninaiomba Serikali izidi kutoa elimu na pesa nyingi kwa ajili ya kuwaelimisha Wananchi na semina mbalimbali kuhusu uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudi upande wa Kanda ya Ziwa; kwa kweli Kanda ya Ziwa tuna masikitiko makubwa, Ziwa tunalo ubavuni lakini ukosefu wa maji unazungumzwa kila leo; kwa nini? Tunaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kutoa majumuisho hapa, utuletee jambo la maana kabisa ili na sisi tuelewe kwamba bajeti hii tumo humo ndani, kwa sababu maji tunayaangalia lakini hatuna maji. (Makofi)

Mkoa mpya wa Geita kama ilivyozungumzwa, kwa kweli nako tatizo la maji limekuwa ni hadithi ya muda mrefu, zaidi ya miaka sasa. Jimboni kwangu Nyang'hwale tatizo la maji ni kubwa sana na nimewahi kuuliza hili suala Bungeni nikaambiwa kwamba, kuna pesa imeshatoka, shilingi milioni 30 ya upembuzi yakinifu, lakini mpaka leo hatujaona chochote kile ambacho kimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la nishati ya umeme Jimbo la Nyang'hwale. Napenda

kuipongeza Serikali kwa kufanya juhudi kubwa, nguzo tayari zimeshasimikwa na nyaya zimeshasambazwa, lakini leo miezi sita umeme haujawashwa. Niliwahi kuuliza hapa nikajibiwa kwamba, umeme huu utawashwa hivi karibuni; sasa ninashindwa kuelewa nitawaeleza nini Wananchi, lakini utakapowaeleza wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu umeme huu utawashwa lini, basi nadhani Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale watakuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie kidogo suala la afya; kwa kweli Jimbo la Nyang'hwale tuna vituo viwili vya afya na tuna zahanati, lakini cha ajabu vituo vya afya vile leo miezi tisa hawajapata bajeti ya ununuzi wa vifaa vya zahanati na vituo vya afya havijapata madawa kwa miezi tisa. Pamoja na kwamba, Kituo cha Afya cha Kalumwa, Mheshimiwa Rais alisema kwamba, kitapandishwa iwe Hospitali ya Wilaya, lakini hakuna mabadiliko ya aina yoyote; mpaka leo hii wagonjwa wanakwenda pale hawapati dawa, hali ya zahanati yenyewe na kituo cha afya ni kibovu kabisa, kwa kweli hali hii inasikitisha. Pia tuna kuna kituo kingine Kata ya Nyang'hwale nacho hakina madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa kifupi kuhusu suala la elimu. Kwa kweli, elimu matatizo yake wachangiaji wengi wamezungumza na mimi naomba nigusie kwa upande wa Jimbo langu la Nyang'hwale. Matatizo yapo mengi, ndiyo maana elimu imeshuka; walimu wachache, madarasa hayatoshi, vitendea kazi, vitabu vya kufundishia havipo, madawati hali ni mbaya, lazima elimu ishuke. Haiwezekani mtoto amekwenda kusoma shuleni anafikia kukaa chini kwenye vumbi, akili yake haiwezi ikashika vizuri. Kwa hiyo, suala hili nalo tujaribu kuliangalia, ni chanzo cha kushuka kwa elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo; Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale wana masikitiko makubwa sana; pembejeo zinakuja kwa muda ambao siyo mwafaka na tumewahi kupokea mbegu ambazo ni mbovu. Wanajiuliza hivi Serikali hailitambui jambo hili? Ninaiomba Serikali ijaribu kufuatilia kwa nini pembejeo zinakuja zimechelewa na pia

zinakuja mbegu ambazo hazina ubora; hili ni tatizo kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano; Jimbo la Nyang'hwale, Wilaya mpya ya Nyang'hwale ina matatizo ya mawasiliano. Wilaya hiyo inakata kumi na mbili, lakini ni kata moja tu ambayo ina mnara, kata zingine kumi na moja hazina minara. Kwa hiyo, tunaomba mawasiliano, kata zote zitakapokuwa na mawasiliano ni moja ya kuchochea maendeleo katika Wilaya yetu mpya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara; Mheshimiwa Rais alikuja kipindi cha kampeni akaahidi barabara ya lami, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara ya lami izungumwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Nassor Amar. Sasa ni Mheshimiwa Christowaja Mtinda na Mheshimiwa Leticia Nyerere, wao watagawana dakika tano tano. Mheshimiwa Mtinda ataanza.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi naomba nichangie ukurasa wa 59 mpaka wa 61 kuhusu suala zima la elimu hususan Mpango wa MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa MMES II ulianza mwaka 2010/2011 mpaka mwaka 2015/2016 ndiyo tunatarajia kwamba huu Mpango utakwisha. Mpango huu unaeleza wazi kwamba, kila Mwanafunzi wa Sekondari ya Serikali anawajibika kupata shilingi 25,000 na hizi shilingi 25,000 zimegawanywa kwa aina mbili; nusu (shilingi 12,500) zitatumika kununua vitabu vya ziada na kiada na shilingi 12,500 zingine zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya mitihani na shughuli nyingine za utawala wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nazungumzia hizi pesa? Mwaka 2011/2012, kutokana na utafiti uliofanywa na Haki Elimu, kitabu hiki kimetoka Septemba, 2012, naomba watendaji mkisome; kinaeleza kwamba, utafiti uliofanywa umeonesha Hazina ilitoa shilingi elfu ishirini na tano elfu na themanini na mbili kwenda katika shule zote za Sekondari za Serikali, lakini katika kutoa hizo pesa, inaonekana Hazina inatoa hela kwenye akaunti za Halmashauri, Halmashauri zilipokea shilingi elfu kumi na tisa mia moja hamsini na saba, pungufu ya shilingi 5,928. Kwenye Halmashauri, pesa zinatakiwa ziwekwe kwenye akaunti za shule, lakini akaunti za shule zilipokea jumla ya shilingi 14,178, pungufu ya shilingi 4,979. Kwa hiyo, pesa zilizopotea njiani katika ngazi hizi mbili jumla ni shilingi 10,907.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa Haki Elimu unaonesha kwamba, pesa za MMES II, ambazo ni mahususi kununua vitabu vya ziada na kiada, pamoja na shughuli zote za mitihani na utawala wa shule, zimekuwa zikipotea kutoka Hazina na kutoka Halmashauri kwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; hizi pesa zinakwenda wapi? Nani anakula hizi pesa njiani? Nani ni mdokozi wa hizi pesa?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakapokuja kutoa majumuisho, mimi sitaunga mkono hoja mpaka nipate maelezo kamili kwamba nani ni mdokozi wa hizi pesa kutoka Hazina kwenda Halmashauri na kutoka Halmashauri kwenda katika akaunti za shule. Matokeo yake, wanafunzi hawapati vitabu vya ziada vya kutosha hasusan vya sayansi, wazazi wanaendelea kuchangishwa michango mingine ya kununua chaki hadi kufuli. Kule Singida ninakotoka, wanafunzi wanachangishwa hela za kununua kufuli za milango na chaki za kuandikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka maelezo nani ameshakamatwa kwa udokozi wa hela za MMES ambazo zinatakiwa zitoke shilingi 25,000 kwa kila Shule ya Sekondari ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa katika eneo hilo hilo la elimu, naomba nizungumzie usimamizi mzima wa suala la elimu. Kumekuwa kuna mkanganyiko hapa, Elimu ipo TAMISEMI, Elimu ipo Wizara ya Elimu; sasa Wizara ya Elimu inatunga Sera, Wizara ya Elimu inasajili shule, ikitunga sera mbovu maana yake tutatoa mitaala mibovu, wanafunzi watafeli; ikisajili shule zisizokuwa na vigezo wanafunzi watafeli; lakini ukienda kumwajibisha Waziri wa Elimu atasema hapana mimi sisimamii Sekondari wala sisimamii Shule ya Msingi nasimamia vyuo; nani awajibike?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna kutupiana mpira hapa, matokeo mabaya ya Elimu ya Sekondari ya juzi, *form four* ya juzi, wanawajibika TAMISEMI kwa maana kwamba ni wasimamizi wa shule, *at the same time* wanawajibika Wizara ya Elimu kwa sababu wanatunga Sera, lakini likija suala la kuwajibika nani a-*step down* wanatupiana mipira!

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri suala la elimu liangaliwe kwa jicho la sawasawa, kama ni kutenganisha elimu ikae kwenye Wizara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wakati tunaendelea na malumbano ya kisiasa humu ndani, Kwimba kuna kaya 328 hawana makazi kwa sababu ya mafuriko. Pamoja na jitihada za Serikali, naomba wapeleke maturubai mengine, chakula cha kutosha na vilevile wapeleke mbegu kwa ajili ya kupanda na kuotesha dengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaendelea na haya malumbano ya kila siku humu ndani, kuna wanawake wa Kwimba na hata Kanda ya Ziwa kwa ujumla, wanaamka usiku wa manane wakitafuta maji na matokeo yake

wanapochelewa kurudi nyumbani wanaambulia kipigo. *Population* ya Kwimba ni watu zaidi ya 316,000 na vilevile tuna mifugo ambayo ni 500,049, tunahitaji maji ya kutosheleza *population* hii ya viumbe 805,000 na siyo 316,000 tu, kwa sababu wanyama au mifugo ni sehemu ya familia yetu. Nashangaa Serikali inatuambia eti tupunguze mifugo kwa kuuza; tutamwuzia nani? Unafahamu sisi kila familia ina ng'ombe; tutamwuzia nani ili tupunguze? Tunachohitaji ni viwanda vya kusindika nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoendelea na malumbano humu ndani, kuna Wanafunzi wa Shule ya Ngudulugulu, wanakalia mawe tena yenye ncha kali. Ninashangaa halafu tunaanza kushangaa kwa nini wanafunzi wamefeli! Ninyi mngekuwa mmekaa kwenye mawe tena yenye ncha kali mngeweza hata kufikiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Waziri husika aende akaitembelee Shule ya Ngudulugulu na asiende bila madawati, angalau aende na madawati 300; na kabla hajaenda Ngudulugulu aende tu hapa *Mlimwa* A *Primary* hapa Dodoma, ajionee jinsi gani Walimu ambao wanatarajia kufundisha watoto wamelundikwa, Walimu watano wanalala chumba kimoja. Hii ni aibu, Taifa letu halitilii maanani elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuvutana humu ndani wakati wafugaji na wakulima wa Kwimba na Kanda ya Ziwa kwa ujumla, hawana bei ya pamba. Tunaiomba sasa Serikali hususan Ofisi ya Waziri Mkuu, mfanye juu chini, wakulima wa pamba wa Kwimba na Kanda ya Ziwa yote, mtenge ruzuku ili waendelee kulima hii pamba ambayo imekuwa ikishushwa bei kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu usemi wa Hayati Baba wa Taifa, ambao unasema hivi; naomba ninukuu kwa Kiingereza: "*We cannot hope to solve our problems by pretending they do not exist.*" Kwa hiyo, ni lazima tutambue kwamba tuna matatizo, tuache kujifanya kwamba hatuna matatizo, nendeni mkashughulikie matatizo yetu. Sisi

Wananchi wa Kwimba, tunawataka Mawaziri husika waje hasa kwa suala la elimu wajionee Wanafunzi wa Ngudulugulu wanavyoteseka, wanavyojeruhiwa kwa kukaa kwenye mawe tena yenye ncha kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nilikuona.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sina nia ya kuchukua muda mrefu, nilitaka kumpa taarifa tu mzungumzaji aliyekaa; pamoja na malumbano haya ya kisiasa yaliyopo anayoyasema, ambayo huwa siyapendi sana, lakini Serikali siyo kwamba haifanyi kazi, Serikali ipo kazini; jana Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ametupa taarifa, hii taarifa siyo ngeni tunaijua kwa sababu mtandao wa Serikali ni mkubwa. Mkuu wa Mkoa ametupa taarifa ya habari ya mafuriko na jana ile ile tumeidhinisha kama walivyoomba, tani 22.2 za chakula na fedha na tumewapelekea maturubai mia tano kama walivyoomba. Kwa hiyo, tupo hapa lakini Serikali ipo kazini, kwa taarifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri na tunakushukuru kwa niaba ya Wananchi wa Ngudu, natumaini pia hizi ncha kali zitashughulikiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Chagulla.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie mambo machache, kwa sababu ya muda nitajielekeza sana kwenye yale ninayotaka kuzungumza lakini yapewe umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba tu na mimi kwa ufupi sana, niwaeleze Watanzania kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inajitahidi sana katika kuwafanyia kazi na kuhakikisha kwamba, yale tuliyoahidi kwenye Ilani ya

Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, yanatekelezwa kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Serikali yoyote Duniani ambayo inamaliza matatizo ya Wananchi wake kwa wakati mmoja na ndiyo sababu maendeleo ni mchakato, mchakato hauwi wa siku moja. Tunachofanya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge wengine wa ukweli ni kuisimamia Serikali ili iweze kutekeleza ahadi zake kwa Wananchi. Hilo ndiyo jukumu letu kubwa sana.

Nataka nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, akiwa ziarani kule Kilosa, ametamka jambo kubwa sana kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi hatujivunii ukubwa, hatujivunii madaraka, lakini tunajivunia kazi ambazo tunatekeleza kwa Wananchi ambao wametuweka madarakani; na kwamba huo ndiyo wajibu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kuhakikisha kwamba, inasikiliza kero za Wananchi na kuzifanyia kazi. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi aendane na kauli hiyo ya Katibu Mkuu wa Chama chetu cha Mapinduzi ili Wananchi waendelee kujenga imani na Serikali yao ya Chama hiki.

Suala la kwanza katika yale niliyopanga kuzungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu hili naomba ulitolee ufafanuzi kwa sababu ni la Watanzania wote. Kwangu kule Mbozi na Mkoa wa Mbeya, gari aina ya Noah zimesajiliwa kwa ajili ya kufanya biashara, lakini zimezuiwa zisifanye biashara, kwa sababu zimeambiwa hazina viwango vya kufanya kazi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, haingii akilini kwamba unaruhusu Pikipiki za miguu miwili, unaruhusu Bajaji sijui za miguu mitatu, ambazo hazina hata usalama ambao upo kwenye magari ya Noah, yanafanya kazi, yanabeba abiria, watu wa SUMATRA wanasema Noah hazina viwango! Hili ni jambo la ajabu sana na ni jambo la kusikitisha, tunaomba Waheshimiwa wanaojenga chuki kwa Watanzania na Serikali yao halina sababu. *(Makofi)*

Kule Mbeya tumekuwa na mvutano mkubwa kweli kati ya Serikali ya Mkoa na Wamiliki wa Noah. Namshukuru

sana Mkuu wa Mkoa na timu yeke, wamejaribu sana kuzungumza na watu wa SUMATRA ili waruhusu zile gari zifanye kazi, lakini inaonekana watu wa SUMATRA wametoa kibali mpaka mwezi wa sita, baada ya hapo hawataziruhusu. Unafanyaje hivyo wakati Pikipiki na Bajaji bado zinaendelea kufanya kazi?

Watanzania hatuelewi na tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili mlitafutie ufumbuzi ili watu wa Noah ambao wamekopa pesa kwa ajili ya kununua magari kufanya biashara, waweze kupata faida, waweze kufanya biashara na kwa maana hiyo kuendesha maisha yao.

Jambo la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu nina *Hansard* hapa ya tarehe 22 Juni, ambayo Waziri wa Fedha wa wakati huo, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa, alisema hapa Bungeni kuhusu ushuru kwa watu wa Bodaboda na naomba ninukuu. Alisema hivi: "Mheshimiwa Spika, baada ya kusikiliza mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge walio wengi kuhusu suala la utozaji kodi Vijana na Wananchi wa kipato cha chini, hasa wale wa Bodaboda, Serikali inapendekeza kuwa tabaka la kwanza libadilishwe kutoka mapato yasiyozidi shilingi milioni tatu kuwa mapato yasiyozidi milioni nne. Tukipandisha hilo tabaka la kwanza kutoka milioni tatu mpaka milioni nne kama mapato ghafi ya chini ya kiwango cha kutoza kodi, kiwango hiki cha chini kisichotozwa kodi, kinapendekezwa kupandishwa ili kuwafanya vijana wetu, wafanyabiashara walio wengi wadogo wadogo kutotozwa kodi ya mapato."

Cha ajabu hili liliahidiwa na Serikali humu ndani na *Hansard* hii ninayo, lakini leo vijana hawa wa bodaboda wamepandishiwa kwamba mapato yao ghafi ni zaidi ya milioni nne, kwa hiyo, wanakuwa *subjected* kwenye kodi ambayo Serikali iliahidi kuifuta tena hapa ndani ya Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili linaleta usumbufu, tulitafutie ufumbuzi pia ili vijana wetu waweze kuwa na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, mwaka jana tarehe 29, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe alisema ndani ya Bunge, nina *Hansard* ya tarehe 29, kuhusu Bodi ya

Kahawa na nilileta mbele ya Bunge kwamba Bodi ya Kahawa imeundwa kinyume na sheria ambayo inasimamia zao la kahawa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na ahadi yako, mwaka mzima mpaka leo ndiyo Waziri wa Kilimo anasema Bodi mpya inateuliwa. Hivi uwajibikaji wa Serikali uko wapi kama suala ambalo Serikali imekiri limechukua mwaka mzima bado halifanyiwi kazi; Watanzania waelewe nini? Hizi ndizo changamoto za Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusichelewe sana kuchukua maamuzi kwa mambo ambayo yako dhahiri kabisa, sheria imevunjwa, jambo linachukua mwaka mzima halijatatuliwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni pembejeo za kilimo. Tumeambiwa kwamba mwaka huu tutabadilisha mfumo wa *voucher* kama ambavyo pia Serikali ilishatoa tamko hapa ndani ya Bunge. Sina uhakika ni kwa kiwango gani Serikali imejiandaa na zoezi hili.

Taarifa ya *CAG* imesema, moja ya changamoto ambazo Serikali imezipata kwenye dhana ya KILIMO KWANZA ni; kwanza, *voucher* zenyewe kuchelewa kuwafikia wakulima; pili, wezi wanaopatikana na jambo hili kutochukuliwa hatua na kwa maana hiyo zoezi lenyewe kutokuwa na uzito unaostahili; na tatu, wanufaikaji wenyewe ni wachache sana.

Sasa tunasema waunde vikundi kwa mwaka huu ili wapate mkopo kupitia huko. Sina hakika je, maeneo yote yenye wakulima vikundi hivi vimeundwa, maana liko tatizo inawezekana vikundi mahali pengine haviko; je, wakulima wale hawatafaidika?

Pili na muhimu zaidi, je, vikwazo vya Benki, kwa maana tunasema kwamba, Serikali inatoa *guarantee* mabenki yatakopesha; je, mabenki hayatakuwa na vikwazo kwa ajili ya vikundi hivi kwenda kukopa huko kwenye Benki? Maana huko ndiyo kwenye shida, tunaweza tukafikiri kwamba tunalitatua lakini likatupa shida zaidi huko baadaye.

Naomba Serikali ijiandae vizuri juu ya utaratibu huu, lakini unajiuliza, je, utaratibu huu utafanya wakulima wanaopata *voucher* hizi au mbolea ya pembejeo za Kilimo waongezeke? Maana yake, kama ni wakulima wale, mwaka jana nadhani wakulima waliopata pembejeo siyo zaidi ya milioni moja na laki nane. Je, watakuwa hao hao, wakati wakulima wanaweza wakawa zaidi ya milioni sita au saba katika nchi hii lakini unawapata wasiozidi milioni moja na nusu; je, utaratibu huu mpya utakuwa na tija? Wakulima wengi watafaidika? Haya ndiyo majibu ambayo tunapenda pia Watanzania ambao wanapenda kulima waweze kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi suala la misamaha ya kodi. Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali ameundwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali na amepewa kazi hiyo ili aisaidie Serikali kuona kwamba pesa zinatumika swasawa. Mwaka jana, Mheshimiwa *CAG,* alitoa ushauri kwa Serikali kwamba, misamaha ya kodi ipunguzwe na mwaka juzi misamaha ya kodi ilikuwa karibu trilioni moja. Baada ya ushauri ule wa *CAG,* mwaka unaoishia Juni, 2012, misamaha ya kodi imepanda zaidi kwenda trilioni moja na bilioni mia tisa, maana yake kumekuwa na ongezeko la misamaha ya kodi kwa karibu bilioni mia tisa.

Sasa huyu *CAG* amewekwa pale aishauri Serikali, ameshauri misamaha ya kodi ipunguzwe ili pesa zile ziende kwenye Miradi mingine kuwasaidia Watanzania. La ajabu sana misaha ya kodi imezidi kuongezeka; hivi kweli tutaenda kwa namna hiyo? Mimi naomba Serikali iliangalie hili na iweze kurekebisha; vinginevyo, maendeleo tunayoyakusudia hayatapatikana kwa *speed* tunayoitaka.

Suala lingine, wamezungumza wenzangu; *pension* kwa wastaafu wetu bado ni kiwango kidogo sana, tunaomba Serikali iangalie upya viwango vya *pension*. Leo mtu wa chini analipwa karibu shilingi 51,000, huyu mtu ameitumikia Serikali kwa miaka 30 au 40 leo unamlipa shilingi 51,000 kwa mwezi; shilingi 51,00 hizi hata nauli ya kutoka Mwanza mpaka Dar es Salaam haitoshi; je, kama mtu ana shida atatekeleza vipi mambo yake?

Mimi naiomba sana Serikali, iangalie viwango hivi vipya, viwango viwe *realistic* hasa katika kipindi ambacho mfumko wa bei katika nchi hii ni mkubwa sana; kumlipa shilingi 51,000 kwa mwezi ni kama kumtania tu mtu ambaye ameitumikia nchi kwa uaminifu mkubwa sana.

Suala la mwisho, ninaomba Serikali iendelee kuzungumza na Walimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Walimu wanatishia kugoma, yako mazungumzo wanatishia kugoma kwa sababu hawajafurahia mwenendo wa Serikali katika kuzungumzia suala kupanda kwa mishahara yao. Naomba Serikali iliangalie hilo ili tusije tukaingia kwenye migomo tena na kusababisha watoto wetu wakaendelea kufanya vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Josephine Chagulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

**MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kabla sijaanza kuchangia, mwaka 1974, Tanzania na Burundi walitishiana pale kidogo. Mwaka ule Tanzania ilitupa bomu nchini Burundi, halafu Warundi wakatupa bomu Tanzania. Walipotupa yale mabomu mawili yaliangukia ndani ya kijiji chetu. Yalipoangukia ndani ya kijiji chetu, tulipotawanyika hakuna aliyejua mke amepitia wapi, mtoto amepitia wapi, mbwa wameenda upande gani, kuku wamebaki au wameenda wapi. (Makofi)

Mimi naomba, kwa Watanzania ambao hawajawahi kuona dalili ya vita, wasiombee. Naomba Vyama, Dini na Madhehebu, hebu tuienzi hii amani tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nirudi kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, nakupongeza kwamba umeweza kutupa Halmashauri za Wilaya Mpya. Ombi letu watu wa Buhigwe wanauliza lini wafanye maandalizi ya sherehe ya kumpokea Mkurugenzi?

Umesema vizuri kabisa kwenye hotuba yako; lini waandae sherehe ya kumpokea Mkurugenzi wa Wilaya ya Buhigwe? Wanataka hilo ili Halamashauri zao zianze kuwa na vikao vyao ili tuweze kupanga bajeti yetu vizuri. Hilo nalo tunaomba utupe majibu kwa sababu umetuambia tu kwa ujumla hujatuambia ni lini utatuteulia hao watu.

Changamoto ya elimu; walimu ni tatizo, nyumba ni tatizo, napenda nishauri; kwa nini tusitumie *NSSF* ambayo imekubali kuingia mkataba na Serikali, ijenge nyumba za walimu, ijenge vyumba vya madarasa halafu Serikali mtaendelea kuilipa taratibu wakati mmetatua hilo tatizo. Buhigwe tuna matatizo ya nyumba za walimu, kiasi kwamba walimu wengine wanakimbia. Tunaomba *NSSF* watakapojenga nyumba hizo za walimu walioko pembezoni na hata walioko katikati ziwekwe *solar*, walimu waweze kusahihisha mitihani hata usiku. Walimu wanashindwa kusahihisha mitihani sasa wanafunzi watafaulu vipi? Kwa hiyo, nalo hilo naiomba Serikali iliangalie kama inaweza kulichukua.

Wananchi wangu wa Manyovu wamenituma wanauliza kwamba walifeli namna gani? Wanafunzi wamefanya Mkutano wakaniambia hawajaelewa kwa nini wamefeli. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali, angalieni, pamoja na kwamba kuna Tume, tuangalie pendekezo la wao kurudia mitihani, lipewe umuhimu.

Tumepata fedha za *RADA,* lakini mchakato wa kununua hayo madawati naona unaenda kidogo kidogo. Tunaiomba Serikali iharakishe, kama kule Kahama wamesema wanakalia mawe yenye ncha kali; siyo kitu kizuri.

**MBUNGE FULANI:** Na wala hayapo!

**MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Afya; tunalo tatizo la madawa katika nchi hii, lakini baada ya kuwa tumeangalia, tumegundua mtu anayesababisha dawa zisiwepo nchini ni Serikali. Serikali imekuwa ndiyo namba moja ambayo imefanya dawa zisiwepo nchini. *MSD* wanaidai Serikali zaidi ya bilioni 52, kwa

ripoti tuliyonayo sasa. Sasa kama wamekata mtaji wa bilioni 52 wao wapate dawa vip? Ruzuku inayotolea kwa *MSD* kwenye kila *quarter* kama wameahidiwa bilioni 45, zinaenda bilioni mbili. Sasa mnataka madawa nchi hii yaweze kuwa wapi?

Mimi ningeshauri kwamba, Wananchi wajue kwamba Serikali inazembea kwenye suala hilo. *MSD* wanajitahidi sasa kupeleka madawa kwenye vituo, ambayo ni njia moja nzuri ya kuwakomboa Watanzania, lakini tunaomba upande wa Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu ulichukulie maanani kabisa.

Upande wa kilimo; kweli pale kwangu Manyovu, tunalima Kahawa na kahawa tunayolima Manyovu ndiyo bora Tanzania nzima. Fanya utafiti usifanye ndiyo nimekwambia. Wapo wakulima wanaokuja kulanguliwa na makampuni yaliyoko mikononi. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Wizara ya Kilimo, wale wote walioenda kukopa Kahawa kwa wakulima wetu wa Kata za Manyovu, Buyama na Buhigwe, wote wakamatwe ili fedha zao ziweze kurudishwa. Kwa sababu huo ni utapeli, Wananchi wetu wanashindwa kulipa hata ada za wanafunzi. Kwa hiyo, tungeomba suala hili Serikali iliangalie.

Bei ya kahawa yetu mwaka jana ilikuwa shilingi 7000 mpaka 8000, sasa hivi imeshuka chini kabisa imekuwa karibu 4000. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iliangalie hilo.

Ahadi za Rais; napenda nimpe shukrani Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ametufanyia makubwa Mkoa wa Kigoma, lakini tunamwomba ile Barabara ya Manyovu - Kasulu nayo kama alivyoahidi, iweze kuungana sasa na ile ya Buhigwe - Nyakanzi. Kilio chetu ni kwamba, Serikali iendelee kuyafanyia kazi.

Naomba niipongeze Wizara ya Mawasiliano, imeanza kuchukua hatua, sasa hivi tumepata mnara mmoja wa Tigo Tarafa ya Myama, ambao tulikuwa hatuna kabisa vijiji 13. Tunaomba sasa mnara wa *Vodacom* na *Airtel* uwekwe pale. Tuna tatizo la mnara tena pale Makao Makuu ya Wilaya

Mpya Buhigwe na tunahitaji mnara mmoja sehemu ya Kinasi. Tunakushukuru sana Mheshimiwa January Makamba na timu yako, kama mtaendelea vizuri namna hiyo na sisi tutawaunga mkono.

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, niliwaomba mnada wa Myama mkasema mtatoa mwongozo bado hamjamtoa; naomba mnipe majibu kwa nini hamtaki kufanya hivyo?

Serikali imeendelea kushabikia wizi; kutokulipa Mwenyekiti wa Kijiji, kutomlipa Diwani vizuri ni sehemu ya Serikali kubariki wizi wa Miradi. Kwa hiyo, ningeomba sana ili tusiwe sehemu ya kubariki Miradi hiyo kuibiwa, basi Serikali iwaangalie hao Wenyeviti wa Vijiji. Unampa kijiji kizima Miradi inaenda pale, halipwi hata senti moja; hivi anaishije? Huwezi kujua kwamba lazima aibe? *(Makofi)*

Vitongoji wameendesha sensa vizuri mmeshindwa kuwalipa, shilingi 5000 mliwaahidi Viongozi wa Vitongoji wa Vijiji mmeshindwa kuwalipa; Serikali bado mnasusua kuwalipa, hebu tunaomba muwalipe, hizi kelele za siasa ndogondogo wengine wanapitia hukohuko ili haya mambo yaishe.

Ziko *pension* za wazee, mipango ipo, tunaomba isirudi nyuma. Wazee wote wakulima na wafanyakazi walioitumikia nchi hii, kwa kweli wamechoka na hii *pension* ianzishwe mara moja ili na wao waweze kujikimu na mambo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Obama. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Nkumba.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tumekuwa tunazungumza hapa Bungeni miaka yote kwamba, kasungura ni kadogo, fedha haitoshi na ni kweli fedha

haitoshi; Miradi ya maendeleo miaka yote inatengewa fedha kidogo kwa sababu pesa kwenye Serikali hakuna. Fedha nyingi za maendeleo tunatenga fungu kutoka kwa wafadhili, wakati huo huo wafadhili hawatoi fedha kwa wakati, wengine hawatoi kabisa na wengine wanatoa wakipenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza ni kwamba, mapato yetu ndani ya nchi bado hatujaweza kuyasimamia vizuri. Tunazo rasilimali nyingi, tuna vyanzo vingi sana vya mapato kwenye Halmashauri zetu, kwenye Manispaa, kwenye Majiji, kinachokosekana ni uzalendo, usahihi na umakini kwenye ukusanyaji wa mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la ajabu kusikia Manispaa ya Ilala hawawezi kukusanya hata nusu ya walichopangiwa. Manispaa ya Kinondoni, angalia tu mfano mmoja, Stendi ya Ubungo kwa siku inaingiza kipato kiasi gani? Soko la Kariakoo, soko kubwa Tanzania linaingiza kipato kiasi gani kwa siku? Lakini Manispaa hiyo hiyo inalalamika kwamba haina pesa, haijakusanya pesa, inategemea Serikali iwape pesa kwa ajili ya Miradi yote ya Maendeleo!

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiposimamia vizuri mapato, Serikali isipowajibika, hatuwezi hata siku moja kuongeza huyu sungura. Tuna mianya mingi sana ya mapato, watendaji wengi sana siyo waaminifu, ipo mianya mingi, mapato yanaingia njia ambazo siyo sahihi, kuna vitabu feki kwenye kukusanya mapato, tuna rushwa inayotumika kwenye kukusanya mapato, wafanyabiashara wengi wanatoa rushwa kwa Maafisa Biashara, hawatoi kile kinachostahili kwa Serikali, mifano ipo dhahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa kutumia Mawakala nao ni tatizo, kwa hiyo, kile kinachotakiwa kuingia Serikalini hakiingii kutokana na mifumo yetu ambayo tumejiwekea.

Suala lingine, hebu Serikali ifanye uchunguzi kwa Watumishi wa Serikali; tunavyofahamu, kila mbuzi siku hizi

anakula kwenye kamba yake. Mtumishi wa Serikali anaingia kazini, kama yuko kwenye mkondo wa mapato, ndani ya miaka miwili mwangalie utajiri wake, wana utajiri wa kutisha. Mimi nina mfano mmoja kwenye Wilaya yangu; Mtendaji wa Kata anafanya kazi ndani ya mwaka mmoja ana nyumba nzuri, ana gari, ana miradi; kwa mshahara upi?

Sasa kaangalie kwenye Majiji, watu ni mabilionea, kaangalie kwenye Manispaa, watu ni mabilionea, kaangalie kwenye Halmashauri, watu wanatembelea magari mazuri hata Mbunge ambaye anakaa miaka mitano hapa hawezi kuwa na mali kama hizo. Hebu ufanyike uchunguzi; nini kazi ya Maafisa Usalama, ni kulinda mali za Watanzania; kwa nini chache ziingie kwenye mifuko ya watu? Wametulia, wafanye uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nimeona amesema kwamba, ame-*introduce* utaratibu mpya kwa ajili ya kuainisha sehemu za mapato pamoja na kuweka utaratibu wa *e-Tax*. Naomba uharakishwe kwenye maeneo yote ya nchi hii, tuweze kubana mapato ya Serikali yapatikane. Utaratibu huo amesema unaanza kidogo sana kwenye Serikali za Mitaa. *Speed* yake ndani ya miaka mitano kwa Serikali za Mitaa 30 tu ni ndogo sana, mpaka tumalize nchi hii itakuwa ni muda mrefu. Naomba sana *speed* iendelee ili tuhakikishe kwamba, mapato yanapatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo bila ya kuendelea kutegemea wafadhili miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wengi wa Serikali yetu na hasa Watumishi wa Umma, hawawajibiki kikamilifu; hakuna nchi yoyote duniani iliyoendelea bila Watumishi kufanya kazi kwa nguvu zote na kwa uzalendo wa hali ya juu. Nchi tunazozitaja kama China na Marekani, watu wanafanya kazi masaa 24 ndiyo maana zimeendelea. Watumishi wengi wanaingia ofisini saa nne asubuhi, anazuga pale saa tano, ameshasaini anaondoka, kwa sababu ana uhakika wa mshahara mwisho wa mwezi, hana shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niishauri Serikali, mwaka jana nilishauri na leo ninashauri, tubadilishe mfumo wa ajira, tuwe na ajira za mikataba; ukimwajiri mtu kwa mkataba utampa malengo, ndani ya miaka mitano aki-*perform* vizuri unamwongezea mkataba, lakini kutakuwepo na uwajibikaji. Hawa Watumishi wa Umma sasa hivi wanajua wafanye kazi wasifanye mshahara uko pale, ni tatizo hatuwezi kupiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Tabora wanateseka sana na barabara. Tunashukuru Serikali ilikubali kuanza Miradi mitatu ya Tabora; Barabara ya Itigi - Tabora, Barabara ya Nzega - Tabora, Barabara ya Tabora - Urambo, leo hii miaka minne hata robo ya ile kazi haijafanyika. Ndani ya miaka minne hiyo, Wataalam Washauri wanalipwa bila kujali barabara imesimama au haijasimama. Ninavyoongea leo, barabara zote, Makandarasi wote wamesimama kazi kwa muda mrefu hawafanyi kazi.

Serikali inatoa fedha kidogo kidogo sana, kiasi kwamba, Makandarasi wamekwama kabisa hamna kazi inayoendelea pale. Ndani ya miaka minne hiyo, *material* yanapanda kila leo, kwa hiyo, Miradi hiyo inaongezeka gharama. Ndani ya miaka minne hiyo, kuna riba kwenye kuchelewesha kutoa fedha ya Mkandarasi, Serikali inalipa; mzigo wote huu ni hasara kwa Serikali ambapo ni Watanzania wanabebeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, fedha itoke barabara zile zikamilike. Leo ukitoka Dar es Salaam kwenda Tabora kwa njia ya basi, kulala njiani siku moja au mbili ni jambo la kawaida kabisa, mimi mwenyewe nimelala wala siyo mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Tabora wanateseka sana, tunashukuru kiwanja cha ndege kimekamilika lakini ni asilimia kidogo sana wanaoweza kutumia ndege, wengi wanatumia barabara. Tunaiomba sana Serikali itoe fedha Miradi ile ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Hansard* ya Bunge ninayo hapa ya tarehe 3 Aprili, 2011, Naibu Waziri wakati huo akiwa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, alisema ndani ya Bunge lako kwamba, barabara zote za Mkoa wa Tabora zitakamilika mapema mwaka 2013/2014. Leo tunakwenda katikati ya mwaka, robo ya kazi haijakamilika. Tunaiomba Serikali ituambie ni lini wataweza kukamilisha barabara zile, wakati miaka minne imefika, kazi haiendi na barabara hata robo ya kazi haijafanyika!

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora; yapo maeneo ya ndani ya nchi hii nadhani watumishi wanaopelekwa kule, hawajapewa semina yoyote wala hata utaratibu wa kuendesha Wananchi wao! Kwa mfano, Wilaya mpya ya Kaliuwa, Watendaji wake ninawashangaa, kuanzia Mkuu wa Wilaya, kila anayeletwa pale ni tatizo. Wananchi tunaowaongoza ni watu wenye akili, watu wenye utashi, watu wenye haki ya kuhoji chochote kinachohusu maisha yao. Kwa upande wa Wilaya ya Kaliuwa kwa hivi sasa, Viongozi hata Watendaji wa Kata, wanaitisha mkutano wa hadhara, Wananchi wanaambiwa wachange fedha za maendeleo, akiuliza tunaomba mapato na matumizi, kafanya kosa la jinai, kwa nini anauliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekubali wenyewe kwamba, tutachanga shilingi elfu kumi kumi kwa ajili ya kujenga shule, ndani ya siku mbili, tatu wanaletewa mgambo na viboko na kupigwa vibaya sana, lazima mtoe kwa nguvu. Hali ya maisha ya Wananchi wa chini tunaijua, leo hii tunawalazimisha kwa viboko tena kwa mgambo wanapigwa kwelikweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoongea sasa hivi na wewe, yupo kijana kapigwa vibaya leo ana siku tatu kwenye Kituo cha Polisi Makazi, kwa sababu alihoji kwenye mkutano wa hadhara kwamba, kwa nini hatusomewi mapato na matumizi, wakasema amewaudhi Viongozi; Utawala Bora uko wapi? Utawala Bora wa aina gani huu?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba utoe elimu kwa watendaji wako watambue Wananchi wanaowaongoza ni watu wenye utashi na utu, wana haki ya kuhoji, watimize wajibu wao, wawapeleke Wananchi kama wanapeleka watu wenye akili na siyo wendawazimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwa kutumia dakika zako kumi kama ulivyopewa. Mheshimiwa Said Nkumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Sakaya, kwa kukubali kuona kazi nzuri za Chama cha Mapinduzi zinazofanywa katika Mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Kasi ya ujenzi wa barabara itaendelea, mimi nina uhakika kabisa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alikuja, kazi kubwa sasa ni kuendelea kumalizia zile barabara ambazo zitakuwa zimebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze tu kwa kusema kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo mengi makubwa, mwenye macho haambiwi tazama. Alikuja Mheshimiwa mmoja kwenye Jimbo langu, kiongozi wa juu kabisa wa Chama kimoja sikitaji hapa, ndiyo mara yake ya kwanza kufika toka azaliwe; akafika akasema mimi toka nizaliwe ndiyo leo nafika, sasa nawashangaeni watu wa Sikonge, miaka yote 50 hii ya Uhuru mko kwenye hali mbaya namna hii.

Nikawa najiuliza huyu bwana ameenda shule au vipi; kama ni miaka yote hii wewe hujafika leo ndiyo unafika, miaka ya nyuma hiyo uliijuwaje! Mabadiliko makubwa sana yako ndani ya Tanzania hii. Serikali ya Chama cha Mapinduzi

imefanya kazi nzuri, kazi yetu Waheshimiwa Wabunge ni kuendelea kuihimiza Serikali hii iendelee kutimiza ahadi ambazo tuliwaahidi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la Watumishi kidogo hapa kwamba, zipo jitihada zimejitokeza za Walimu, naipongeza sana Serikali tumeanza kuziba mapengo, lakini tuna upungufu mkubwa sana kwenye Sekta ya Afya na vilevile Maafisa Wagani. Jambo hili ni la nchi nzima, naiomba sana Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hapa la Katiba na jambo hili ni zito, la Watanzania wote na si la Vyama vya Siasa. Wakati Mheshimiwa Rais, alipopata madaraka kwa awamu iliyofuata, alikuja hapa akatueleza anayo nia thabiti ya kuhakikisha kwamba, Watanzania itakapofika mwaka 2015, watakuwa na maandalizi makubwa ya kuwa na Katiba mpya. Wote tulifurahia na wote tuliliunga mkono jambo hili, kwa sababu baadhi ya Vyama vingine vya Siasa vilikuwa vinalalamika kwamba, Katiba iliyopo inakipendelea Chama cha Mapinduzi.

Tumekaa wote hapa na baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Siasa, hasa CHADEMA, walikuwa wanatamka hapa kwamba, wakishika nchi, siku 100 tu watahakikisha watakuwa na Katiba mpya. *(Makofi)*

Tumekwenda kwenye mchakato na ndugu zetu hawa tumeshirikiana nao hapa, maoni ya Wananchi yamekusanywa na Tume iliyoundwa na wenzetu wakapata fursa ya kwenda kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais wetu muungwana sana akawakaribisha, wamekula vitafunwa, wamepata na soda. Sasa tumeanza kusikia tena hao hao ambao tumekubaliana nao hapa, wanaanza mgogoro; mimi najiuliza wanataka kurudi tena Ikulu kwa chakula cha mchana au cha jioni? *(Makofi)*

Kwa sababu tumekaa hapa tumekubaliana na jambo hili ni la nchi, Watanzania wanalisubiri kwa hamu, kila Vyama vya Siasa, wanalisubiri kwa hamu jambo hili ili tutengeneze

mazingira tutakapoingia kwenye Uchaguzi mwaka 2015, tuingie kwenye Katiba mpya, watu wanaanza mgogoro.

Sasa mimi niwaombeni, Ikulu hamrudi tena, kitaeleweka hapahapa. Katiba hii ni ya Watanzania, siyo ya CCM, siyo ya CHADEMA, Wananchi wanaihitaji, wanaisubiri na kwa kweli katika jambo hili, naiomba Serikali msirudi nyuma, tusonge mbele kuwahakikishia Watanzania wote, mwaka 2015 tunatumia Katiba mpya, baada ya miaka 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, mimi nasema machache tu yatawatosheni. Mwisho ni suala la Ushirika. Sheria zetu za Ushirika zinatoa fursa kwa Viongozi wa Ushirika na Wanaushirika wenyewe kuamua mambo yao na yanapofika mahali kuwa mabaya, hawadhibitiani wao, lakini Wanaushirika wanageuka kuilaumu Serikali. Mimi nasema sheria zetu hizi ni vizuri sasa tukaziangalia upya; kuna udhaifu mkubwa sana, kuna wizi mkubwa sana ndani ya Vyama vyetu vya ushirika nchi nzima, lakini kwa sababu nchi nzima, lakini kwa sababu Sheria hii inawalinda, inawafunga, wao wanakaa kama wigo hivi, Serikali haipati mwanya wa kuwashughulikia hawa watu.

Sasa nataka niseme kuwa, tunayo mabadiliko, yanakuja huko ya muundo mpya wa ushirika, naomba sana Sheria yetu ya Ushirika iangalie namna gani watu watakaopata uongozi kwenye Ushirika wanawaibia Wanaushirika, wakulima wanakosa tena imani na Serikali yao, ni namna gani sasa wanadhibitiwa, ni namna gani wanachukuliwa hatua kubwa za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano hai, mimi ni mkulima wa Tumbaku, sasa kuna wengine hapa wanapiga kelele ya Tumbaku ina athari, Tumbaku ina athari. Katika jambo hili naomba tuachane, kwa sababu kila zao hapa lina athari zake. Watu mnalima miwa hapa, kwani hatujui baadhi ya miwa mingine mnatengeneza pombe haramu. Watu mnalima Korosho, watani zangu kule Kusini, lile bibo si mnatengeneza ulaka ninyi tumepiga marufuku hapa? Watu

mnalima Kahawa huko na Arusha huko, Kahawa inaleta Presha nayo, tumepiga marufuku hapa? *(Kicheko)*

Kwa hiyo, kwenye Tumbaku tuacheni, sisi Soko la Tumbaku lipo tutaendelea kulima Tumbaku. Kwanza, sisi hatuvuti Tumbaku, wale wanaonunua Tumbaku watakapoona sasa hawaihitaji, tutaacha, tutalima mazao mengine, sisi tutaendelea kulima Tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, mmeingia Mkataba na Watu wa China, soko linaongezeka, kwa hiyo, Watanzania wataendelea kupata fursa ya kuendelea kulima zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, Tabora tunalima Tumbaku lakini wapo wajanja wachache wamewaingiza mkenge Wakulima wa Tabora, wamewaletea mizigo ya madeni makubwa. Watu wa Tabora wanakopa pembejeo, pembejeo zile zinapitishwa kwenye makisio, kwenye vyama vyao vya msingi, lakini wakubwa wachache wengine wamewawekea madeni makubwa mengine ya ziada, wanaleta Makandarasi kutoka Dar es Salaam kuja Tabora kujenga Magala; Tabora hakuna Makandarasi?

Nataka niwaambie sasa na ninyi mnanisikia huko, nataka niwaambie wakulima wote wa Tabora ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa utaratibu kwenye makisio, tutalipa madeni hayo tu ambayo yamepita kwenye Vyama vyetu vya Msingi. Yale yaliyosababishwa na Viongozi, yaliyosababishwa na watu wanaotoka kwenye mabenki kutaka kuwahujumu wakulima, watayalipa wao wenyewe. Wakulima wa Tabora hatutakubali kulipia watu wachache ambao wameingia katika utaratibu wa kuwaibia Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipendi nimalize muda wangu nigongewe kegele, baada ya maneno haya, naomba niunge mkono hoja; nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Nkumba.

Mheshimiwa Neema Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Ezekiah Wenje na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa ajiandae.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mimi napenda nianze kuzungumzia suala la maji. Natambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba, kiwango cha watumiaji wa maji mijini kinaongezeka kutoka asilimia 84 mwaka 2010/11 hadi kufikia asilimia 86 mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia juhudi zinazofanywa katika utekelezaji wa kuhakikisha kwamba, suala la maji Jijini Dar es Salaam linakwisha kufikia mwaka 2014 Februari, hii ikiwa ni pamoja na kupanua mitambo ya Ruvu Chini na Ruvu Juu. Ushauri wangu kwa Serikali, isimamie kwa makini zoezi hili la kuhakikisha kwamba, maji Dar es Salaam sasa yanapatikana ifikapo mwaka huo wa 2014. Naipongeza sana Serikali yangu kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Sasa nizungumzie suala la maji vijijini; ndiyo Serikali imejitahidi kuongeza kiwango cha watumiaji maji vijijini kutoka milioni 16.3 mwaka 2006 hadi kufikia milioni 20.6 mwaka 2012. Kama tunavyojua, sehemu kubwa ya Tanzania ipo vijijini, kwa hiyo, bado kuna uhitaji mkubwa wa maji vijijini na tatizo la maji bado linaendelea kuwa kubwa. Hivyo, nilikuwa naishauri Serikali iendelee kufanyia kazi ili maji vijijini lisiwe tatizo. Mfano mdogo ninao pale Wilaya ya Wanging'ombe, kuna Kata ya Saja na Kijombe; Kata hizi mbili, vijiji vyake havina maji kabisa. Vijiji hivyo ikiwa ni pamoja na Kijombe yenyewe, Igenge, Isimike, Uhenga, Ukomora, Ryadebwe, Ryamruku, Mayala na Iyai.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ituangalie watu wa Wanging'ombe, kwa sababu maji wanayokunywa katika Kata hizi ni machafu, hayastahili

kabisa kwa afya ya Mtanzania. Halikadhalika, hali ni mbaya pale Njombe, bado tunahitaji maji, hilo nalo mtufikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la nishati, ndiyo, naishukuru Serikali yangu kwa kupunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka shilingi 385,682 hadi kufikia shilingi 150,000 kwa wakazi wa vijijini, lakini vilevile, kuna punguzo la kutoka shilingi 385,682 hadi kufikia shilingi 272,000 kwa wakazi wa mijini. Hii sasa imeleta hamasa kubwa sana kwa wakazi wa vijijini, wako tayari kuunganisha umeme, lakini kama nilivyokwambia kwamba, sehemu kubwa ya Tanzania ni vijijini na wakazi wa vijijini wanahitaji umeme pia.

Nitoe mfano mdogo tu; katika Wilaya mpya ya Wanging'ombe, kati ya vijiji 102 ni vijiji kumi tu ambavyo vina umeme. Ukitoka Kijiji cha Urembwe kwenda Kipengele, utakuta nyumba nzuri sana zimejengwa, lakini hazina umeme. Hivyo basi, naiomba Serikali, iwaangalie watu wa vijijini nao wanataka umeme katika maeneo mbalimbali.

Kuna vijiji vingi tu ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Dulami, Igagala, Igosi, Wangama, Kinenuro, Hekule, Namambegu na Iyai, vyote hivi ni Vijiji vya Wanging'ombe, naiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma iweze kuwapatia umeme, ukizingatia kwamba hii ni Wilaya mpya na pia iko katika Mkoa mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda nizungumzie suala la elimu. Natambua juhudi zilizofanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba inaboresha elimu ya msingi na hii tumeiona kutokana na ufaulu mkubwa wa watoto wanaotoka shule ya msingi kwenda sekondari. Vilevile, Serikali imeweza kujenga shule nyingi za Kata, ambazo watoto wetu sasa wanaofaulu kutoka shule za msingi wanakwenda kusoma katika sekondari hizo, lakini bado tatizo liko kubwa sana katika elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijitahidi kuziboresha Shule za Kata, kwa sababu tumeona mfano

katika mwaka 2012 matokeo ya Kidato cha Nne, hayakuwa mazuri na hii ni kwa sababu shule zile hazina walimu wa kutosha, hazina vitabu na hazina maabara. Hivyo basi, kwa upande wa Serikali nilikuwa naomba iboreshe shule hizi ili watoto waweze kufaulu vizuri.

Zamani kabla Shule za Kata hazijakuwepo, watoto hawa wenye uelewa wa kati walikuwa hawaendi shule, walikuwa wanakwenda shule za binafsi ambazo ni nzuri; kule kuna vitabu, kuna walimu, kuna maabara na ndiyo maana tulikuwa tunaona ufaulu wa watoto ulikuwa uko juu. Kitendo cha wale watoto sasa kuwa wanafaulu kwenda Shule za Kata, ndiyo maana tunaona sasa hivi matokeo yanakuwa mabaya. Halikadhalika, kwa wazazi, ninawaomba wazazi wenzangu; ule mwenendo tuliokuwa nao katika shule za awali na msingi, za kufuatilia maendeleo ya watoto uendelee na kwa shule za sekondari, tusidhani kwamba mtoto akishafika shule ya sekondari ndiyo tayari ameshakuwa mkubwa.

Vilevile, nije kwa watoto wetu; watoto wetu nao wanatakiwa wawe tayari kwa ajili ya kusoma; ndiyo, siku hizi kuna mambo mengi ya utandawazi yameingia, baba anaweza akamnunulia mtoto *ipad* au *lap top* nzuri, lakini zitumike katika masuala ya elimu, wawe wanatazama masuala ya elimu na siyo kushinda kwenye *twitter* na *facebook,* kitu ambacho wanasahau masomo yao. Hili nalo linachangia sana vijana nao wanatakiwa wabadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI. Katika utafiti uliofanywa mwaka 2011/2012 na masuala ya viashiria vya Malaria na UKIMWI, imeonesha kwamba kuna kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI kutoka 5.7% mwaka 2007/2008 hadi kufikia 5.1% mwaka 2011/2012. Ni jambo zuri, lakini bado naona kuna kundi kubwa la vijana wenye miaka kati ya 23 - 24 ambao maambukizi yao kwa upande wa wanawake ni 6.6% na kwa wavulana ni 2.8%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina wasiwasi sana hapo kwa sababu kundi hili ni kubwa, la wasichana na vijana pia, nina wasiwasi hii nguvu ya Taifa inapofikia miaka 10 au 15 mbele naona nguvukazi kubwa ya Taifa itakuwa imepotea. Hivyo basi, naiomba Serikali iliangalie kundi hili kwa umakini na kuweza kulipangia mikakati mbalimbali na kuhakikisha kwamba, maambukizi haya hayaji tena kuwa maambukizi mapya. Vilevile, *TACAIDS* kama *TACAIDS,* naomba waniambie wana mikakati gani katika kuhakikisha kwamba, wanalifikia kundi hili la vijana ambao wana miaka 23 - 24 kwa kuwa maambukizi makubwa yapo katika kundi hili la vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kule Njombe hali ni mbaya; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba Mkoa ule unashughulikiwa ipasavyo katika suala hili na *TACAIDS* nao wana mikakati gani na Mkoa ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala la afya ya mtoto na mama. Katika afya ya mtoto, napenda niipongeze Serikali yangu kwa kupunguza vifo vya watoto wachanga. Japokuwa kuna watu hawalioni hilo lakini mimi nimeliona na watu wengine wengine pia wanajua kwamba vifo vya watoto wachanga sasa hivi vimepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spoika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya. Mheshimiwa Profesa Msolla.

**MHE. NEEMA H. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru. Mheshimiwa Prof. Peter Msolla.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nianze kuzungumzia juu ya usalama wa chakula. Tanzania tuna bahati ya kuwa na eneo kubwa, takriban hekta milioni 44, zinazofaa kwa kilimo, lakini vilevile tunazo hekta karibu milioni 29.4 ambazo zinafaa kwa umwagiliaji. Serikali yetu ilikuja na mpango kabambe wa azma ya KILIMO KWANZA na kule kumewekwa malengo tofauti. Lengo mojawapo lilikuwa ni kuongeza bajeti kwa ajili ya umwagiliaji, kwa kutambua kwamba kilimo cha umwagiliaji ndiyo chenye uhakika, kwamba, itaongeza bajeti ya umwagiliaji ili ifikapo mwaka 2015 tuweze kuwa na hekta milioni saba tunazomwagilia, lakini leo hii tuna hekta 370,000 tu, hatujafikia hata asilimia moja.

Sasa kutoka tarehe 3 Agosti, 2009 mpaka leo hii, tungependa kujua ni mikakati gani inayochukuliwa ili tuweze kufikia azma hiyo ifikapo mwaka 2015. Vilevile, Serikali iliahidi kwamba, itaanzisha Mfuko Maalumu kwa ajili ya KILIMO KWANZA, hili nalo limefikia wapi? Iliagiza vilevile kwamba, itaanzisha Wakala wa Taifa wa Umwagiliaji Nchini, yaani *National Irrigation Agency,* tungependa kufahamu mikakati yake inakwendaje kwa sababu kuna maeneo mengi yanayofaa kwa umwagiliaji. Nikizungumzia juu ya Kilolo, tuna maeneo mengi ya Bonde la Mahenge, Ruaha Mbuyuni, iko Nyanzwa na maeneo mbalimbali, ambayo yanafaa sana kwa ajili ya umwagiliaji lakini hayajaweza kufanyiwa kazi.

Jambo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, katika Dira yetu ya Taifa kufikia mwaka 2025, Serikali imelenga Tanzania iwe ni nchi yenye uchumi wa kati tufikapo wakati huo na kwamba, itategemea zaidi viwanda kuliko kilimo. Wananchi wengi wameitikia kuanzisha viwanda vidogovidogo na moja ya viwanda ambavyo navifahamu ni viwanda vya kutengeneza madawa ya wanadamu na vilevile ya mifugo; lakini watu hawa wanapata shida sana kwa sababu mahitaji yao ya viwanda hivyo, baadhi yao wanahitaji malighafi kutoka nje. Wakileta malighafi kutoka

nje wanatoza ushuru wa thamani, yaani *VAT* na vilevile *Import Duty* na wakileta hapa hiyo gharama inamwendea zaidi mtumiaji wa mwisho. Mtu anayeleta dawa hiyohiyo iliyotengenezwa ng'ambo, inaingizwa hapa nchini, haitozwi kodi yoyote na yeye anakuja hapa anauza moja kwa moja. Sasa tunawasaidiaje Wananchi wetu ambao wamejitolea na kuingia katika upande huo? Tungeomba kodi hizo ziondolewe ili ziwe *zero rated,* wanufaike zaidi Wananchi ambao ndiyo wanufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni hili ambalo linahusu utoaji wa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri, wengi wameshalizungumza. Tulisikia kwenye hotuba kwamba, wale watakaopata Hati Chafu watapewa 25% ya fedha za maendeleo. Sasa jambo la kujiuliza; unayemwadhibu ni nani? Unaowaadhibu ni Wananchi wenyewe ambao wanahitaji haya maendeleo na kwa sehemu kubwa wanakuwa wamejitolea vilevile; kwa nini asiadhibiwe yule ambaye ni mhusika au mtendaji badala ya kuiadhibu Halmashauri yenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Serikali ingeangalia Watendaji katika Halmashauri zetu, watazame uwezo wao kwa sababu baadhi ya Wilaya, kwa mfano, Kilolo ni Wilaya ambayo si ya siku nyingi, bado ni mpya na kati ya mwaka jana na sasa Watumishi wa Halmashauri kumi wamehamishwa; saba wamepelekwa Njombe, wengine wamepelekwa Mpwapwa na wengine wamekwenda Kilosa. Unawaondoa watu ambao tayari wamakwishaanza kuzoea na wakati huohuo vibali vya ajira havitolewi, tunategemea ufanisi wao wa kazi utakuwaje kama kila siku tunaleta mtu mpya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya elimu, kwanza, niipongeze sana Serikali kwa kuwekeza zaidi kwenye elimu, yaani *investing in human brain*. Hakuna nchi yoyote Duniani ambayo imeendelea bila kuwekeza zaidi kwenye elimu. Kutokana na Mpango wa MMEM na Mpango wa MMES, idadi ya wanafunzi wanaoingia mashuleni katika

ngazi zote iwe shule ya msingi au sekondari, kwa kweli imeongezeka sana.

Mipango hii miwili imesaidia sana kuongeza idadi ya wanafunzi hata kufikia Elimu ya Juu, lakini huku kuna MMEM na hapa pana MMES, ukifika juu huku hakuna Mpango kamili. Kulikuwepo Mpango wa MMEJU, yaani Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu na Ufundi, tunahitaji uwapo wa namna hiyo; Mpango huo utatekelezwa lini na ulikwishasomwa hapa ndani ya Bunge hili kwamba jamani tuwe na Mpango huko juu. Kubwa zaidi, elimu inaanzia na mwalimu, maana kule ndiko tunakokabidhi watoto wetu. Ubora wa walimu tulionao hasa hii miaka ya karibuni kwa kweli inatia shaka, kwanza, utaratibu wa kuwasajili hawa walimu *(recruitment)* ni kwamba, utachagua wale wengine wote wanaokwenda sekondari na sehemu nyingine, lakini huyu anayebakia hapa chini ambaye ufaulu wake siyo mzuri, yeye ndiyo unamwambia nenda kwenye kozi ya ualimu! Mimi nafikiri huu siyo utaratibu mzuri. Sasa tunakabidhi watoto wetu kwa watu ambao uwezo wao ni mdogo. Mimi nashauri kwamba, hii Sekta ya Ualimu ipewe umuhimu unaostahili ili uweze kuvutia watu wengi zaidi, vijana wenye uwezo zaidi wajiunge kwenye huu ualimu. Pia mishahara iwe bora zaidi ili tuweze kupata wenye uwezo; vinginevyo, tunakabidhi watoto wetu kwenye mikono ambayo uwezo wao pamoja na upungufu mwingine, unazidi kuwa mdogo.

Naomba nitoe mfano; Finland na Singapore na kuna nchi nyingine, kuingia kusomea ualimu ni ngumu zaidi kuliko kuingia kusomea udaktari wa mwanadamu, kwa sababu kule unatakiwa uwe *top notch* na mishahara yao ni mizuri. Sisi tumegeuza, kwa hiyo, ubora wa vijana wetu hauwezi kuwa mzuri kiasi hicho. Nashauri Serikali yetu iliangalie hili ili tuweze kupata vijana wengi zaidi. Baya zaidi, katika upande wa sayansi, vijana ambao wanaingia kwenye masomo ya sayansi ni wachache sana ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Peter Msolla.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na ninakushukuru sana. Mheshimiwa Ezekiah Wenje, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, kwa dakika tano tano.

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kwenye Bunge hili, Wabunge tulifanya kitu kinaitwa *Mob Justice,* tulipokuwa tunashughulikia suala la Mheshimiwa Maige, kwa sababu tu Wizara yake ilionekana kwamba wamepoteza Twiga wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kwa kusema kwamba, Duniani hapa tunaangalia *opportunity cost;* thamani ya Twiga wawili ukipeleka kwenye soko, watakuwa sana na shilingi milioni mia moja. Wanafunzi 360,000 wa Tanzania waliopata *zero* thamani yao ni kubwa kuliko Twiga wawili waliopotea. Leo watu wanashangaa kwa nini Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri Shukuru Kawambwa, ajiuzulu.

Kama tulimwadhibisha Mheshimiwa Maige kwa sababu ya Twiga wawili, tukamwajibisha Mheshimiwa Chami kwa sababu ya *TBS,* sijui magari yamepimwa hovyohovyo huko nje ambapo thamani yake ukiikadiria haivuki shilingi milioni 200; leo tunakataa tena ninyi mnaunga mkono kwamba mnashangaa kwa nini Mheshimiwa Mbowe kwenye *speech* yake anataka Mheshimiwa Shukuru Kawambwa ajiuzulu! Yaani hao Twiga wawili wana thamani kuliko watoto wa Tanzania 360,000 ambao wamefeli na hatima yao mpaka sasa haijulikani; na ndiyo maana *this is pathetic;* yaani kuna

Mzee mmoja anaitwa Mheshimiwa Chiligati, hawa ndiyo waliowahi kuwa Mawaziri, alipokuwa anazungumza hapa alisema kwamba, yeye analinganisha ubora wa elimu, yaani kwake ubora wa elimu ni wingi wa madarasa, bila kuangalia *output* inayotoka kwenye hayo madarasa. Baraza la Mawaziri ndiyo *think tank,* hii ndiyo *engine* inayoendesha hii nchi; sasa kama nchi ilikuwa inaendeshwa na watu kama hawa ndiyo maana leo tupo kwenye hii *mess* tuliyonayo leo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikwambie kwamba, hali ya elimu kwenye nchi hii ni *pathetic*, watoto wanakaa chini kwenye shule zote ndani ya miaka 50 ya Uhuru kwenye nchi ambayo imejaa misitu ambayo inatoa mbao mpaka mbao nyingine mnasafirisha kupeleka nje, lakini watoto wanakaa chini! Ndiyo maana tunazungumza na ninyi ndiyo mnatupa hoja za kuzungumza, kwa sababu mmefumbia macho matatizo ya msingi ya Watanzania, ndiyo maana tunasema leo kwa mfano nauli za daladala zimepanda kwa sababu gharama ya kuendesha shughuli ya daladala iko juu, kwa sababu vipuri vyote vya magari wana-*import* kutoka nje. Pesa ya Watanzania thamani yake inashuka *against dollar;* kwa hiyo, unapoingiza vipuri ni lazima bei iende juu. Kwa hiyo, gharama ya kuendesha shughuli za daladala zinapanda kwa sababu pesa imeshuka thamani, hii haihitaji *magic*. *(Makofi*)

Halafu Mheshimiwa rafiki yangu Bwana Lusinde anasema, namna ya kupeleka thamani ya pesa ya Tanzania ni kuweka picha ya Nyerere, halafu Mawaziri wanapiga makofi. Sasa, yaani ninyi mmeruhusu nchi hii, ndiyo maana rafiki yangu Mheshimiwa Msigwa anasema, ninyi mmeruhusu akili ndogo kutawala akili kubwa kwenye nchi hii na ndiyo maana tupo hapa. Sasa kama mko hapa mnapigianapigiana makofi wakati hii nchi ipo kwenye mess, *this is pathetic! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nadiriki kusema kwamba, mmetuweka katika *state* ambayo *this Government I can really say, I can dare say and I want to go into history that I have said; the Government is impotent, it is*

*incompetent and it is governed by the lord of others! (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hivi; kwenye haya Mabaraza ya Katiba, ukisoma *speech* ya Mheshimiwa Mbowe imejaa *solutions* nyingi tu, nyingi tu zimejaa, kwa sababu ya *narrow interpretation* ya watu wengine wanasema eti hii tunalalamika. Tumeshawashauri mara nyingi mpaka tumechoka, kama hamsikii mmeshauriwa kwa miaka 50 bado nchi inapiga hapo *mark time,* sasa tuwafanyeje? Yaani ninyi mnataka tuje hapa tuwapongeze kwa kuiumiza nchi! Haya, ngoja niwape mfano mwingine, hapa walisema kwamba ... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, dakika zako zimeshakwisha. Mheshimiwa Msigwa, dakika tano.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na leo naomba nianze kwa kunukuu Maandiko Matakatifu katika Kitabu cha *Proverb* au Mithali 27:22 cha Mfalme Suleiman, anasema: “Mpumbavu hata ukitwanga upumbavu wake kwenye kinu pamoja na ngano upumbavu wake hautamtoka na mlango wa 26 *Proverb* hiyo hiyo anasema; mpumbavu hastahili heshima.”

Nataka nitoe rai kwa Watanzania ambao mlituchagua kwa kura nyingi tuje katika Bunge hili, tusimamie fedha ambayo ni kodi yenu. Ninataka niseme, kwa sababu ya dakika chache tu kwa sababu mtu ana cheo, ambayo ni dhana ya Kiafrika, tu kwa sababu mtu ana cheo; anaweza akawa Mbunge, Diwani, Waziri au wa cheo chochote, haimaanishi kwamba ana akili iliyo nzuri. *Crown does not change your mind*, kama umepata cheo huna ufahamu mzuri, unabaki kuwa huna ufahamu mzuri pamoja na cheo chako. *(Makofi)*

Watanzania wote mnaonisikia kupitia Bunge hili, nchi hii siyo mali ya wanasiasa, kukaa mbali kuwaachia wanasiasa tu kwa sababu wana vyeo ndiyo mahali ambapo tumefika. Taifa hili linapozungumza Walimu wanalalamika, dawa

hakuna hospitali, madawati hakuna, maji hakuna, elimu dhaifu, barabara mbovu, asilimia 89 ya shule za Tanzania hazina vyoo, watu wanashindwa mahali pa kujisaidia. Asilimia 14 ya Watanzania (Watanzania milioni 6.3), hawana vyoo wanajisaidia porini.

Leo ninapozungumza, misitu kwa siku moja inakatwa hekta 349.5, yaani hekta zaidi ya 800 zinateketea, halafu tunakaa hapa, kuna watu *the so called the first class economist,* wanapuuza maneno yenye hekima ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, *they just cannot see!* Watanganyika tusidanganyike eti kwa sababu watu wana vyeo, maana yake wana *sound mind.* Mtu anaweza akawa na vyeo, lakini kichwani kama Biblia jinsi inavyosema, umejaa upumbavu na mpumbavu hata ukitwanga kwenye kinu upumbavu wake hauwezi kutoka. Miaka miwili tumezungumza Tanzania ni Taifa la pekee ambalo akili ndogo inatawala akili kubwa; *when are we going to change?* Tunaridhia tu mambo madogomadogo, Bunge lina kazi ya kuchunguza watu wanapeana mimba saa ngapi? *Is this our job* wakati Watanzania wako kwenye *mess* namna hii?

Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana nilikuuliza swali kwamba nchi hii kuna udini, Zanzibar wanalazimisha watu wafunge. Ulinijibu swali kisiasa hapa, leo watu wanauana halafu tunaita Wachungaji wakae kwa kuwa mmekuwa mkiwaita mnawapa chai na maandazi, wanataka chai na maandazi? Wanataka amani!

Jana kuna mtu amekamatwa Kanisani Anglikana ana *machine gun* na risasi 28; haya hayazungumzwi, tunaacha kuzungumza mambo ya msingi kama watu tuliokomaa, Watanzania wametuamini, tunaleta ngonjera na mambo ya ajabuajabu katika nyumba hii, halafu tunasingiziana vitu vya ajabuajabu, tunakula kodi za Watanzania; *why*? Kwa nini hatuwahurumii Watanzania? *(Makofi)*

Wakazi wa Iringa jana nilikuwa naongea na ninyi, haya ndiyo nimekuja kuzungumza mnisikilize. Serikali haitaki kutusikiliza, tunaacha kupanga tujue tunatokaje katika

matatizo haya, wazee mliwaahidi watakuwa na dirisha la bure, hakuna dawa. Akina mama wajawazito kwamba dawa zipo hospitalini, wakienda hakuna dawa. Badala ya kujadiliana haya mambo, tunaanza ngojera na kulaumiana kama Watanzania; *why? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Msigwa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa na kwa heshima ya makuzi na malezi niliyolelewa, nimeshindwa kumzuia kwa sababu sikulelewa hivyo, nilifikiri lazima amalize *speech*. Nataka kusema tu, na hii nataka kuweka rekodi kama taarifa kwamba, *speech*, kanuni hiyo ya taarifa kwani huijui! *Speeches* zote mbili zimekiuka Kanuni ya Bunge. Kama Mheshimiwa Juma Nkamia aliweza kufuta neno lile, maneno kama haya ya wapumbavu siyo maneno ya kiungwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema nimeweka tu rekodi kama taarifa na wewe unajua kwamba, waliotakiwa kusema leo ni Mheshimiwa Matiku na mwingine, wamewaachia hawa waseme waliyoyasema, kwa sababu wana ujuzi wa kusema hayo waliyoyasema. Kwa hiyo, nasema nimeweka rekodi kwamba, lugha aliyoitumia Mheshimiwa Msigwa siyo ya Kibunge. Siyo *Bible?*

Nasema tu lugha ya matusi, Mheshimiwa Naibu Spika, ni pande zote, hii lugha haikubaliki. Nilitaka ajue hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Kama nilivyowaomba asubuhi kwamba, nina orodha kubwa ya wachangiaji, nisingependa tuchukue muda sana. Kwa kweli na mimi nimevumilia kwa shida kidogo na nilitaka wale ambao wanalalamikia kiti kila wakati kwamba kina upendeleo, waone jinsi ambavyo sijamwingilia Mbunge mwingine yeyote katika maneno kwamba, akili ndogo inatawala akili kubwa, wakati hawa waliochaguliwa wamechaguliwa na Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Maneno kama *this government is impotent;* kuwaita watu wazima ni *impotent,* sijui kama ni maneno ya kiungwana! Kuwaita watu wengine wapumbavu, yaani unapokuwa umelalamika ni vizuri uwe unapima vilevile upande wako. Nia yangu siyo kupoteza muda, Mheshimiwa Anna Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Mtanda.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naomba niunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Nataka nianze na maneno ambayo huenda ikawa msemaji wa mwisho kwa kuwa yeye ni *Reverend* anayajua vizuri zaidi, lakini niweke pia na nukuu aliyoisema Mheshimiwa Mbilinyi, kwa kunukuu maneno vilevile ya Maandiko Matakatifu yanayohusu mwanamke mpumbavu. Niseme hivi; wote sisi tunayajua hayo maandiko, lakini maneno haya ya kusema mwanamke mpumbavu hayasemwi kwenye siasa na wala hayana uhusiano na siasa, maneno haya yanasemwa Kanisani wakati wa kumfunda mwanamke ambaye anaolewa au anaenda kwenye *kitchen party* akayaseme hayo, lakini kwenye siasa siyo mahali pake. *(Makofi)*

Mimi naomba niwaombe akina mama, tusikubali kudhalilishwa, iwe kwa neno la Mungu au la kisiasa. Kumwita mwanamke mpumbavu popote alipo, nataka niwaombe Wanawake wa Mbeya na wa Iringa kwamba mnaambiwa wapumbavu, ndiyo, na naomba kabisa vyama vyote, mtindo wa kutumia majukwaa kuwakashifu wanawake uachwe na ukome kabisa. (*Makofi*)

Hapa nataka nilisemee hili la kuwaita wanawake wapumbavu, eti kwa sababu Biblia imesema hivyo; sijui alikuwa anawasema wanawake wa wapi hao wapumbavu, kwa sababu wako wanawake kwenye vyama vyote ndiyo mnawaita wapumbavu? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili hata lile alilokuwa amelisema Mheshimiwa Lusinde mimi sikulifurahia,

la Mbunge mimba isiyotarajiwa sikulipenda. Nilifurahi sana Mheshimiwa Sakaya aliposema anaomba uthibitisho wa hilo, lakini sasa sielewi kwa nini Mheshimiwa Sakaya akaliondoa. Kama wapo wanawake hasa Wabunge wanaopata mimba bila kutarajia, nasema hili siyo jambo jema kwa sababu sisi ni watu wazima na kama tupo wa namna hiyo humu ndani, basi hatuna mamlaka ya kuwasema wasichana wadogo wanaopata mimba. Hatutakuwa na mamlaka yoyote. *(Makofi)*

Linalonisikitisha ni kwamba, mwanamke anaposemwa iwe kwa chama chochote tunapiga makofi. Niliwaona wanawake wanamshangilia Mheshimiwa Mbilinyi, niliwaona wanawake wanamshangilia Mheshimiwa Lusinde, nasema kwa wanawake ni aibu kubwa. Mwanamke mwenzako anapotukanwa siyo wakati wa wewe kushangilia. Lazima tulipige vita hili, hatuwezi kuliendekeza. Kuanzia leo nimewaambia kwenye Sekretarieti yetu ya Ulingo kwamba, tutasikiliza maneno yote, majukwaa yote, kama kuna mtu atakashifu mwanamke, tutakwenda wanawake katika maeneo hayo kupiga debe kwamba hamstahili kura zetu. Tunaomba heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu maandamano ndani ya nchi hii. Naomba Serikali iweke utaratibu, hata kama ni haki, haiwezekani mtu anapoamua maandamano ayafanye siku anayotaka yeye na saa anayotaka yeye. Lazima tuwe na utaratibu wa maandamano, siku maalum na mahali maalum, siyo mahali popote, lazima utaratibu huo uwepo. Watu wanafanya kazi Jumatatu mpaka Jumamosi, kama wanataka kuandamana lazima kuwe na utaratibu, ama maandamano yawe Jumamosi au Jumapili, au kama watu wanataka kufanya siku ya sikuu wafanye, lakini tuwaache Watanzania wafanye kazi katika nchi hii. Haifai kila siku tunakuwa na maandamano popote. *(Makofi)*

Hata yale maandamano wanayotaka ya kumwambia Mheshimiwa Kawambwa ajiuzulu, nani kakukataza kusema? Sema, lakini kusema mtafanya

maandamano nchi nzima, watu waache kazi kwa ajili hiyo, waende mahali palipoandaliwa wakayaseme hayo watasikilizwa tu, lakini siyo hili la kila siku maandamano, maandamano, maana sasa linakuwa kama ni tishio tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, Serikali iliamua kufunga shule zile za bweni za *Form One* mpaka *Form Four* ili shule ziwe za *Form Five* na *Six. Masasi Girls* ni mojawapo; Shule hii ilikuwa inachukua wasichana 600 wa *Form One* mpaka *Form Four*, leo mmeweka *Form Five* na *Six* wanafunzi 90 tu. *Dormitories* zote ni nyumba za popo, panya na buibui, huu ni ubadhirifu na kutuonea watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mimi sitaki kusemea juu ya gesi, lakini hili la kufunga shule ambazo zilikuwa zinachukua wasichana wa mkoa ule ambazo ni *Masasi Girls* na *Mtwara Girls,* mmezifunga, wasichana waliopo pale ni wachache, ni *wastage*. Pale pana nyumba za walimu za kutosha, mabweni ya kutosha, sasa leo *Masasi Girls* ina wanafunzi 90 kati ya 600; kwa kweli ni jambo la ajabu sana. Sisi ndiyo palikuwa mahali tunapopeleka wasichana wakakae kwenye bweni, sasa hatukatai kwamba mfungue *Form Five* na *Six*, lakini muweke *Form One* mpaka *Six*. Mnakwenda kufunga mahali ambapo shule zenyewe za sekondari hata za binafsi hazipo! Huu ni uonevu, tunaomba hilo jambo mlisahihishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia suala la matumizi ya nyenzo za Umma. Tunayo matatizo makubwa sana katika nchi, kila Wizara, wote wanataka kutafuta nyenzo. Ziko nyenzo ambazo tungeweza kuzitumia kwa pamoja; mfano, kama tunataka kufanya *patrol* baharini ama ziwani, siyo lazima watu wa uvuvi wawe na boti yao, siyo lazima jeshi wawe na boti yao, siyo lazima na watu wa *immigration* wawe na boti yao. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiwa ndiyo Kiongozi wa Serikali, wakalishe watu tutumie rasilimali zilizopo kwa pamoja, kwa sababu huu mtindo wa kila mmoja anaagiza anachokitaka yeye ili akitumie mahali pamoja, mwisho sisi wenyewe kwa wenyewe

tutagongana humo baharini. Kwa hiyo, ninaomba sana kuwe na matumizi mazuri ya vifaa vya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, ni kutoitendea haki nchi, kuwa na viporo vingi; mfano, ni yale Makao Makuu ya Zimamoto, sasa ni miaka mitatu sijui mitano, haiishi, mwaka huu pia hawakupata fedha. Tunaomba sana, tumalize viporo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema, tumalize viporo kabla hatujaanza vingine. Tunaomba kuona viporo vyote vinamalizika. *(Makofi)*

Kuhusu ukurasa wa 27 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi nilichokielewa ni kwamba, zile shilingi bilioni 440 ni Mradi mzima wa kuwezesha familia maskini. Ndivyo nilivyoelewa na kwamba tumeanzia kuzitambua hizo familia Bagamoyo, lakini itakapofika Januari, 2014 kaya zote katika nchi nzima zitakuwa zimetambuliwa. Ndivyo nilivyoelewa mimi; sikuelewa kabisa kwamba, fedha hizi zinakwenda Bagamoyo, sijui labda sikuelewa vizuri; lakini hapo hapo hivi mpango huu unawahusishaje wazee? Tusisahau kwamba, ninyi ndiyo vijana leo ambao mnaweza mkapanga ratiba zote za kuwanusuru wazee, baada ya miaka kadhaa mtakuwa wazee. Mtakuja kujuta kama hamtaweka utaratibu wa kuwaenzi wazee wa nchi hii, kwa sababu uzee siyo ajali. Kwa hiyo, kama Serikali imefikiria kuzifikiria familia ambazo ni maskini, ninawaomba sana sana, muwafikirie pia wazee wa nchi hii ambao siyo wengi, wanajulikana, nao wapate chochote. Hata wale ambao walikuwa siyo wafanyakazi, lazima muwafikirie wazee wote kwa pamoja, wameitumikia nchi hii, wamelilea Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tena kwamba, naomba sana ndani ya Bunge hili, maneno yasiyokuwa ya heshima, kama mnataka kutukanana wenyewe kwa wenyewe tukananeni, lakini mimi nakataa kabisa maneno yasiyo ya heshima kuelekezwa kwa wanawake. Nasema iwe mwisho na tutachukua hatua. Kwa hili, nawasemea wanawake wote, wa vyama vyote na wa nchi hii popote walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi niliyoipata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, kwa wosia wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Khaji na Mheshimiwa Muhammad Chomboh ajiandae.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia mada hii.

Naomba nianze kwa kuwakumbusha wenzangu katika Bunge hili kwamba, pale Misri tunaye Kiongozi wa Serikali sasa hivi Mheshimiwa Mohammed Morsi, ambaye alitumia muda mwingi sana kuwashawishi Wananchi kuandamana na hatimaye kuuondoa Utawala wa Hosni Mubarak; lakini Wananchi walewale ambao walifunzwa tabia ile ya maandamano, leo wamegeuka na wanataka Mohammed Morsi aondoke madarakani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukifikiri kwamba leo unafanya hivi kwa sababu Serikali ya CCM ipo madarakani, ujiandae na wewe kwenye Serikali yako ya njonzi itakapofika kwamba utashughulikiwa kwa mtindo ule ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisijiondoe kwenye hoja zangu za msingi. Ninaomba kwanza nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kwa kutoa msaada mkubwa sana katika hospitali yetu ya Mkoa wa Lindi. Nilikuwa naamini Mbunge mwenzangu kutoka Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Salum Barwany, aliposimama hapa angetoa shukrani zetu kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Lindi, lakini ninaamini alighafilika. Kwa hiyo, ninamshukuru sana kwa kutoa vifaa vyenye thamani ya *billions of money* kwa hospitali ya Mkoa wa Lindi na sasa tatizo kubwa la vifaa limepungua Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kutoa tani 161 za msaada wa chakula kwa wapiga kura wa Jimbo langu na kunusuru maisha ya Wananchi wa Kitongoji cha Mkalimbe na Kata ya Kilangala kwa ujumla. Hoja yangu ya msingi hapa ni kwamba, Wananchi wa Wilaya ya Lindi wanao uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula endapo watawezeshwa. Endapo Serikali itajikita kufuatilia maombi ambayo tumeyaleta pale TAMISEMI ya kutenga shilingi milioni 560 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Kinyope ili tuweze kuongeza Mradi ule wa kilimo tuweze kulima ekari zaidi ya 600 badala ya 225 za hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuliomba Bonde la Narunyu liweze kutengewa shilingi milioni 750 ili tuweze kuzalisha kwa sababu ni fedheha kwa Wananchi wa Mkoa wa Lindi. Wananchi wa Mkoa wa Lindi wanayo mabonde mengi, tunaweza kuzalisha chakula cha kutosha na tusitegemee msaada wa mahindi ya njaa kutoka Serikalini.

Bajeti hii hapa, fedha za maendeleo kwenye wilaya yangu imetengwa shilingi 1,885,433,000, haiwezi kutosha kwa sababu zinaweza kutumika kwa kilimo katika Bonde la Narunyu na Kinyope peke yake. Ninaiomba Serikali izingatie hili. *(Makofi)*

Tunayo mabonde mengine, Mto wa Longa, Nyengedi, Utimbe, Mahiwa, haya ni mabonde ambayo yanaweza kutuondoa kwenye tatizo la njaa badala ya kutumia fedha nyingi kutoa chakula kutoka kule Peramiho. Tumetumia fedha nyingi sana kusafirisha kile chakula kutoka Songea. Tupewe fedha zile tuzalishe kwenye mabonde haya. Hilo namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili kuhusu zao la korosho na namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameelezea katika ukurasa wa 31 na 32 wa Hotuba yake kwamba ni vizuri sasa Serikali na mimi ninaunga mkono na Waheshimiwa Wabunge muunge mkono jambo hili, kuanzishwa kwa ule Mfuko Maalum *(Price Stabilization Fund),* kwa sababu Zao la Korosho limekuwa likisuasua katika bei yake mwaka hadi

mwaka; ninafikiri ni lazima Serikali ilete *compensation* kwa sababu Vyama vya Msingi 14 katika Wilaya ya Lindi vimekopesha korosho, Serikali tunawadai shilingi bilioni 1.2. Ninaomba sasa kupitia uanzishwaji wa Mfuko huu, tuweze kupewa hii shilingi bilioni 1.2 kwa Vyama vya Msingi 14 ili waweze kulipa Wakulima wa Kijiweni, Mvuleni na maeneo yote ya Wilaya ya Lindi, ambao wanavidai Vyama hivi vya Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna suala la barabara; niliwahi kuuliza swali Bungeni na Serikali ilikubali maombi yetu kwamba, tupewe shilingi milioni 380 ili tuweze kutengeneza Barabara ya Mchinga kwenda Mvuleni kwa sababu eneo lile la Bamvua hapapitiki na Serikali ilikubali maombi haya. Sasa nataka tuyaone kwenye bajeti yako wapi ili Wananchi wa maeneo haya waweze kuwa na uhakika kwamba daraja lile ambalo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, awamu hii inatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Nachui, Mheshimiwa Mbunge Membe alitoa shilingi milioni 65, tuliomba Serikalini tupewe milioni 200 ili Daraja lile liweze kujengwa kwa sababu sasa limejengwa nusu halipitiki. Sasa tunaomba Serikali muunge mkono juhudi za Mheshimiwa Mbunge ili Daraja la Nachui liweze kupitika. *(Makofi)*

Maeneo mengine kama vile Barabara ya Nangalu, Barabara ya Mipingo, tunaomba Serikali kupitia Mfuko huu wa Barabara itenge fedha ili tuweze kuboresha barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda haraka haraka ili kwenda na wakati. Tumezungumzia kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Mimi nina imani kubwa kila Mbunge akisimama tunalo tatizo la ardhi, tuna tatizo maeneo yetu ya nchi hayajapimwa. Ufumbuzi wa jambo hili ni kuanzisha *satellite city,* tuwe na *satellite city* ambayo hawa watu wa ramani wanahitaji shilingi bilioni 15 ili ardhi ya nchi yetu ipimwe kwa njia ya *satellite* ili wananchi wote waweze kumiliki hati

za ardhi na waweze kuzitumia hati hizo kama dhamana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaomba Serikali ijielekeze kutekeleza mpango wa kuwa na *satellite city* hapa Dodoma ili ardhi ya nchi hii iweze kupimwa na ili tuweze kulinda mipaka yetu kwa njia ya *satellite* tuweze kuwa na hali bora ya ulinzi na usalama. Tutakuwa tumemaliza kabisa tatizo hili, tutakuwa tumemaliza migogoro ya ardhi ya wafugaji na wakulima. Wananchi wetu watakuwa na uwezo wa kuwa na hati ili waweze kukopesheka kwenye mabenki. Hili ni jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tukizungumzia hapa Miradi ile mitano ya *World Bank.* Ninashukuru baada ya usimamizi na ufuatiliaji mkubwa, sasa hivi Mradi ule wa Maji wa Namkongo unakwenda vizuri. *(Makofi)*

Shilingi milioni 182, *World Bank* wametupa fedha tunaendelea. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali, lakini naomba mkandarasi yule afanye kazi hii kwa uhodari mkubwa na tarehe 23 nitakwenda kuangalia Mradi ule, kama bado unasuasua unaenda kwa mwendo wa konokono, basi tutabanana ili mambo yaeleweke.

Ninaiomba sasa Serikali, Miradi hii kwenye Vijiji vya Nyangamara ‘A’, Wananchi walichangishwa shilingi milioni moja, Mbunge wao Mheshimiwa Membe, alitoa shilingi milioni 15. Nyangamara ‘B’, Wananchi walichangishwa shilingi milioni moja, Mbunge akachangia milioni 12. Kijiji cha Litipu walitoa shilingi 700,000, Mbunge amechangia shilingi milioni nane kwenye Miradi hii, lakini toka Mbunge amechangia na Wananchi wamechangia, hawaelewi fedha yao iko wapi. Tunaomba sasa Serikali ijielekeze kutatua tatizo la maji Nyangamara ‘A’, Nyamangara ‘B’, Litipu na Londo Mnara; hayo ni mambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa mawasiliano nchini. Bunge lililopita tulijadili humu na Waheshimiwa Wabunge tukilifanyia masihara jambo hili litatuondoa

madarakani. Litatuondoa kwenye Majimbo yetu, kwa sababu tulikubaliana kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote *(UCAF),* hadi leo hii bado Mradi huu hatuelewi umeishia wapi na kuna mikakati gani. Kwa hiyo, ninaomba kwa kuwa mliahidi ndani ya Bunge hili lazima mtueleze, Wananchi wa Mipingo mnara wao wataupata lini, Wananchi wa Rutamba wataupata lini, Wananchi wa Kilolabwani wataupata lini. Pia, Kijiji cha Chiponda, Miima, Mandwanga, Naukauka, Nachunyu na Navanga, wana haki ya kupata mawasiliano na Bunge hili tuliridhia kwamba sasa tuondoe tatizo la mawasiliano vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie pensheni kwa wazee.

*(Hapa kengele pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Nitaunga mkono hoja baada ya kupata ufafanuzi wa haya niliyoyasema.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Chomboh.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia jioni hii kupata fursa ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa 56 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo hapa amezungumzia suala la bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna budi wote kuishukuru Serikali ya China, kwa msaada wao wa kutujengea au azma ya kutujengea Bandari ya Bagamoyo. Kwa kweli ni

jambo zuri na ni jambo ambalo inabidi tushukuru kwa sababu mja asipomshukuru mja mwenzie, hata Mungu hatamshukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzuri na neema hii ambayo tumeipata, lakini hapa kidogo nina jambo nami ninataka kusema kuhusu Bandari ya Mwambani Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakukuzungumzwa lolote kuhusiana na Bandari ya Mwambani Tanga, ambayo kwenye mipango mingi ilikuwa tayari ni bandari iliyokuwa inangojea muda wake wa kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Tanga walikuwa na matumaini makubwa sana na tamaa waliyopewa na Serikali hii ya CCM kwamba, Bandari ya Mwambani Tanga ingeweza kujengwa katika kipindi cha mwaka huu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalazimika kusema hili kutokana na kauli kinzani za Watendaji Wakuu wa Wizara hii, ambao wamekuwa wakizitoa za kusema kuhusu Bandari ya Tanga, Wananchi sasa wamekuwa hawaelewi nini kitatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ninukuu baadhi ya maeneo ambayo ameyasema Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, mwezi Desemba, 2012. Naomba uniruhusu niyanukuu. Mheshimiwa Mwakyembe alisema: "Ujenzi wa Bandari mpya ya Mwambani ambao haujaanza utaanza na wale wote ambao wanaubeza Mradi huu mwisho wake wataumbuka. Akaendelea kusema; hawa Wapinzani wanaobeza Mradi huu wa Bandari ya Mwambani Tanga wajue kwamba, wataumbuka kwani Mradi huo upo na ndani ya miezi sita ujenzi wake utaanza kwani kila kitu kipo tayari bado utekelezaji tu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni ya Waziri, namwamini sana ni mchapa kazi, lakini kinyume chake alikwenda Naibu Waziri na Gazeti la Mtanzania la Oktoba 3,

mwaka 2012, likatoa habari yake ikisema; Waziri apinga ujenzi wa Bandari ya Mwambani Tanga. Ninanukuu baadhi ya vifungu ambavyo alisema. Alisema: "Naibu Waziri wa Uchukuzi ameshauri Uongozi wa Mamlaka ya Bandari kuchukua hatua za haraka kuboresha Bandari ya Tanga ili kukabiliana na upinzani wa kibiashara. Ni vyema Bandari hiyo ikaboreshwa baada ya Mkoa huo kutumia muda mwingi kufikiria ujenzi wa Bandari mpya ya Mwambani. Ushauri huo aliutoa wakati alipotembelea Bandari ya Tanga na alisema kwamba, suala la ujenzi wa Bandari mpya ya Tanga ni la muda mrefu na utekelezaji wake unaonekana kuwa mgumu." Mwisho wa kunukuu maneno ya Mawaziri wote wawili wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Tanga wamekaa katika mkao ambao hawajui nini hatma ya bandari ile. Mimi napata shaka kwa sababu katika uhuru wa miaka 50 hadi leo bandari zilizokuwepo kubwa tatu, tama ya bandari ya nne ndiyo imepatikana hii ya Bagamoyo. Sasa sielewi kama uwekezano wa kujengwa kwa Bandari ya Tanga upo. Naomba Serikali iwaambie Wananchi wa Tanga ni nini, kwa sababu uongo umeshasemwa hapo kama ni ukweli wathibitishe; je, Bandari ya Tanga ipo kwenye mpango au ndiyo *kushinei*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuache ya bandari, nataka kuja katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini niende kwa Waziri wa Uwezeshaji, mama yangu Mheshimiwa Nagu, kwenye kifungu ambacho alizungumzia habari ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana *(YDF).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo yake Mheshimiwa Waziri na mimi naomba ninukuu kidogo; Mfuko wa Maendeleo ya Vijana *(YDF),* ulianzishwa na Serikali mwaka 1993. Lengo kuu la Mfuko huu ni kuwasaidia vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 35 kupata mikopo yenye masharti nafuu, kuwajengea uwezo wa kuibua Miradi yao ya Maendeleo kwa lengo la kujitegemea na kukuza uchumi wa nchi. Lengo zuri kabisa Mheshimiwa Waziri na mimi ninapongeza kwa malengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka 1993 mpaka mwaka 2003, Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana waliotarajia waweze kujiendeleza umepatiwa shilingi bilioni 1.2. Fedha hizo ukizigawanya kwa Mikoa 21 ambayo iliainishwa, kila Mkoa ulipata shilingi milioni 58 tu kwa miaka 20 na ukigawanya kwa kila mwaka kila Mkoa umepata shilingi milioni 2.8, hiyo ni pesa kwa kila Mkoa, Vijana wa Tanzania wajiendeleze. Hii ni dhihaka, huku ni kuwadhihaki Vijana wa Kitanzania na badala yake unawapa shilingi bilioni 1.2 Vijana wa Tanzania katika miaka 20, halafu unakuja kusema bilioni moja itengewe kwa wafu watarajiwa. Leo imekuwa wafu watarajiwa wana thamani zaidi katika nchi hii kuliko Vijana wa Tanzania. Hili halikubaliki na pesa hizi naomba Waheshimiwa Wabunge msikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa utamaduni wa Kiafrika hakuna mtu anayetaka miti yake achukue pengine. Tunayaona na hakuna hata mtu mmoja. Mimi nadhani hili suala la kuzungumzia habari ya Mfuko wa Makaburi ya wakubwa tuachane nalo na pesa hizi zielekezwe nguvu kwa Vijana. *(Makofi)*

Mhesimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa kuwa muda unakwisha, naomba kidogo niongelee Kitabu hiki cha CHADEMA, siyo Kambi ya Upinzani, sisi Wapinzani lakini hatuko humu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu na mimi nasema ninyi, kwa sababu wamezoea sana kuifanya Zanzibar ni kitambaa chao cha kujifutia mafua na sisi tunasema Wabunge wa Zanzibar tukiwepo hapa tukikubali hawa wainyanyase Zanzibar, tunapoteza maana, hatuwezi kukubali. Amekuja Mheshimiwa Mbowe hapa amejamba ameondoka, jana kaibukia Kibaha. Mnasema Wazanzibari wana udini, sisi Wazanzibari tunalingia dini yetu ya Kiislam, ni asilimia 98, nyamaza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwepo siku mtu anayeitwa Mchungaji akimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Zanzibar kuna udini kwa sababu wanawake wanakatazwa

kutembea uchi; huo ndiyo utamaduni wa Iringa? Wazanzibari hatuwezi kutembea uchi, kama hivyo ndivyo ...

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwambie akae, huyu ni mchungaji wa watu, mchungaji wa nguruwe! Mchungaji gani anahimiza tena anamwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu wa nchi ya Tanzania anamwambia kwa nini Wazanzibari wanakataza watu wasitembee uchi; huo ndiyo utamaduni wa kwenu? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha Rais wa nchi anapokwenda kwenye nchi anavyoonekana ndiyo mwonekano wa Wananchi wake na Mbunge wa Jimbo anapokuja hapa ndiyo mwonekano. Sitaki niamini kama Wananchi wa Iringa wana akili mbovu kama Mchungaji huyu! *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika.

**WABUNGE FULANI**: Hapo hapo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, ni kengele ya pili hiyo. Wabunge wawili nimewaona wakitaka miongozo na sitaruhusu zaidi ya hao wawili. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, tuanze na Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako; ninamheshimu sana Mbunge aliyepita na atambue kwamba, Taifa hili halina dini na hili ndilo tatizo la watu wa Zanzibar, ukigusa dini wanaleta

matatizo. Nchi hii hamuwezi kuifanya ya Kiislam hata siku moja, hii nchi ni ya Watanzania wote. Kwa sababu tukigusa mambo ya kidini mnataka ..., tunawaeleza ukweli nchi haina dini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, unatakiwa uongee na mimi, usiongee na watu wengine.

**MBUNGE FULANI:** Tunaelewa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema, tukiendelea kufumbia macho mambo haya ndiyo yanaligawa Taifa. Wazanzibari siku zote wao wakiguswa panauma. Watu wa Iringa ndiyo wananijua kama mimi ni mchungaji au siyo mchungaji, siyo wewe, nchi hii haina dini.

**NAIBU SPIKA:** Nimeshakuelewa kuhusu mwongozo wako. Nimeshakusikia mwongozo wako. Sasa Mheshimiwa Godfrey Zambi, mwongozo wa mwisho.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Natumia Kanuni ya 68(7), lakini nikirejea Kanuni ya 64(f) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni zetu za Bunge zinatukataza kutumia lugha ya matusi, lakini pia kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchungaji Msigwa alipokuwa anachangia hapa ndani ametumia Biblia kuwatukana Viongozi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia Biblia ndani ya Bunge kuwatukana Viongozi wa Serikali ni kuidhalilisha Biblia yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna Wakristo wanaosikia huko nje, kama kuna Wachungaji, Maaskofu na nani wanaosikia huko nje, wameona namna gani ambavyo

Biblia imedhalilishwa, kwa sababu sina hakika kama wanataka Biblia itumike kwa ajili ya kuwatukana Viongozi wa Serikali. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Omba Mwongozo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mwongozo ninaoomba; je, ni kitendo kinachoruhusiwa kutumia Biblia ndani ya Bunge kwa ajili ya kutukana Viongozi wa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako na kama ikiwezekana, Mheshimiwa Msigwa atoe au a-*withdraw statement* yake aliyotumia Biblia kwa ajili ya kutukana Viongozi wa Serikali, kwa sababu hata sisi Wakristo ndani ya Bunge tusingependa Biblia itumike kwa ajili ya kutukana Viongozi wa Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Muhammad Chomboh, endelea kuchangia. Mheshimiwa Wenje, kaa chini, hatuwezi kuendelea na mambo hayo. Wachangiaji sasa, nilisema ni wawili tu; Mheshimiwa Muhammad Chomboh.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa uwezo wa kusimama jioni hii. Pia ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wao wapo sasa hivi katika runinga wakiangalia kinachoendelea katika Bunge letu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba utulivu tuendelee kuwasikiliza wanaochangia.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Jambo ambalo naamini kabisa siyo wengi ambao walikuwa na mategemeo ya kitu kinachoitwa Upinzani ndani ya Bunge, walitegemea wapate Upinzani ambao utaleta tija na maslahi

ya nchi yao, badala yake kuna mambo ambayo hata mtu mmoja, Mtanzania mwenye uchungu na nchi yake, asingekubali kuyaona haya yanayotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kwanza ningeipongeza Serikali kwa kuona katika ukurasa wa 20 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuunda chombo kinachoitwa *President's Delivery Bureau,* kwa ajili ya ku-*counter check* uwajibikaji wa wafanyakazi wetu au wafanyakazi wa Serikali ili ku-*deliver* maendeleo yanayotokea au kila mmoja kazi aliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri na ni jambo zuri sana kwa maslahi ya nchi. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya na inaendelea kufanya, ingawa kuna Watanzania wenzetu wachache ambao tumewapa dhamana ya kuweza kufikisha malengo ambayo Serikali kwa nia safi tu, yaweze kuwaondolea matatizo wapate maslahi ya nchi yao kama Chama cha Mapinduzi na Serikali yake inavyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwao ndugu zangu hao ambao wanaturudisha nyuma wamo katika Serikali, lakini ndiyo wapo mwanzo kabisa kuilaumu Serikali hii kwa sababu tu ya Chama cha Mapinduzi na wao wakijifanyia vile ambavyo wao wanataka. Tuna ushahidi ambao tunauona sasa hivi na kikubwa zaidi, Watanzania walipokuwa wanataka kuwa na Vyama Vingi, walikuwa na nia nzuri sana ya kuweza kuki-*challenge* Chama cha Mapinduzi kiweze kuendelea zaidi na kupatikana maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake sasa kinachotokea humu ndani ni mambo ya ajabu sana. Ndugu zangu nilikuwa na mengi sana ya kusema lakini kila ninapowaangalia wasemaji wawili waliotangulia; Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Msigwa, kwa nia eti wao ni Wapinzani; hivi huu ni Upinzani gani; wa maslahi ya Tanzania au ni Wapinzani kwa maslahi binafsi? (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja hapa ndugu zangu kuna watu ambao wana mategemeo makubwa sana na sisi, mtu kama mchungaji ambaye kwa kawaida yake au kwa kawaida ya busara inavyotakiwa, uchungaji ni kuchunga watu kwa kutumia busara; lakini kuja na kitabu ambacho anakiamini yeye kwamba ni kitakatifu, anawatukana watu kwa kutumia kitabu hicho; ndugu yangu pale akawa anauliza wewe unachunga watu, unachunga nguruwe; ukweli huyu hata kuchunga nguruwe hafai! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawasikitikia sana watu wa Iringa tena ninawahurumia sana, Mheshimiwa Wenje anaiita Serikali *impotent;* sijui Kiswahili hiki! Mimi ni muungwana, kulitamka hili neno kwa Kiswahili maana yake ni hanithi, lakini sisi Wazanzibari tunasema hivi ...

**MBUNGE FULANI:** Hatujasikia.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Shazia au sindano haiwezi kushona kama hujaitunga uzi. Tumeelewana? Kama hujatunga uzi huwezi kushona. Sasa yeye ambaye anajifanya yeye sindano lazima atatungwa uzi ndiyo ashone, hii ndiyo tafsiri yake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawaambia ndugu zangu, wanachokitaka Watanzania ni upinzani wa maendeleo. Serikali yetu naiasa isimamie hiki kinachoamuliwa humu ndani ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Isimamie na ihakikishe inakwenda mpaka chini, kwa sababu miongoni mwa hao ambao wanawapa nafasi ya kuja kuzungumza ndiyo tuliowapa madaraka na wanakaa baa kututukana, wanakaa sokoni kututukana, leo mpaka Bungeni wanakuja kututukana; tunafanya nini? Tunawajibika ku-*deliver* na Serikali ichukue nafasi yake ya kusimamia jambo hili linatendeka na mtu awajibishwe kwa mujibu wa makosa ambayo anayafanya, tuache kuoneana huruma, tuache mambo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezoea kila siku kuleta mipango mizuri, tunasema kwamba fulani amekuja kuiga

kwetu, leo tumeshakuwa na *bureau* hii ya kuweza ku-*deliver,* hebu tuchukueni hatua. Watanzania hawataki kufanya kazi; kuanzia asubuhi, wiki nzima, wako mabaa tu kunywa na kulewa na kustarehe, leo sisi jambo kubwa sana tunapenda kuiga starehe za watu wengine *as if* Tanzania iko *above the world.* Tufanyeni kazi tubadilike na Serikali lazima isimamie, kuna wakati Mheshimiwa Mrema, alipokuwa Naibu Waziri Mkuu hapa, alipanga siku za kulewa na siku za kustarehe, lakini sasa kuanzia asubuhi wiki nzima watu wanakwenda. *(Makofi)*

Hivi sasa kuna kitu kimoja hiki tunachokiita Upinzani; mimi Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, namheshimu sana, lakini hapa sijui alipitiwa maskini; najua mwenzangu na mimi haoni mbele bila ya kuvaa miwani kama mimi, lakini hiki hakitaki miwani. Anasema: "Vilevile bado hakuna mwafaka juu ya uhalali wa idadi kubwa ya Wajumbe wa Katiba kutoka Zanzibar kushiriki."

Jamani, inapozungumzwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Muungano wa nchi mbili ikiwemo Zanzibar. Kinachoongelewa hapa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wazanzibari kwa nini wasishiriki *accordingly*, hapo watakuwa wanazungumza ndiyo baadaye watakapojua haya ya Tanganyika haya ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chomboh. Sasa ni Mheshimiwa Modestus Kilufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili la Watanzania lina imani kubwa sana na Wabunge. Watanzania wana imani kubwa sana na Wabunge na Serikali yao, lakini wana imani

kubwa sana na Watendaji mbalimbali wa Serikali kwa maana ya kuwatumikia. Ndugu zangu tusipoangalia, tutaendelea kulaumiana na pengine hata salamu itakosekana. Tatizo kubwa la nchi hii halitaisha kama hatutaimarisha uchumi wa nchi hii. Migogoro yote na migongano yote ya maendeleo kutokufikiwa katika nchi hii ni mahali pamoja tu, kutokudhibiti Uchumi wa Taifa ukakua ukafikia mahali ukaweza kukidhi haja ya Miradi ya Maendeleo na matumaini ya Watanzania kupata maisha yaliyo bora.

Ndugu zangu, lipo tatizo; kutokuwa na uchumi mzuri, ajira imekuwa ni tatizo katika nchi hii. Tumeshuhudia viwanda vingi ambavyo vilikuwepo vyote vimepotea, vimekufa kwa hoja tu ya kutaka kuwapa watu kutoka nje au ndani, wawekezaji ambao wameshindwa kuviendesha na hivyo kusababisha ajira kupungua kwa Watanzania. Si hivyo tu, hata ajira ambazo zinapatikana nazo zimeacha utaratibu wa kawaida. Wapo vijana vyuoni lakini wanapomaliza hawajui waende wapi, utaratibu uliokuwepo zamani ilikuwa akimaliza anaelewa amepangiwa anakwenda wapi; lakini sasa hivi kutokana na ukata imefika mahali inashindikana hata kuwapangia vijana pa kwenda na hivyo kufanya wakae mitaani wasijue cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri tunayoyafanya, kwa heshima kubwa naiomba Serikali na Wabunge wenzangu kwa ujumla na Watendaji mbalimbali wa Serikali mahali popote walipo hasa Wabunge wenye mamlaka, tufike mahali tutunge sheria ambayo itasaidia kudhibiti uchumi wa nchi usipotee. Bila ya kuweka miiko katika nchi hii, uchumi hautaimarika hata kidogo, utachezewachezewa kana kwamba nchi hii ni maskini, kitu ambacho siyo kweli.

Ifike mahala kama kweli tuna uzalendo wa kutosha tuweke miiko kwamba, yeyote atakayeingia mikataba mibaya ambayo atalisababishia Taifa hili kupoteza mapato yake, achukuliwe hatua za kinidhamu, ikiwezekana hata kifo. Tukifanya hivyo watu watafanya kazi kwa kuogopa. Sasa hivi watu wanafanya kazi bila woga katika nchi hii, kila mtu

mahali alipo anafanya anavyotaka akijua hakuna sheria inayombana. Hakuna Taifa lililoendelea ambalo halikuwa na miiko. Walijiwekea miiko yao na kwa utamaduni wa wenzetu, akikosea kidogo tu tayari anajiuzulu mara moja, ni miiko waliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa China wakati wa kuingia kwenye Shirikisho la Biashara Duniani kuhusiana na wakubwa, walifika mahali wakasema hapana sisi tutaamua tutakapoona tupo tayari. Wamekuja kuingia mwaka 2001 baada ya kuona sasa mambo yao yamekaa sawasawa. Huwezi wewe sungura ukasema unashindana na tembo hata kidogo. Nchi zote zilizoendelea mipango yao ni kuhakikisha sisi tutaendelea kubaki soko lao na tusipoangalia tutaendelea kubaki hivyo hivyo. Tufike mahali sasa na sisi tukubaliane mikataba ambayo italeta tija kwa Taifa hili, bila ya kufanya hivyo, nawaambia hapa hatutaelewana na nchi hii haiwezi kwenda hata kidogo. Tuweke miiko ndugu zangu Wabunge ya kulinda uchumi wa nchi hii. Bila ya kufanya hivyo, nchi hii itaendelea kuwa maskini na tutaendelea kuhangaika na nchi hii siyo maskini kama tunavyofikiria. Nilitaka niseme hilo ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao vijana wetu wengi wamekosa ajira, viwanda vimekufa, tumeshuhudia viwanda vya nguo tulivyokuwa navyo vimekufa, viwanda vya nyama na vya ngozi vimekufa, ajira hamna, tumeangalia mashamba makubwa ndiyo hivyo tena ajira hakuna. Tumeona vyombo kama vya Magereza vimekuwa ni mzigo kwa Taifa hili; kila siku watu wanapelekwa kwa kesi ambazo wala hazina kichwa. Serikali inaingia gharama kuwalisha watu ambao hawana sababu ya kukaa huko. Tuna vyombo vya Mahakama ambavyo mtu ukipelekwa pale kisheria, lakini tuna Mabaraza ya Kata yangeimarishwa, mambo mengi yangeishia kule wasingekwenda Mahakamani wakafungwe. Haya Magereza yangewekewa utaratibu ili Serikali isiendelee kuingia hasara. Yapewe utaratibu ambao hata wale wafungwa wakitoka pale waweze kwenda kujiajiri baadaye na kuwa Watanzania wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Mbarali. Naishukuru sana Serikali kwa kutusikia Wananchi wa Mbarali, suala la mpaka wa *TANAPA* kwamba sasa ramani ya kwanza ambayo ilichorwa mara baada ya Serikali kuchukua eneo lile ndiyo uwe mpaka na *GN* uwepo hapo na siyo kule kwenye mapendekezo ya Mkoa ambao ulikuja kumega ardhi ya Wananchi ambayo haikuwa na sababu ya msingi. Naomba niishukuru sana Serikali kwa kuwajali na kuwasikiliza Wananchi wa Mbarali; kwa hilo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Tunachongoja sasa hivi Wananchi wa Mbarali ni kuona mpaka ule ambao Serikali ilishauandaa toka mwanzo unawekwa *GN* tofauti na mpaka uliopendekezwa na mkoa ambao hauna maslahi kwa Wanambarali na wala kwa Taifa zima la Tanzania. Migogoro kama hii nawashukuru sana Viongozi ambao mmechukua nafasi ya Wizara hii nyeti, msimame imara kutatua migogoro yote katika nchi hii tukiachana na Mbarali. Wanambarali wanasubiria mpaka uwepo ambao utasaidia kuondoa kero mbalimbali ambazo wanazipata Wanambarali kwa kutokuwepo na mpaka na ile *GN* iliyowekwa kwenye mpaka uliopendekezwa na mkoa sasa iende kwenye mpaka ambao ulikubaliwa na Serikali toka ilipochukua lile eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Halmashauri chache katika nchi hii zilizopata Hati Chafu kutokana na ubadhirifu wa fedha zilizopelekwa kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa Wananchi zimetumika vibaya. Wanambarali wamenituma niiulize Serikali; Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nipate jibu utakapokuwa unajibu hoja.

Wananchi wanataka kupata mustakabali wa fedha zao zaidi ya shilingi bilioni mbili zilizoletwa Mbarali kwa ajili ya maendeleo sasa watu wachache wamegawana, wanataka kujua hawa watu wamechukuliwa hatua gani? Wanambarali wanataka majibu. Kaguzi mbalimbali zimefanyika, zote zinathibitisha kwamba kuna ubadhirifu wa fedha, wanataka kuona wale waliosababisha ubadhirifu, najua siyo wote; wamechukuliwa hatua, kwa nini kuna kitendawili hatua

hazichukuliwi? Wachukuliwe hatua hawa ili iwe fundisho na kwa Halmashauri nyingine zinazotumia fedha za maendeleo ya wananchi kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anapomaliza atoe tamko Wanambarali wasikie na zile fedha zilizopotea zinarudi vipi kwa Wananchi wa Mbarali. Haiwezekani sisi tukaadhibiwa kwamba tusipewe fedha za maendeleo kwa sababu ya watu wachache tena Watendaji wa Serikali waliohujumu fedha za maendeleo. Wananchi wa Mbarali wanataka jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbarali ni Jimbo ambalo limebahatika kuwa na Miradi mingi sana ya Kilimo cha Umwagiliaji. Naishukuru sana Serikali kwa kuona hilo na kweli bonde lile linafaa kwa kilimo. Wakulima wa Mbarali wameitikia wito huo, Miradi iliyopelekwa na Serikali tuliyosaidiwa inaendelea vizuri, mpaka sasa ninapozungumza tuna mpunga mwingi. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aje aone magodauni yalivyojaa mpunga mle ambao kwa sasa umekosa soko. Serikali imeagiza mchele kutoka nje, umeingia kwa wingi sana kiasi kwamba mpaka mchele wa ndani ya nchi ambao ni bora sana kuliko ule wa kutoka nje umekosa soko. Naiomba Serikali kama mliweza kuruhusu mchele mbovu kuingia nchini ambao haufanani na wa nchi yetu, basi mtutafutie vilevile mchele mwingine, huu mchele mzuri tupeleke huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na mambo yote niliyoyasema yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilufi, muda wako umeisha. Ahsante. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Rage ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKIMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, nipende tu kutoa pole kwa Wananchi wa Kata ya Nyachiluluma,

ambao walipata maafa kutokana na mvua kubwa ambayo ilinyesha, yenye upepo mkali sana na baadhi ya watu wakapoteza makazi yao na wengine wakafariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na Bajeti za Halmashauri. Kwa miaka mingi sasa tumekuwa tukipitisha bajeti hapa, lakini bajeti za maendeleo zimekuwa hazipelekwi kwa wakati mwafaka. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2012/13 katika Halmashauri ya Geita tulipanga shilingi bilioni 13 za maendeleo lakini mpaka sasa zimepelekwa shilingi bilioni 1.8 tu, kiasi kwamba, shughuli za maendeleo kule Geita hali ni mbaya sana. Mwaka huu kwa kuwa kuna mvua nyingi sana, barabara nyingi za vijijini hazipitiki; kwa mfano, Ilangasika kimekuwa kama kisiwa katika Kata ya Rwamgwasa. Vilevile kuna Kasungamile kutoka pale katika Kijiji cha Nyabulolo kuelekea Kamena, barabara hiyo haipitiki ni kwa sababu bajeti haziendi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bajeti tunazopitisha hapa katika Bunge hili hasa zile za maendeleo, tuhakikishe zinapelekwa kwa wakati ili Wananchi waweze kunufaika na kuweza kupata shughuli za maendeleo katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la maji katika Kanda ya Ziwa ni tatizo kubwa sana. Wenzetu ambao wako katika Mikoa ya Shinyanga na Kigoma ni sehemu zinazotarajia bomba la kutoka Ziwa Victoria. Sisi ambao tuko Kanda ya Ziwa penyewe; kwa mfano, Geita kuna vijiji ambavyo vinagusa Ziwa Victoria lakini vijiji hivi havina maji. Kwa mfano, Geita, Jimbo la Busanda, kuna vijiji kama vile Bukondo, Kasamwa, ambavyo vimegusa Ziwa Victoria lakini havina maji. Vilevile kuna vijiji ambapo ule Mgodi wa *GGM* wamechukua maji Nungwe kupeleka mgodini, wametoa Nungwe, kijiji ambacho hakina maji, bomba hili limepita Salagurwa hakuna maji.

Tunaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka mpango mkakati kwa ajili ya kuleta maji katika Kanda ya

Ziwa. Ikiwezekana wachukue maji katika Ziwa Victoria, kwa sababu kule sisi maji siyo tatizo, kuna Ziwa Victoria lipo pale; kwa nini Serikali isiweke mkakati wa kuweza kutoa maji Ziwa Victoria ili Wananchi waliozunguka Ziwa Victoria hasa Geita, Mwanza na sehemu zingine kama Mara na Bukoba, tuweze kupata maji safi na salama ili Wananchi wetu waweze kunufaika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kuhusiana na suala la madini. Nilikuwa nikisoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeangalia katika ukurasa wa 42 ambao unazungumzia Sekta ya Madini. Nimejaribu kuangalia Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba, wameweka mpango mzuri kabisa na mkakati na programu ya mafunzo, pamoja na kuwatengea maeneo wachimbaji wadogo wa madini. Cha kusikitisha, nimeangalia kuanzia mwanzo wa bajeti mpaka mwisho, lakini sijaweza kuona kwa upande wa Geita. Watu wa Nyarugusu, wanayo tabu, hawana maeneo ya uchimbaji. Ni miaka mingi sasa kila mwaka nikisimama katika bajeti nazungumzia Wananchi wa Nyarugusu kupewa maeneo ya kuchimba. Kwa hiyo, niombe tu sasa kupitia bajeti hii, niiombe Ofisi ya Waziri Mkuu, waangalie uwezekano wa kuweza kuwapatia Wananchi maeneo ya kuchimba. *(Makofi)*

Vilevile hata wale ambao walipata kama watu wa Rwamgasa walipewa maeneo ya uchimbaji pamoja na Mgusu. Naomba kituo cha kuwawezesha wachimbaji wadogo ambacho kilitarajiwa kujengwa Rwamgasa, ni miaka mitatu sasa mipango imepangwa lakini hakuna utekelezaji unaoendelea.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali iweke uwezekano mkubwa wa kuanzisha kituo hiki. Kila ninapokwenda, Wananchi wananiuliza kwamba hiki kituo kinaanza lini, mimi sina majibu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, anapomalizia aseme sasa ikiwezekana labda Wizara ya Nishati na Madini wawaambie Wananchi wa Rwamgasa na Wananchi wa Geita kwa ujumla kwamba, wanaanzisha kituo hiki lini. Wakiwezeshwa hawa wachimbaji

wadogo, nina uhakika hata masuala ya watu kugoma hayatakuwepo na hakutakuwa na migomo ya aina yoyote, kwa sababu Wananchi watakuwa na shughuli zao, zitakazowapatia kipato chao bila matatizo yoyote.

Vilevile kwa upande wa nishati, nichukue nafasi hii kushukuru sana Serikali kwa umeme wa *MCC*, ambao tayari sasa nguzo zimeenea Bukoli, Rwamgasa kule pamoja na Nyarugusu, Bukondo sehemu za Chigunga, Katoro kote huko kuna nguzo za umeme. Swali ambalo Wananchi wamekuwa wakiniuliza ni kwamba; sasa mbona umeme huu unapita juu kwa juu, nguzo hazipiti kwenye vituo vya afya wala shule za sekondari na wala katika vituo vya polisi. Kwa hiyo, niombe tu kwamba, katika bajeti hii Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka umeme huu katika sekta muhimu kama vituo vya afya, zahanati na shule za sekondari ili Wananchi wote waweze kunufaika na huduma hii ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine muhimu kabisa ni la mikoa mipya. Geita ni mkoa mpya, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia mkoa mpya ili kuweza kuleta huduma karibu na Wananchi na mikoa mingine ya Simiyu na Katavi. Niombe tu, kwa sababu mikoa hii ni mipya inahitajika miundombinu ya kutosha, bila miundombinu ya kutosha watumishi hawawezi kufanya kazi zao kwa ufanisi. Kwa hiyo, niombe hizi bajeti tulizopanga za mwaka huu haziwatoshi. Nikiangalia Mkoa wetu wa Geita mwaka jana tulikuwa na watumishi 12, leo tuna watumishi 80, lakini bajeti ya *OC* ni ile ile. Kwa hiyo, naiomba Serikali iongeze bajeti na vitendea kazi havitoshi. Geita pale tuna magari mawili tu na gari la Mkuu wa Mkoa limekuwa *written-off* limepata ajali. Kwa hiyo, naiomba Serikali iiwezeshe mikoa hii mipya ili waweze kufanya kazi zao vizuri kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala muhimu la fedha ambazo tulizitenga mwaka jana kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya mikoa mipya hasa Geita kule, mpaka sasa fedha hizi hazijafika katika mikoa hii. Kwa hiyo, nipende tu kuiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, wakati wa hitimisho tuweze

kusikia kwamba hizi fedha zinakuja lini ili shughuli za ujenzi kwa mikoa mipya ziweze kuanza.

Nichukue nafasi hii kusema kwamba, Serikali ituangalie watu wa Kanda wa Ziwa, itupatie maji. Wananchi wanateseka sana na naendelea kusisitiza, maji ni uhai kwa hiyo tunahitaji maji ya kutosha. Wananchi wanauliza kila siku mbona ziwa lipo hapa Serikali inashindwa nini kuleta maji. Naiomba Serikali, kipaumbele ni maji. Wananchi wakiulizwa kipaumbele cha pili ni maji, kipaumbele cha tatu ni maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ijikite katika suala la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, umewasomesha Wabunge wengi ambao hawajui kuchangia kama Wabunge wa Majimbo, namna gani ambavyo unaweza kutetea hoja za Wananchi.

Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Ismail Aden Rage.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa msaada mkubwa alionipatia kule kwenye Jimbo langu, kunipa tani 353 za chakula, lakini kuna janga lingine ambalo limetokea pale, naomba vilevile mnisaidie; kuna mapigano yalitokea ya wakulima na wafugaji, wafugaji wakachomewa nyumba zao 16 na mifugo 103. Kwa hiyo, chakula cha msaada mlinipa lakini huku tayari kumetokea janga lingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu wewe ni msikivu na unajali sana maslahi ya vijana wako, naomba uwaangalie wale wafugaji ambao nyumba zao 16 zimechomwa moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nataka nianze kwa Halmashauri zote nchini. Naomba kuwepo na utaratibu wa Halmashauri kuajiri wafanyakazi wakiwemo na Waheshimiwa Madiwani, badala ya kila mfanyakazi kutegemea mtuletee kutoka TAMISEMI. Mnapotuletea, wakifanya maovu badala ya kuwafukuza na kuwafungulia mashtaka mnawahamisha, matokeo yake Halmashauri zinabaki katika janga la gharama kubwa sana ya matumizi ya pesa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala limekuwa gumu sana kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, Halmashauri nyingi zimekuwa zina watumishi lakini watumishi hawa wanakaimu kwa muda mrefu. Kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Korogwe, kuna Wakuu wa Idara wanakaimu zaidi ya miaka minane. Sasa Wakuu wa Idara hawa wanaokaimu wanashindwa kutoa maamuzi, matokeo yake Halmashauri zetu zinazidi kudidimia na hatimaye zinapata Hati Chafu. Sababu ni woga wa kuhodhi yale madaraka. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba uwaachie watumishi waajiriwe watufanyie kazi wakiwa wanajiamini kabisa kwamba wamepewa madaraka na wanafanyakazi pasipo na matatizo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Tender Board*, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tushirikishwe Wabunge pamoja na Madiwani wote nchi nzima. *Tender Board* imekuwa ni kero kubwa kwa Wananchi hasa wa chini. Kwenye Jimbo langu kumetokea mtu ka-*tender,* amechukua madaraka ya kukusanya mapato katika Halmashauri ya Korogwe Vijijini lakini utashangaa, yule bwana badala ya kukusanya madeni anawatia hasara wafanyabiashara kiasi ambacho hivi sasa mfanyabiashara anaambiwa lipa gharama za nyuma, akikataa kulipa analetewa bili ambayo haijawahi kutokea hata siku moja.

Amefika mahali mfanyabiashara analipa shilingi milioni 49 na wafanyabiashara hawahawa ndiyo ambao wananisaidia mimi wakati nikipata matatizo kwenye Jimbo langu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala la *Tender Board*

kuwaachia watu wachache wasimamie Miradi hii ni uonevu na kutokutendewa haki sisi Wabunge pamoja na Waheshimiwa Madiwani. Tunaomba hao wote wanaoelekeza kwenye *Tender Board* na sisi tuwepo tuangalie mikataba inasemaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mkuu wangu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe Vijijini, ametusaidia sana kiasi cha kuyaweka mazingira haya safi. Kinyume cha hapo, nina wafanyabiashara zaidi ya 20 wanapelekwa Mahakamani na huyu mwenye *tender* anachukua hela hizo anaziingiza kwenye akaunti yake, Halmashauri kila mwezi anaambiwa atoe shilingi milioni 2.3, lakini wafanyabiashara hao wanalipishwa hela ambayo haijawahi kutokea. Haya yametokea Mombo, haya yametokea kwa Wafanyabiashara wa Hale, Mashewa, Bungu na Wafanyabishara wa Magoma. Sasa wafanyabiashara hawa tukiwa na shida ndiyo tunakwenda kuwalilia. Leo hii mtu anakuja, badala ya kuingiza mapato haya kwenye akaunti ya Halmashauri, anaziingiza kwenye akaunti yake. Huu kama siyo wizi ni nini? Naiomba Serikali yako Tukufu ambayo ni sikivu sana waliangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taratibu moja ambayo imeendelea sana, kwa mfano, Halmashauri nyingi zimetajwa hapa na Wilaya zimepandishwa hadhi, lakini nasikitika sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wengi wamekuja kujifunza katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mombo. Hii Mombo kuwa Halmashauri ya Mji ni kitu gani tumekosea watu wa Korogwe? Hebu tunaomba tuelewe; kila waliyejifunza pale Mombo Mamlaka ya Mji wamekuwa Halmashauri ya Wilaya. Leo Mombo kuna tatizo gani? Kila linapotokea Mombo siisikii nataka mniambie katika majumuisho kwamba hii Mombo ni lini itakuwa Halmashauri. Kinyume cha hapo mimi kama Mbunge wa Jimbo lile mnaniweka katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa wakati huo alikuja mpaka kwenye Kata ya Kizara akawaahidi wananchi wa Kizara kwamba ikifika mwaka 2012 Mawasiliano katika

Kata ya Kizara yatakuwepo. Lakini cha kushangaza mpaka leo hii hakuna mawasiliano ya aina yoyote wala hakuna utaratibu wa aina yoyote. Kwa hiyo matatizo haya yamejitokeza Kizara, yametokea kule Kigwasi Kalalani kule ambako kunatoka madini hakuna mawasiliano yamejitokeza Chekelei katika sehemu ya Usambala, hakuna mawasiliano kabisa. Wananchi kila siku wananiuliza Mbunge ulivyokuja uliahidi kwamba mawasiliano yatapatikana. Leo hii nashindwa hata kwenda kufanya mkutano wa hadhara. Serikali yangu tiifu, ambayo inajali sana maslahi ya wapigakura, naomba nijue hiki kilio kikubwa sana kwa sisi ambao tumechaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo; katika Jimbo langu limezunguka sana na mashamba ya mkonge na Mkoa mzima wa Tanga mnajua umezungukwa na mashamba ya mkonge lakini kuna mashamba yanayoendelezwa na mashamba mengine hayaendelezwi na kila siku ugomvi huo wa wakulima na wafugaji unasababishwa na mashamba ya mkonge. Hebu watengeni hawa watu, yale mashamba ambayo hayaendelezwi wapewe wananchi. Kila siku tukija Bungeni tunazungumzia mashamba, kila tukija Bungeni tunazungumzia mashamba, mashamba hayo wengine badala ya kuyaendeleza wanapanda majani ya ng'ombe; badala ya kuyaendeleza wanapanda mahindi; kama ni mahindi basi wapewe wananchi.

Kuna mashamba makubwa sana Mkoa wa Tanga. Leo hii sisi Wabunge wa Mkoa wa Tanga tumekuwa ni kero tunaonekana hatuwasemei. Sasa Serikali ambayo ni sikivu kila siku tunaambiwa hati ziko mezani kwa Mheshimiwa Rais, hizi ni hati gani ambazo ziko miaka yote hii? Mnatuweka kwenye mazingira gani sisi Wabunge, tutakwenda kuwaambia nini wananchi?

Naomba kuna masuala mengi sana kuhusiana na mashamba haya haswa Bonde la Mkomazi. Mheshimiwa Rais alipokuja aliahidi kwamba Bonde la Mkomazi litafanyiwa upembuzi na kutakuwa na maji. Nashukuru Serikali imenipa milioni 300, lakini milioni 300 kwa Bonde la Mkomazi hazitoshi.

Naomba Serikali katika majumuisho waseme Bonde la Mkomazi mnaliongezea kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji; Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la maji katika Jimbo langu ni kero kubwa sana na bahati nzuri hata Naibu Waziri alikuja kule akatupa matumaini makubwa sana lakini suala hili limekuwa hakuna maji katika Mkoa wa Tanga na vyanzo vya maji viko vingi. Kwa mfano, Kerenge, tumekwenda katika msitu unapewa masharti magumu ya kuchukua maji. Maji tu bila kukata msitu unapewa masharti magumu.

Benki ya Dunia imekuja, watu wanatakiwa wapewe misaada lakini kwangu mimi nasikia Benki ya Dunia kwa wenzangu tu, kwangu siisikii, lakini naambiwa kuna hela zimetengwa, hizi hela ziko wapi? Mimi kama Mbunge mbona sizijui, kama zipo zifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo wa Waswahili wanasema hivi ukiwa mwongo ujanani, uzeeni utakuwa mchawi. Kwa hiyo, sasa sitaki kuwa mchawi. Huu ni msemo, kuna sehemu kama Magoma hakuna maji, Mombo hakuna maji, Kata ya Magamba kwa Lukonge hakuna maji na nimewaahidi Wananchi kwamba Serikali itachimba kisima maji hakuna. Hii imekuwa ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Ismail Aden Rage.

**MHE. ISMAIL A. RAGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote, ningependa kunukuu kitabu cha Marehemu Shaaban Robert ni mtaalam sana wa Lugha ya Kiswahili kuliko sisi sote tuliomo humu ndani. Kitabu chake cha Kusadikika anasema haya: *"Ni bora mtu kuwa maskini wa fedha kuliko kuwa maskini wa maarifa."* Mambo mazuri yanayofanywa na Serikali ya CCM wenzetu hawa hawayaoni, mimi naomba tuwasamehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kujikita kwenye mambo matatu au manne muhimu yanayohusu Manispaa yangu ya Tabora na Mkoa mzima wa Tabora. Napenda kumpongeza kwanza Mkuu wangu wa Mkoa, katika Mkutano wa *RCC* tarehe 11 Machi, 2013, tulipokuwa tunaongea juu ya matatizo ya barabara zetu za Tabora; Barabara za Tabora ambazo zinatakiwa ziwe na lami, kwa mfano Barabara ya Tabora - Urambo ilitakiwa tukabidhiwe tarehe 4 Januari, 2013, imechelewa kwa zaidi ya miezi 20 mpaka leo hatujakabidhiwa na hatujui tukabidhiwa lini. Barabara ya Tabora kwenda Ndono, ilikuwa tukabidhiwe tarehe 3 Septemba, 2012 hatujakabidhiwa mpaka leo. Barabara ya Tabora - Nzega tulitakiwa tukabidhiwe tarehe 2 Aprili, 2013 na kweli ninao ushahidi wa *Hansard* ambayo niliuliza maswali mwaka 2011, 2012 na mwaka huu pia na majibu niliyopata ni kwamba, barabara hizi zitajengwa na zitakwisha kwa wakati wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapokuwa anatoa hoja yake atuhakikishie Wananchi wa Tabora hizi barabara zitakwisha lini. Jana nimerudi kutoka Tabora, kuna maafa makubwa yametokea Tabora, sasa hivi huwezi kutoa mzigo wa aina yoyote kutoka Dodoma au Dar es salaam kupeleka Tabora. Pale Kizenga maji yamekata barabara, kuna mabasi na magari ya mizigo yasiyopungua 150 yako pale. Barabara ya kutoka Nzega kwenda Tabora, Kimiziwa, maji yamechukua barabara nzima. Nimepita kwa tabu jana mahali panaitwa Simbo, ilibidi kwanza tupite kwa miguu halafu ndiyo tupite kwa gari dogo. Hali ya Tabora sasa hivi inatisha. Ninaomba tafadhali, Mkoa wa Tabora una heshima yake katika nchi hii, tusidharauliwe hata kidogo; ni moja kati ya Mikoa michache katika nchi hii umetoa Wabunge 11 wote wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule inaitwa *Tabora Boys Secondary School,* katika nchi yoyote ile tumekuwa na tabia wanasiasa wote hata hawa wadogo ambao hawamjui vizuri Mwalimu, kutoa mifano yake na kumtukuza kila wakati. Mimi nasema hamtukuzi Mwalimu. Mwalimu, Marehemu,

Mungu amuweke mahali pema, elimu yake aliyoipata ameipata *Tabora Boys;* lakini nenda kaangalie hali ya *Tabora Boys* inatisha.

Wamarekani wana Chuo chao kule Atlanta kinaitwa *Morehouse University,* alisoma yule mkombozi wa watu weusi, Dkt. Martin Luther King, kile chuo kimetukuzwa kiasi cha kwamba, tarehe 19 mwezi ujao, Rais Obama anakwenda pale kutunuku shahada kwa wanaomaliza shule. Sasa sisi Tabora, licha ya kuwa na *Tabora Boys* ni mji ambao Azimio la Kupata Uhuru wa Tanganyika Kura Tatu lililofanyika katika Ukumbi wa *Parish Hall* mwaka 1958, halafu Tabora bado haitakiwi kuangaliwa katika hali inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea kwa uchungu sana kwa sababu nimelalamika sana kila ninapochangia hasa Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee tatizo la maji. Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alituahidi pale Tabora kwa awamu mbili; kwenye Sherehe za kina mama na alipokwenda kuomba kura za Wananchi kwamba, tutapata maji kutoka *Lake Victoria* pale Ihelele. Nimepata bahati ya kufika pale Ihelele na shahidi ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji, tumekwenda pamoja, ilibidi kumfuata Mwanza mwenyeye nikampokea tukaenda mpaka pale. Mradi ule ni mkubwa kuliko Mradi wowote wa maji katika Bara letu la Afrika, wa pili ni ule wa Cape Town. Jambo la kushangaza, pale pana uwezo wa kuzalisha maji kwa siku moja lita milioni 120, lakini maji yanayozalishwa sasa hivi katika Mji wa Kahama na Shinyanga ni lita milioni 17 tu. Kuna *access* ya milioni 103, tunapoteza pesa zetu bila sababu yoyote.

Serikali iliwekeza pale shilingi bilioni 283. Niliongea mwaka jana na katika bajeti ya mwaka jana Serikali ilitenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kufanya *feasibility study*. Hivi *feasibility study* toka mwaka jana mpaka mwaka huu, huo uchunguzi gani unaofanywa? Kwa mujibu wa Sheria za nchi, *tender* ikitangazwa kimataifa inachukua siku tisini. Sasa sijui

hii *tender* inayotangazwa inachukua zaidi ya siku 356 kwa Kanuni ipi? Nitaomba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anapoongea, suala hili atuhakikishie Wananchi wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Maji ya kutoka *Lake Victoria* yatasaidia Igunga, yatasaidia Wilaya ya Nzega, yatasaidia Wilaya ya Tabora Mjini, yatasaidia Wilaya ya Urambo na yatasaidia Wilaya ya Sikonge. Kwa mujibu wa kumbukumbu za kitaalam, Mkoa wa Tabora wanasema ni *semi-arid*, huwezi ukachimba chini ya ardhi ukapata maji na kama utayapata utapata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Mamlaka za Maji za Miji. Tabora tuna Mamlaka ya *TUWASA,* inafanya kazi nzuri sana. Nilipochaguliwa maji yalikuwa yanatoka lita milioni nane kwa siku. Leo ndani ya miaka miwili na nusu, *TUWASA* wameweza kutoa maji lita milioni 16. Kinachosikitisha, pesa ambazo wanadai kwenye huduma wanazozitoa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi na Jeshi la Kujenga Taifa ni zaidi ya shilingi milioni 640. Shirika dogo kama hili litakwenda namna gani? Namshukuru sana Profesa ameandika barua kwa Waziri wa Fedha, akiomba kwamba angalau Wizara ya Fedha iingilie kati tuweze kulipwa hizo pesa Shirika langu la Tabora liweze kuwa Shirika bora hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009 Bunge lako Tukufu lilitengeneza Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maji wa Taifa. Napenda niwakumbushe kama wamesahau, ni Sheria namba 44, lakini jambo la kusikitisha leo ni mwaka wa nne ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rage!

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii bila wasiwasi wowote. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. Nakuona Mheshimiwa umesimama; haya ruksa kwa dakika moja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68 (7) inayosema: "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo ama baadaye atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge aliyemaliza kuongea, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kuna jambo ambalo amelifanya naomba mwongozo wako kama linaruhusiwa, la kutumia vitabu vitakatifu ndani ya Bunge lako Tukufu. Kwa sababu ametumia Biblia na humu tuna madhehebu mbalimbali; je na *Quran* inaruhusiwa kuingia ndani ya Bunge hili Tukufu?

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. EZEKIA D. WENJE**: Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, haya wa mwisho kabisa huyo. Mheshimiwa Wenje kwa nusu dakika na Mheshimiwa Mfutakamba umesimama? Samahani, sana Kiti change mara nyingi tunakupunja sana. Baada ya Mheshimiwa Wenje dakika moja.

**MHE. EZEKIA D. WENJE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 64 (g). Naelewa kwamba, tunapozungumzia masuala ya imani tunakuwa *very emotional* na wakati mwingine tunaweza tukawa *carried away* na tukasema maneno mengi ambayo mengine yanaudhi. Kwa heshima kubwa, ni hatari sana mijadala hii inapoelekea na mwongozo ... *(Kicheko)*

*It is okay*, ninyi mnaweza mkapuuza kwa sababu hamwoni kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ninaouomba, rafiki yangu Mheshimiwa Khatib, Mbunge wa Konde, alivyokuwa anazungumza amediriki kutumia lugha ambazo hazistahili kutumika hapa Bungeni kwa kusema, akasema na mlisikia wote kwamba, Mheshimiwa Mbowe alikuja hapa akajamba halafu akaenda. Sasa naomba nimalizie kwa kusema, inasikitisha sana kama hawa watu wenye umri kama huu wanafurahia maneno ya kitoto kama haya. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA**: Nakushukuru Mheshimiwa Wenje. Kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Mfutakamba ni wa mwisho. Naomba tumsikilize.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 64(f) na (g), nisome tu; "(f) Mbunge yoyote hatasema vibaya au kutumia lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote; (g) Hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Wenje wakati akitoa matamko yake anasema Serikali hii ni ya mahanithi (*impotent)*. *Impotent* tafsiri yake ni mahanithi. Mheshimiwa hapa tuna viongozi wana wajukuu wana watoto pengine kuzidi yeye. Naomba afute kauli yake, naomba mwongozo wako huwezi kusema lugha kama hiyo Bungeni.

**MBUNGE FULANI**: Au tutamshughulikia Bwana Wenje.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kelele zote humu ndani zinaonesha jinsi ambavyo sasa mnazifahamu Kanuni na mnaona kabisa pale mahali ambapo Kanuni zinakuwa hazizingatiwi. Moja ya maeneo ambayo mara nyingi sana tumesimama na kusisitiza ni eneo hili la kuwa na lugha ya staha ndani ya Bunge. Kwa manano mafupi tunaita lugha ya Kibunge. Yapo maneno hutarajiwi Mheshimiwa Mbunge kuyatamka. Sasa hii ni Wizara ya kwanza katika

mlolongo ambao ninyi mnafahamu katika zoezi zima ambalo tunaendelea nalo la Bajeti litakalochukua hadi mwezi wa sita mwisho. Sasa Wizara ya kwanza tukianza kwa lugha hizi, mimi sina hakika kama tutafika mwisho. Wako Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamezungumzia matatizo ya Wananchi, wamefikisha hoja kwa heshima, kwa ustaarabu na hao nawapongeza sana. *(Makofi)*

Ni jambo lisilofichika kwamba, wapo wengine ambao walisamama wao lengo lao lilikuwa ni kukashifu na kutukana na kutumia maneno yoyote yale ya kuudhi sijui kwa madhumuni gani. Sasa niseme tu kwamba, hizi kesi ukizitazama ziko nyingi zinazojirudia. Mimi kwa hatua hii, nitoe karipio kwa wote ambao wamekuwa wanajihusisha na lugha ambazo hazikubaliki humu Bungeni na niwaambie Wananchi wanatusikiliza na hawafurahishwi hata kidogo na hiki kinachoendelea. Nafikiri hata wale waliokuwa wanatetea kwamba, Bunge liwe *live,* sasa wanatuelewa kwa nini baadhi walikuwa wakifikiri kwamba iko haja ya kuwa na aina fulani ya mchujo ili kuondokana na baadhi ya vitu ambavyo vinaenda ambavyo havikupaswa kuwepo hata mara moja.

Sisemi kwamba hilo ndilo lengo la Bunge, hapana; lakini niseme kwa kweli tunawaomba sana Waheshimiw Wabunge, mmesikia Wabunge wanaowakilisha matatizo ya Wananchi wanazungumza vipi, tuwaige hao. Hatujaja hapa kutukanana, hatujaja hapa kuvunjiana heshima, dakika zenyewe chache, tano au kumi; wasilisha matatizo ya Wananchi.

Kwa hiyo, huo ndiyo mwongozo wangu kwa wote kabisa waliohusika na waliotajwa, sina haja ya kurudia jina moja moja kwamba tujichunge kuanzia sasa, tuendelee kufanya kazi yetu ya Kibunge kama Wabunge. Meza hii haitasita kuchukua hatua za kinidhamu kuanzia sasa kwa wale ambao wataendelea na tabia ya kutumia maneno ambayo hayakubaliki katika jamii ya Kitanzania hivihivi kirejareja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muda wetu ulipofika, sasa naomba kwa heshima na taadhima, niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 16 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*